**20 JUNI, 2023**

**BUNGE LA TANZANIA**

---

# MAJADILIANO YA BUNGE

---

## MKUTANO WA KUMI NA MOJA

**Kikao cha Hamsini na Moja – Tarehe 20 Juni, 2023**

*(Bunge Lilianza Saa Tatu Asubuhi)*

**D U A**

*Mwenyekiti (Mhe. Daniel B. Sillo) Alisoma Dua*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa tukae.

Katibu.

**NDG. RUTH MAKUNGU – KATIBU MEZANI:**

**MASWALI NA MAJIBU**

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa tunaanza Ofisi ya Rais - TAMISEMI namwita Mheshimiwa Florent Laurent Kyombo Mbunge wa Nkenge sasa aulize swali lake.

Na. 664

**Hitaji la Hospitali ya Wilaya – Misenyi**

**MHE. FLORENT L. KYOMBO** aliuliza: -

Je, ni lini Serikali itatenga bajeti ya ujenzi wa Hospitali ya Wilaya pamoja na Vituo vya Afya Misenyi?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri Ofisi ya Rais, TAMISEMI Mheshimiwa Deo Ndejembi majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DEOGRATIUS J. NDEJEMBI)** alijibu: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Florent Laurent Kyombo, Mbunge wa Jimbo la Nkenge, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka wa fedha wa 2021/2022 na hadi kufikia Mei, 2023 kiasi cha shilingi bilioni 1.5 zimekwishatumika katika ujenzi wa majengo saba ya Hospitali ya Wilaya ya Misenyi na kiasi cha shilingi milioni 500 kilitengwa kwa ajili ya ujenzi wa Kituo cha Afya cha kimkakati cha Kanyigo kilichopo katika Halmashauri ya Wilaya ya Misenyi. Aidha, katika mwaka wa fedha wa 2023/2024, Serikali imetenga shilingi milioni 800 kwa ajili ya kuendeleza ujenzi wa Hospitali ya Wilaya ya Misenyi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali itaendelea kutenge bajeti kwa ajili ya ujenzi na ukamilishaji wa miundombinu msingi katika hospitali na vituo vya afya kote nchini vikiwepo vya Halmamashauri ya Wilaya ya Misenyi.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Laurent swali la nyongeza.

**MHE. FLORENT L. KYOMBO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nipongeze kwa majibu mazuri ya Serikali, na ni kweli majengo saba yamejengwa. Naomba kuuliza maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la kwanza, katika majengo hayo hatuna wodi ya watoto, akina baba, akina mama pamoja na *theatre*;

Je, ni lini sasa wodi hizo zitajengwa?

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini la pili, ili hospitali hiyo iendane na kutoa huduma ya haraka kama ambavyo *speed* ya ujenzi imeenda inahitaji kuunganishwa na barabara ya lami ambayo iliahidiwa na kiongozi wa kitaifa.

Je, na barabara hiyo ambayo iko chini ya *TARURA* ni lini itajengwa kwa kiwango cha lami kuelekea katika hospitali iweze kutumika itakapo funguliwa?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DEOGRATIUS J. NDEJEMBI):** Mheshimiwa Mwenyekiti, nijibu maswali mawili ya Mheshimiwa Kyombo, la kwanza hili la kutokuwa na wodi ya watoto, akina baba na *theatre* vile vile katika Hospitali ya Wilaya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama ambavyo nilikuwa nimeshasema kwenye majibu yangu ya msingi kwamba Serikali imetenga shilingi milioni 800 katika mwaka wa fedha wa 2023/2024 ambayo itakwenda kwa ajili ya kuendeleza ujenzi wa Hospitali hii ya Wilaya ya Misenyi na watapata wodi ya watoto, baba na vilevile *theatre*. Ni lengo la Serikali hii ya Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan kuhakikisha kwamba miundombinu katika sekta ya afya ipo ya kutosha kwa ajili ya kutoa huduma kwa wananchi wa nchi hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikienda kwenye swali lake la pili la barabara inayounganisha hospitali. Barabara hii ina urefu kama wa kilomita nne kutoka kwenye barabara kuu inayokwenda Mtukula ambayo ni barabara ya *TANROADS*. Hivyo naomba nichukue nafasi hii mbele ya Bunge lako Tukufu kumwelekeza Meneja wa *TANROADS* Mkoa wa Kagera kwenda kufanya tathmini ya barabara hii na kuiweka katika mipango yetu kwa ajili ya kutafuta fedha na kuweza kuijenga ili wananchi waweze kufika hospitali kupata huduma za afya kwa wakati.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Omari Kigua, swali la nyongeza.

**MHE. OMARI M. KIGUA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana. Kwanza niipongeze Serikali ya Chama Cha Mapinduzi kwa kutujengea Vituo vya Afya kwenye tarafa tatu. Tuna tarafa nne Wilaya ya Kilindi lakini tuna Tarafa moja ya Kimbe

haina kituo cha afya na umbali kutoka tarafa hiyo hadi Makao Makuu ya Wilaya ni takribani kilomita 120;

Je, nini mpango wa Serikali wa kujenga kituo cha afya kwenye tarafa hiyo? Ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DEOGRATIUS J. NDEJEMBI):** Mheshimiwa Mwenyekiti, nijibu swali la Kigua Mbunge wa Kilindi, kwamba Tarafa ya Kimbe haina na kituo cha afya. Serikali imetenga mwaka wa fedha uliopita zaidi ya bilioni 117 kwa ajili ya ujenzi wa vituo vya afya vya kimkakati kote nchini ambapo vingine vilikwenda kwa Mheshimiwa Kigua kule Kilindi. Tutakaa na Mheshimiwa Kigua kuona hii Tarafa ya Kimbe nayo tunafanyaje ili iweze kutengewa fedha kupata ujenzi wa kituo cha afya kama vile kata ya kimkakati ili hizi kata zote zinazozunguka tarafa hii ziweze kupata huduma nazo za afya.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Profesa Ndakidemi, swali la nyongeza.

**MHE. PROF. PATRICK A. NDAKIDEMI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa fursa. Tunaishukuru sana Serikali kwa kutujengea Kituo cha Afya cha Uru Kusini na kinakaribia kinakamilika;

Je, Serikali ina mpango gani kupeleka vifaa na wahudumu ili wananchi waanze kupata huduma?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DEOGRATIUS J. NDEJEMBI):** Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali katika mwaka huu wa fedha 2022/2023 imeajiri watumishi wa afya wapatao 8,000 ambapo wengine watapangiwa katika Halmashauri ya Moshi Vijijini anapotoka Prof. Ndakidemi kule. Lakini vile vile katika mwaka wa fedha 2023/2024 Serikali imeweka kwenye bajeti shilingi bilioni 112 kwa ajili ya

ununuzi wa vifaa tiba. Vitakapo nunuliwa tutahakikisha na Moshi Vijijini napo kwa Mheshimiwa Profesa Ndakidemi nao wanapata vifaa tiba hivi.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Kikoyo, swali la nyongeza.

**MHE.OSCAR I. KIKOYO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana. Wilaya ya Muleba ni Wilaya kongwe hapa nchini lakini haina hospitali ya Wilaya na mwaka jana Mheshimiwa Rais alitupatia fedha kuanza ujenzi wa hospitali hiyo.

Je ni lini sasa ujenzi utakamilika wa Hosoitali ya Wilaya ya Muleba?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DEOGRATIUS J. NDEJEMBI):** Mheshimiwa Mwenyekiti, ujenzi wa Hospitali hizi za Wilaya huwa unaenda kwa awamu na fedha hutolewa kwa awamu.

Awamu ya kwanza hutolewa milioni mia tano ama wakati mwingine bilioni moja kwa ajili ya kuanza ujenzi huo; na katika kila mwaka wa fedha Serikali hutenga fedha kwa ajili ya kuendelea na kumalizia ujenzi wa Hospitali hizi za Wilaya. Nimtoe mashaka Mheshimiwa Mbunge, tutakaa na wenzetu wa Wizara ya Fedha kuona katika mipango yao wameweka kiasi gani katika mwaka wa fedha unao fata ili ziweze kwenda Muleba kule kwa ajili ya ukamilishaiji wa Hospitali hii ya Wilaya.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa *Engineer* Samweli, swali la nyongeza.

**MHE. ENG. SAMWELI X. HHAYUMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipatia nafasi. Tarafa ya Balangaralu Makao Makuu yake yako Kata ya Balanga na pale hakuna Kituo cha Afya.

Je, Serikali ni lini itapeleka fedha ili kituo cha afya kijingwe pale?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DEOGRATIUS J. NDEJEMBI):** Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali itapeleka fedha katika Tarafa aliyoitaja Mheshimiwa Hhayuma kule Hanang kwa kadri ya upatikanaji wa fedha. Tutaangalia katika mipango iliyopo katika mwaka wa fedha unaofata 2023/2024 kuona kama fedha yoyote imetengwa kwa ajili ya kwenda Halmashauri ya Wilaya ya Hanang ili tuweze kuhakikisha inaenda haraka kwa ajili ya ujenzi wa vituo vya afya.

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa tunaendelea Wizara hiyo hiyo, swali la Mheshimiwa Dkt. Frolence Samizi Mbunge wa Mhambe litaulizwa kwa niaba yake na Mheshimiwa Sylivia Sigula.

Na. 665

**Kumaliza Ujenzi Kituo cha Afya Kata ya Kizazi Muhambwe**

**MHE.SYLIVIA F. SIGULA K.n.y. MHE. DKT. FLORENCE G. SAMIZI** aliuliza: -

Je, ni lini Serikali itapeleka fedha kumalizia ujenzi wa Kituo cha Afya Kata ya Kizazi?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DEOGRATIUS J. NDEJEMBI)** alijibu: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI naomba kujibu swali la Mheshimiwa Dkt. Florence George Samizi, Mbunge wa Jimbo la Muhambwe kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, Katika mwaka wa fedha wa 2023/2024, Serikali imetenga shilingi milioni 500 kwa ajili ya ujenzi wa Kituo cha Afya Kata ya Kizazi.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Sylivia, swali la nyongeza.

**MHE. SYLIVIA F. SIGULA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza niipongeze Serikali na niishukuru kwa majibu mazuri. Tunashukuru kwa hizo milioni mia tano kwa ajili ya ujenzi wa kituo cha afya, lakini nina maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la kwanza, Wilaya ya Kibondo kata ya Nyaruyoba hakuna Kituo cha Afya na wananchi wanahangaika. Tumeahidiwa milioni 200 kwa ajili ya ujenzi wa wodi.

Je, ni lini Serikali itatuletea milioni 200 hizo?

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini swali la pili Wilaya ya Buhigwe kata ya Mbanga na Kata ya Mhinda hakuna Vituo vya Afya, wananchi wanatembea umbali mrefu kupata huduma.

Je, ni lini Serikali itajenga Vituo vya Afya katika kata hizo?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DEOGRATIUS J. NDEJEMBI):** Mheshimiwa Mwenyekiti, nijibu maswali mawili ya nyongeza yaliyoulizwa na Mheshimiwa Sigula; la kwanza hili la Nyaruyoba kule Wilayani Kibondo milioni mia mbili, tutakaa na Mheshimiwa Mbunge ili tuweze kuwasiliana na idara ya afya katika Ofisi ya Rais TAMISEMI kuona fedha hizi zilizo ahidiwa zinaweza kwenda mara moja kwa ajili ya kuanza ujenzi wa kituo cha afya kule Wilayani Kibondo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikienda kwenye swali lake la pili, tutafanya tathmini kule Wilayani Buhigwe na kuona vituo hivi vya afya alivyoviomba Mheshimiwa Sigula kama vina kidhi vigezo vya kuweza kupandishwa hadhi na kuwa vituo vya afya ili tuweze kutenga fedha katika mwaka wa fedha unaofata kwa ajili ya kuanza ujenzi wake mara moja.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Sophia Mwakagenda, swali la nyongeza.

**MHE. SOPHIA H. MWAKAGENDA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Kata ya Kiwila katika Jimbo la Rungwe ni kata yenye wakazi wengi sana na kituo cha afya bado hakija malizika.

Je, ni lini Serikali mtatuongezea nguvu ili tuweze kumaliza kituo kile na kusaidia wananchi wa kata ile?

**MWENYERKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DEOGRATIUS J. NDEJEMBI):** Mheshimiwa Mwenyekiti, nijibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Mwakagenda kuhusu kata ya Kiwila kumaliziwa kituo chao cha afya. Nitakaa naye kuweza kujua ni majengo yapi ambayo bado hayajakamilika na kuhakikisha kwamba tunaona ni mipango ipi iliyotengwa na Halmashauri ya Wilaya ya Rungwe. Lakini vile vile sisi katika Ofisi ya Rais, TAMISEMI tutaona kwenye bajeti ya mwaka 2023/2024 ni kiasi gani kimetengwa kwa ajili ya Kituo hiki cha Afya Kiwila ili fedha hizo ziweze kwenda mara moja kwa ajili ya kumalizia majengo hayo.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Flatei Gregory Massay, swali la nyongeza.

**MHE. FLATEI G. MASSAY:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa nafasi. Mbulu Vijijini wananchi wamechanga na wamejenga kwenye Kata ya Geterei *OPD* kama Kituo cha Afya, na Kata ya Maseda vilevile; je, lini mtapeleka fedha kuunga juhudi za wananchi?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DEOGRATIUS J. NDEJEMBI):** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza niwapongeze Mheshimiwa Mbunge Flatei Massay vile vile na Mheshimiwa *DC* wake pale Ndugu Heri James kwa jitihada kubwa ambazo wanazifanya kwa ajili ya kusukuma gurudumu la maendeleo kwa kuhamasisha wananchi kujenga miundombinu ya afya. Nitakaa na Mheshimiwa Flatei kuona ni

mipango gani ambayo imewekwa kwetu katika Ofisi ya Rais, TAMISEMI kwa ajili ya kumalizia vituo vya afya ambavyo amevitaja.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Michael Mwakamo, swali la nyongeza.

**MHE. MICHAEL C. MWAKAMO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipa nafasi. Mwaka mmoja nyuma Waheshimiwa Wabunge wote tulitakiwa kutoa vipaumbele vya ujenzi wa Vituo vya Afya kwenye majimbo yetu. Mimi Mbunge wa Jimbo la Kibaha Vijijini ni miongoni na nilipewa Kituo cha Afya cha Kata ya Ruvu, lakini hadi leo hakuna kinachoendelea; je, nini kauli ya Serikali kwenye kuanzisha ujenzi wa kituo hicho?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DEOGRATIUS J. NDEJEMBI):** Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka wa fedha wa 2021/2022 Serikali ilijenga vituo vya afya 234 kote nchini, na hii ni *commitment* kubwa ya Rais wetu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dkt. Samia Suluhu Hassan ya kuhakikisha tunapata vituo vya afya kwenye maeneo yote ya kimkakati hapa nchini ikiwemo kule Kibaha Vijijini alipotaja Mheshimiwa Mwakamo. Tutakaa tuone katika mipango iliyowekwa mwaka 2023/2024 wa fedha, ni kiasi gani kimetengwa kwa ajili ya Kibaha Vijini ili kqenda kujenga kituo cha afya hicho cha kimkakati ambacho amekitaja Mheshimiwa Mwakamo.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Boniphace Getere, swali la nyongeza.

**MHE.BONIPHACE M. GETERE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nikushukuru. Jimbo la Bunda limekuwa na kituo cha muda mrefu cha zamani kinaitwa Ikizu, na kimechaka sana, na Serikali imetoa ahadi ya kukarabati vituo vya zamani vya afya;

Je, ni lini Kituo cha Ikizu kitakarabatiwa kwa ahadi ya Serikali?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DEOGRATIUS J. NDEJEMBI):** Mheshimiwa Mwenyekiti, nitakaa na Mheshimiwa Getere ili kuweza kuona ahadi hiyo ya Serikali ilitolewa lini ili tuweze kuifatilia vizuri kwenye idara husika ambayo ilitoa ahadi hiyo na tuweze kuhakikisha tunapata fedha kwa ajili ya kukarabati kituo cha afya hicho alichokitaja Mheshimiwa Getere.

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa tunaendelea Wizara hiyo hiyo. Mheshimiwa Joseph George Kakunda Mbunge wa Sikonge sasa aulize swali lake.

Na. 666

**Halmashauri ya Sikonge kupewa fedha kujenga Vituo vya Afya**

**MHE. JOSEPH G. KAKUNDA** aliuliza: -

Je, ni lini Halmashauri ya Sikonge itapatiwa shilingi bilioni 1.5 kwa ajili ya kujenga Vituo vya Afya Ipole, Kipanga na Usunga?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DEOGRATIUS J. NDEJEMBI)** alijibu: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Joseph George Kakunda, Mbunge wa Jimbo la Sikonge kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka wa fedha 2021/2022 Serikali ilitenga shilingi milioni 500 kwa Halmashauri ya Wilaya ya Sikonge kwa ajili ya ujenzi wa Kituo cha Afya Tutuo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali itaendelea kuweka mipango Madhubuti ya ujenzi wa vituo vya afya vikiwemo vituo vya afya vya Ipole, Kapanga na Usunga ili kuendelea kutoa na kuboresha huduma za afya nchini.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Joseph George Kakunda, swali la nyongeza.

**MHE. JOSEPH G. KAKUNDA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana majibu ya Serikali yamekuwa mazuri. Lakini kwa hali ya Jimbo la Sikonge ilivyo, kilometa za mraba 27,873, kuna wananchi wanatembea kilomita 70 mpaka kilometa 100 kufikia kituo cha afya cha karibu; je, Serikali haioni kwamba Wilaya au Jimbo kama la kwangu wanatakiwa waweke kipaumbele maalum ili watu wasiwe wanatembea kilomita 100 kufata kiyuo cha afya?

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili hizo fedha ambazo nimeuliza mimi bilioni 1.5 ni ela kidogo sana kwa Serikali; je, lini watatupatia hizo ela ili tuanze na hivyo vituo vitatu tulivyopendekeza?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DEOGRATIUS J. NDEJEMBI):** Mheshimiwa Mwenyekiti, nijibu maswali mawili ya Mheshimiwa Kakunda Mbunge wa Sikonge, la kwanza la Serikali kuona umuhimu. Serikali inaona umuhimu wa kujenga vituo vya afya kote nchini na ndio maana Serikali hii ya Awamu ya Sita ya Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan ilijenga vituo vya afya 234 kwa kutumia zaidi ya bilioni 117 kwa ajili ya kupeleka huduma karibu na wananchi. Tutakaa kuona ni mipango ipi iliyowekwa katika mwaka wa fedha 2023/2024 kwa ajili ya kujenga vituo vya afya katika Wilaya ya Sikonge.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikienda kwenye swali la pili, tutaangalia kadri ya upatikanaji wa fedha. Tutawasiliana na wenzetu wa Wizara ya Fedha kuona tunapataje fedha hii kwa ajili ya kusogeza huduma karibu kule Jimboni Sikonge.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Selemani Zedi swali la nyongeza.

**MHE.SELEMANI J. ZEDI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Mwaka huu wa fedha unaoisha 2022/2023 Serikali ilitenga milioni 500 kwa ajili ya kuanza ujenzi wa Kituo cha Afya kwenye Kata ya

Igusule, Jimbo la Bukene Halmashauri ya Wilaya ya Nzega. Sasa, ukizingatia kwamba bado siku chache mwaka huu uishe;

Je, Serikali inatoa kauli gani kuhusu kupeleka fedha hizi sasa milioni 500 ambazo ilizitenga kwenye Kata ya Igusule ili ujenzi wa Kituo cha Afya uanze?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri majibu kwa ufupi.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DEOGRATIUS J. NDEJEMBI):** Mheshimiwa Mwenyekiti, nitakaa na Mheshimiwa Zedi kuona hizi milioni 500 zilizotengwa ni hatua gani imefikiwa kwa ajili ya kuzipeleka kwa ajili ya kuanza ujenzi wa kituo cha afya kule Igusule, Jimboni Bukene.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Tarimba, swali la nyongeza.

**MHE. TARIMBA G. ABBAS:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nikushukuru. Niipongeze Serikali kwa kujenga vituo 234 vya afya nchini kikiwemo kituo cha kisasa kabisa pale katika Kata ya Kinondoni ambacho tayari kimeanza kufanya kazi. Tatizo ni uhaba wa madaktari na wauguzi;

Je, Serikali haioni umuhimu sasa wa kuhakikisha vituo hivi vipya ambavyo vimejengwa vinapata na kuondolewa tatizo la kuwa na madaktari na wauguzi?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DEOGRATIUS J. NDEJEMBI):** Mheshimiwa Mwenyekiti, nijibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Tarimba la kupata madaktari na wauguzi katika kituo cha afya Kinondoni. Jitihada za Serikali ya Awamu hii ya Sita katika kuhakikisha vituo vya Afya vyote vilivyojengwa na vilivyopo vinapata watumishi wa kutosha imefanyika kubwa katika mwaka wa fedha huu 2022/2023 kwa kuajiri watumishi wa afya 8070. Tayari watumishi hao wameanza kupangiwa maeneo yao ya kazi ikiwemo Halmashauri ya Kinondoni. Hivyo basi nimtake Mkurugenzi wa

Manispaa ya Kinondoni kuhakikisha kati ya wale ajira mpya atakao wapokea aweze kuwapangia katika vituo hivi vya afya ambavyo vimejengwa kwa fedha nyingi iliyotolewa na Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Masache Kasaka, swali la nyongeza.

**MHE. MASACHE N. KASAKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipa nafasi. Kituo cha Afya cha Matwiga, Isangawana na Mafyeko vilipata milioni mia tatu kila kituo na ujenzi wake ulishaanza;

Je, ni lini Serikali itatoa fedha ili vituo hivyo viweze kumalizika na baadaye wananchi waweze kupata huduma?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DEOGRATIUS J. NDEJEMBI):** Mheshimiwa Mwenyekiti, nijibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Masache Kasaka Mbunge wa Lupa; changamoto iliyojitokeza kule Wilayani Chunya ilikuwa kwamba fedha ilipelekwa na Serikali kwa ajili ya ujenzi wa Kituo cha Afya kimoja. Wao wenyewe walikaa kwenye Baraza la Madiwani wakaamua kugawanya fedha ile na kuanzisha ujenzi wa vituo vya afya viwili. Ni mategemeo yangu kwamba walipopitisha maamuzi yale walijua wana mapato ya kutosha kwa ajili ya kumalizia vituo vya Afya hivi vya Isangawana na Mpepo kule. Lakini nitakaa na Mheshimiwa Kasaka kuona ni namna gani tunaweza tukakaa, tukazungumza na Mkurugenzi wa Halmashauri ili waweze kumalizia maeneo haya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mgogoro ule ulianzishwa na wao wenyewe Madiwani kwa kugawanya fedha iliyotolewa na Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa ajili ya ujenzi wa kituo cha afya kimoja.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Dkt. Ishengoma, swali la nyongeza.

**MHE. DKT. CHRISTINE G. ISHENGOMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kuniona. Kituo cha Afya cha Mafiga ni kituo kikubwa ambacho hasa kinatoa huduma kwa akinamama wajawazito. Je, ni lini Serikali itatoa hela ya kumalizia jengo la upasuaji?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DEOGRATIUS J. NDEJEMBI):** Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali itatoa fedha kwa ajili ya umaliziaji wa Kituo hiki cha Afya Mafiga kadri ya upatikanaji wake, lakini tutaangalia katika mwaka wa fedha 2023/2024 kama kuna fedha imetengwa ili iweze kupelekwa mara moja kwa ajili ya kumalizia kituo hicho.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, tunakushukuru sana kwa majibu ya Waheshimiwa Wabunge.

Tunaendelea na Wizara ya Fedha na Mipango, Mheshimiwa Dkt. Oscar Ishengoma Kikoyo, Mbunge wa Muleba Kusini, sasa aulize swali lake.

Na. 667

**Benki ya Wakulima Mkoa wa Kagera**

**MHE. DKT. OSCAR I. KIKOYO** aliuliza:-

Je, Serikali ina mkakati gani wa kuinusuru Benki ya Wakulima Mkoa wa Kagera ambayo ipo chini ya uangalizi wa *BOT*?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, Wizara ya Fedha na Mipango, Mheshimiwa Hamad Chande, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Fedha na Mipango, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Oscar Ishengoma Kikoyo, Mbunge wa Muleba Kusini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, mnamo tarehe 4 Januari, 2018 Benki Kuu ya Tanzania iliifutia leseni ya kufanya biashara Benki ya Wakulima Mkoa wa Kagera baada ya kushindwa kutimiza masharti ya leseni. Sambamba na uamuzi wa kuifutia leseni, Benki Kuu iliamua kuiweka benki hii chini ya ufilisi na iliiteua Bodi ya Bima ya Amana *(Deposit Insurance Board - DIB)* kuwa mfilisi wa benki hiyo. Kwa muktadha huo, iliyokuwa Benki ya Kagera *Farmers' Cooperative Bank Limited* haipo chini ya uangalizi wa Benki Kuu ila ipo chini ya ufilisi wa *DIB* baada ya kufutiwa leseni ya biashara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa Sheria ya Benki na Taasisi za Fedha, 2006, benki ikishafutiwa leseni na kuwekwa chini ya ufilisi hakuna tena uwezekano wa benki kuendelea kuwepo na hivyo Serikali haina mpango wa kuifufua benki hiyo ila inafanya ufuatiliaji ili kuhakikisha kuwa zoezi la ufilisi linakamilika. Hadi Machi 2023, Bodi ya Bima ya Amana ilikuwa imelipa fidia ya bima ya amana jumla ya shilingi milioni 846.11 kwa wateja 1,389 waliokuwa na amana kwenye Benki ya Wakulima ya Kagera kati ya jumla ya shilingi milioni 899.56 zilizopaswa kulipwa kwa wateja 2,797 kulingana na matakwa ya sheria, ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Dkt. Oscar Kikoyo, swali la nyongeza.

**MHE. DKT. OSCAR I KIKOYO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa majibu ya Serikali. Kwa kuwa ni suala la Kisheria sitakuwa na swali la nyongeza nitachangia kwenye Bajeti Kuu, nashukuru sana.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Mheshimiwa Naibu Waziri, tunakushukuru kwa majibu ya Waheshimiwa Wabunge.

Tunaendelea na Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi, Mheshimiwa Ally Anyigulile Jumbe Mlaghila, Mbunge wa Kyela, sasa aulize swali lake.

Na. 668

**Barabara ya kutoka Ibanda – Itungi *Port***

**MHE. ALLY A. J. MLAGHILA** aliuliza:-

Je, ni lini ujenzi wa barabara ya kutoka Ibanda hadi *Itungi Port* (kilometa 25) utaanza?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, Wizara ya Ujenzi, Mheshimiwa *Engineer* Godfrey, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE)** alijibu: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Ally Anyigulile Jumbe Mlaghila, Mbunge wa Kyela, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mkataba wa ujenzi wa Barabara ya Ibanda – Kajunjumele – Kiwira/*Itungi Port* yenye urefu wa kilometa 32 ulisainiwa rasmi mnamo tarehe 27 Desemba, 2022 na kupewa kibali cha kuanza ujenzi mnamo tarehe 31 Machi, 2023. Kwa sasa Mkandarasi yupo eneo la mradi anaendelea na ujenzi wa Kambi za Mkandarasi na Msimamizi wa mradi ikiwa ni pamoja na maandalizi mengine kwa ajili ya kuanza ujenzi, ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Ally, swali la nyongeza.

**MHE. ALLY A. J. MLAGHILA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niishukuru sana Serikali ya Chama cha Mapinduzii kupitia Rais wetu Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, kwa ujenzi wa barabara hii na kwamba sasa imeanza. Sasa, nina maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la kwanza; je, Serikali imejiridhisha na uwezo wa Mkandarasi huyu mpaka kumpata maana inachoonekana sasa ni kwamba mkandarasi anasuasua sana tangu alipopewa ile *site*?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili, wananchi wote ambao wamepitiwa na barabara hiyo tangu miaka mitano iliyopita waliambiwa wasiendeleze maeneo yao na mpaka sasa hivi hawajalipwa maeneo yao na bado hawajapewa hata kiasi chochote au karatasi lolote linalooonesha kwamba wanaweza kulipwa kiasi fulani. Je, ni lini Serikali itawalipa wananchi wanaopitiwa na barabara hii pesa zao za fidia?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI (MHE. *ENG.* GODFREY K. MSONGWE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Ally Anyigulile Jumbe Mlaghila, Mbunge wa Kyela, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge na wananchi wa Kyela kwamba Mkandarasi ambaye amepewa kazi hii ana uwezo wa kutosha ndiyo maana amepewa kazi hiyo. Vile vile, ni mkandarasi ambaye alifanyiwa *due diligence* kwa maana ya kuangalia uwezo wake wa kifedha kwa maana ya mtaji lakini pia na vifaa vya kufanyia kazi hiyo. Kwa hiyo, tunaamini uwezo huo anao na ataijenga hiyo Barabara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu swali lake la pili la fidia. Ni kweli wananchi hawa bado hawajalipwa fidia, lakini nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge na wananchi wa Kyela kwamba uthamini ulishakamilika na majedwali ya malipo yalishakamilishwa na tayari Wizara ilishapeleka uthamini kwa maana ya gharama watakazolipwa ambayo ni bilioni 1.734 kwa wananchi wanaostahili kulipwa, hususani wale ambao watapisha ujenzi huu na watalipwa kwa mujibu wa Sheria yetu ambayo tunaituma kwa watu wanaopisha ujenzi wa barabara, ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Kabula, swali la nyongeza.

**MHE. KABULA E. SHITOBELA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante, je, ni lini ujenzi wa Barabara ya Hungumalwa – Kwimba kwenda Magu utaanza?

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Shitobela, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Barabara aliyoitaja ya Hungumalwa – Ngudu – Bukwimba hadi Magu ni barabara ambayo kumekuwa na watu wengi ambao wameipigia kelele sana. Hata hivyo, nataka nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba, katika mwaka wa fedha ambao bajeti tayari imeshapitishwa barabara hii imetengewa fedha kwa ajili ya kuanza ujenzi kwa kiwango cha lami kwa sababu usanifu ulishakamilika tayari, ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mashimba Ndaki, swali la nyongeza.

**MHE MASHIMBA M. NDAKI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Barabara ya Njia Panda - Ikungu kwenda Malampaka kilometa 14 au 15 inajengwa kwa lami, leo ni mwaka wa sita lakini zimejengwa kilometa nne tu. Sasa naomba kujua ni lini Serikali itatenga kiasi cha pesa cha kutosha ili kuweza kukamilisha ujenzi wa barabara hiyo ambayo ni muhimu kuunganisha Mkoa wa Simiyu na Kituo kikubwa cha *SGR* pale Malampaka?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante, naomba nikubaliane na Mheshimiwa Mbunge kuhusu swali lake la muhimu sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, barabara aliyoitaja ni kweli ndio barabara ambayo inaunganisha *SGR,* Mkoa wa Simiyu na hata watu ambao wanaweza kwenda na ndio kituo sahihi na hiyo barabara ndiyo inayounga. Kwa hiyo, naomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba, Serikali itafanya kila kinachowezekana kuhakikisha kwamba ahadi iliyoitoa ya kujenga hizo kilometa 14 ambazo bado kilometa 10 tunaikamilisha ili

kuhakikisha kwamba Kituo cha Malampaka kitakuwa ni muhimu sana kwa wananchi wa Maswa na Bariadi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba, Serikali inafahamu na itahakikisha kwamba inaijenga hiyo barabara kwa kiwango cha lami, ahsante.

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa tunaendelea na Wizara hiyo hiyo, Mheshimiwa Asha Abdullah Juma, Mbunge wa Viti Maalum, sasa aulize swali lake.

Na. 669

**Kukabiliana na ajali za majini**

**MHE. ASHA ABDULLAH JUMA** aliuliza:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kukabiliana na ajali za majini?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UCHUKUZI (MHE. ATUPELE F. MWAKIBETE)** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Asha Abdullah Juma, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali kupitia Shirika la Uwakala wa Meli Tanzania *(TASAC)* imeanza kutekeleza Mradi wa Ujenzi wa Kituo cha Kikanda cha Uratibu wa Shughuli za Utafutaji na Uokoaji Majini *(Regional Maritime Rescue Coordination Center – MRCC)* kupitia mradi unaoendelea katika Ziwa Victoria na vituo vidogo vinne vya uratibu wa shughuli za utafutaji na uokoaji majini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mradi huu unatekelezwa kwa fedha za ndani pamoja na mkopo kutoka Benki ya Maendeleo ya Afrika *(AfDB)* ambapo katika mwaka 2023/2024 umetengewa Shilingi bilioni 1.74. Aidha, kupitia mradi huo zitanunuliwa boti tatu

kwa ajili ya shughuli ya utafutaji na uokoaji ambazo kwa sasa zipo katika hatua za manunuzi, ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Asha Abdullah Juma, swali la nyongeza.

**MHE. ASHA ABDULLAH JUMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa majibu ya Serikali. Kwa kuwa ajali ni jambo ambalo *sometimes* haliepukiki, linaweza likatokea wakati wowote. Swali la kwanza; ili kuhakikisha usalama na kuepuka ajali za majini, je, *TASAC* inachukua hatua gani za kila siku za kuimarisha uokozi kwa ajili ya ajali za majini?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili; je, Serikali ina mpango gani katika kuwekeza kwenye dhana kama vile boti za mwendokasi, vifaa na kuwawezesha kwa kuwapa utaalam wa uokozi wakati wa ajali za majini?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UCHUKUZI (MHE. ATUPELE F. MWAKIBETE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Asha Abdallah Juma, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kupitia Shirika letu la *TASAC* Serikali imeendelea kuchukua hatua mbalimbali hususani katika uokozi maeneo ya majini, ziwani pamoja na baharini kwa kuchukua hatua mbalimbali. Hatua ya kwanza, huwa tunatoa elimu kwa wadau wote wanajishughulisha na masuala ya uvuvi baharini ama baharia. Hatua ya pili, kupitia *TMA (*Mamlaka ya Hali ya Hewa Nchini) ambako tunatoa taarifa ya hali ya hewa kila siku kwa Maziwa yote Ziwa Victoria, Ziwa Tanganyika, Ziwa Nyasa pamoja na Baharini ili kujua mwenendo wa upepo pamoja na hali ya Maziwa hayo na Bahari kwa ujumla.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hatua nyingine, tunafanya uchunguzi wa ajali ili kubaini vyanzo vya ajali hizo na itatusaidia katika ajali nyinginezo zitakazojitokeza na kuzuia zisitokee.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine tumefanya mafunzo kwa Mabaharia kupitia *International Maritime Organization* na kupewa vyeti (Ithibati) kwa Mabaharia wote ambao wako katika maeneo hayo ya maziwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili kuhusu vifaa, kama ambavyo nimejibu kwenye jibu langu la msingi kwamba Serikali katika mwaka wa fedha ujao imetenga takribani bilioni 1.74 kwa ajili ya ununuzi wa boti mbili kwa ajili ya uokozi ambapo boti moja itakuwa kama *ambulance* katika kutatua changamoto zote ndani ya maziwa na baharini, ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Aida Khenani, swali la nyongeza.

**MHE. AIDA J. KHENANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Kwa kuwa vifo vingi vinavyotokea Ziwa Tanganyika vinatokana na wananchi kutumia usafiri ambao sio salama, kwa sababu hatuna usafiri wa uhakika kwa maana ya meli. Je, Serikali haioni haja sasa ya kupeleka usafiri wa kisasa Ziwa Tanganyika ili kuokoa vifo vya watu vinavyotokea?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu kwa ufupi.

**NAIBU WAZIRI WA UCHUKUZI (MHE. ATUPELE F. MWAKIBETE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Khenani, Mbunge, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, bajeti yetu ya Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi iliyosomwa tarehe 22 na 23, tulifanya *Commitment* kwamba mwaka wa fedha ujao 2023/2024 tunakwenda kujenga na kununua meli mbili za kisasa. Vilevile, hivi karibuni tulikuwa na vikao na Waheshimiwa Wabunge wote wa Mikoa ya Kigoma, Rukwa pamoja na Katavi kuhakikisha kwamba haya ambayo Serikali imefanya *commitment* katika bajeti, tunakwenda kuyafanya na naamini tutayatekeleza, ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Stanslaus Nyongo, swali la nyongeza.

**MHE. STANSALAUS H. NYONGO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Kwa mustakabali huo huo kwa jinsi zinavyotokea ajali nyingi si baharini tu hata pale panapotokea barabara inapokutana na reli kuna ajali nyingi sana zinatokea na kusababisha madereva wa treni sasa hivi wanapiga *horn* usiku kucha na kusababisha watu kutokulala hususani pale treni inapopita ili kuepusha ajali za barabarani zinazotokea. Je, Serikali ina mpango gani wa kuweka *automatic gates* katika kila barabara na reli inapokatiza ili kuondoa ajali na kutokupiga *horn* usiku zinazowafanya watu kukosa usingizi?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu kwa ufupi.

**NAIBU WAZIRI WA UCHUKUZI (MHE. ATUPELE F. MWAKIBETE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Nyongo, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kumekuwa na changamoto kubwa sana kati ya maeneo ambapo barabara inapita na reli inapita. Kwa kutambua hilo, Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi kupitia Shirika letu la Reli Nchini, tumetangaza tenda kwa ajili nya kuweka mifumo mipya *automatic systems* ambayo itakuwa ni *gate way* inajifunga na kufunguka *automatic*. Vile vile, tenda hii mwisho wa ku–*submit* ni kesho.

Kwa hiyo, wale wote ambao wako *interested* na ni *international tender,* wanakaribishwa kuomba ili tuweze kutengeneza mifumo yote na maeneo yote ya mapitio kati ya barabara na reli, ahsante.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Wizara hiyo hiyo, Mheshimiwa Ally Mohamed Kassinge, Mbunge wa Kilwa Kusini, sasa aulize swali lake.

Na. 670

**Fidia kwa wananchi kupisha ujenzi wa Kiwanja cha Ndege- Kilwa**

**MHE. ALLY M. KASSINGE** aliuliza:-

Je, ni lini wananchi 144 wa Kilwa Masoko ambao maeneo yao yalichukuliwa kwa lengo la upanuzi wa Kiwanja cha Ndege watalipwa fidia?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UCHUKUZI (MHE. ATUPELE F. MWAKIBETE)** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Ally Mohamed Kassinge, Mbunge wa Kilwa Kusini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kutekeleza zoezi la ulipaji fidia kwa wananchi waliopisha upanuzi wa Kiwanja cha Ndege cha Kilwa Masoko, Serikali imehuisha uthamini wa mali za wananchi ndani ya kipindi cha robo ya kwanza ya Mwaka wa Fedha 2022/2023, ambapo idadi ya wananchi iliongezeka kutoka 144 waliofanyiwa uthamini mwaka 2013 hadi kufikia wananchi 438.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sasa Serikali ipo katika hatua za mwisho za maandalizi ya uwekaji wazi Daftari la Fidia *(Valuation Report Disclosure)* kwa wananchi husika kabla ya kuwasilishwa kwa Mthamini Mkuu wa Serikali kwa idhini, ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Ally Mohamed Kassinge, swali la nyongeza.

**MHE. ALLY M. KASSINGE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa nafasi ya swali la nyongeza na nitakuwa na maswali mawili ya nyongeza. Nishukuru Serikali kwa hatua hiyo, lakini niombe mchakato wa malipo sasa uharakishwe kwa sababu uthamini huu umefanyika kwa muda mrefu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la kwanza; kumekuwa na changamoto katika umakini wa uhakiki hususani uliofanyika katika kipindi hiki cha pili ambapo wananchi wengi wamekuwa wakilalamika kwamba wanapunjwa, kucheleweshwa kwa malipo haya na malalamiko mengine mengi. Je, Mheshimiwa Waziri baada ya Bunge hili atakuwa tayari kuambatana nami kwenda Kilwa Masoko kukaa na wananchi hawa kuwasikiliza kero zao na hatimaye kuwapatia majawabu?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili; Mradi na Mpango huu ni wa muda mrefu, je, ni lini sasa upanuzi na uboreshaji wa Kiwanja cha Ndege Kilwa Masoko utaanza?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UCHUKUZI (MHE. ATUPELE F. MWAKIBETE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Ally Mohamed Kassinge, Mbunge wa Kilwa Kusini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimpongeze Mheshimiwa Mbunge kwa ufuatiliaji wa jambo hili la fidia kwa wananchi wake na Serikali imeendelea kulifanyia kazi. suala la kuambatana naye nimhakikishie nitaambatana naye mara baada ya vikao vya Bunge. Vile vile, nitakuwa na ziara katika Mkoa wa Lindi (Kilwa) Morogoro, Ruvuma pamoja na Iringa. Hivyo, Mheshimiwa Mbunge hata huko Kilwa nitafika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili; ni lini hasa upanuzi wa kiwanja utaanza. Ni kwamba tayari tumekuwa na awamu mbili za upanuzi wa kiwanja hiki ambapo awamu ya kwanza ilikuwa kwa ajili ya kutanua ile *run way* kuweka moramu na sasa hivi tumejenga jengo la abiria lililogharimu takribani milioni 137. Awamu ya pili itafadhiliwa na Benki ya Dunia ambayo iko katika mpango wa Serikali wa mwaka wa fedha ujao. Kwa hiyo, baada ya hapo kiwanja hiki kitakuwa kimekamilika, ahsante sana.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Saashisha Mafuwe, swali la nyongeza.

**MHE. SAASHISHA E. MAFUWE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Wananchi wanaozunguka Uwanja wa Ndege wa *KIA* wamekwishafanyiwa tathmini ya baadhi ya maeneo ambayo yanapaswa kupisha Uwanja wa Ndege wa *KIA*. Swali langu, je, ni lini sasa Serikali itaanza kulipa wananchi hawa fidia?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UCHUKUZI (MHE. ATUPELE F. MWAKIBETE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Mbunge Saashisha, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli eneo alilolisema katika uwanja huu Serikali imefanya tathmini na uthamini na kinachoendelea sasa tumeshapeleka lile daftari kwa Mthamini Mkuu wa Serikali, tayari kwa ajili ya malipo na kwenda kupeleka Hazina. Kwa hiyo nimwombe Mheshimiwa Mbunge na wananchi wawe wavumilivu wakati wanasubiri malipo yao, ahsante.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu ya Waheshimiwa Wabunge. Tunaenda Wizara ya Katiba na Sheria, Mheshimiwa Nashon William Bidyanguze, Mbunge wa Kigoma Kusini, sasa aulize swali lake.

Na. 671

**Kurejesha huduma za Mahakama ya Mwanzo Kata ya Kalya Buhingu – Kigoma Kusini**

**MHE. NASHON W. BIDYANGUZE** aliuliza:-

Je, ni lini Serikali itarudisha huduma za Mahakama za Mwanzo katika Kata ya Kalya Buhingu?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, Wizara ya Katiba na Sheria, Mheshimiwa Pauline Gekul, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Katiba na Sheria, naomba sasa kujibu swali la Mheshimiwa Nashon William Bidyanguze, Mbunge wa Kigoma Kusini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mahakama inaendelea na mipango ya kufanya ujenzi na tayari huduma imerejeshwa kuanzia mwezi Julai, 2022 na mpaka sasa wapo watumishi wanatoa huduma kwa kutumia Ofisi za Kata. Kuanzia mwezi Julai 2022 huduma iliporejea hadi Machi, 2023 jumla ya mashauri 38 yamesajiliwa na kusikilizwa katika Mahakama hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mpango wa ujenzi wa Mahakama, tumepanga kujenga Mahakama ya Mwanzo Mgambo mwaka 2024/2025, ambapo ndiyo Makao Makuu ya Tarafa ya Buhingu. Hivyo, tunatajarajia kuwa wananchi wa Kalya watapata huduma katika Mahakama ya Mwanzo Mgambo. Ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Nashon, swali la nyongeza.

**MHE. NASHON W. BIDYANGUZE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante, naomba nilulize swali la nyongeza. Kwamba Mahakama ya Mwanzo kule Kalya inaendelea ni kweli. Sasa nilikuwa naomba niishauri Serikali kwamba yule Hakimu wa Mahakama ya Mwanzo kule Kalya basi aje kwenye Makao Makuu ya Tarafa pale Buhingu kabla jengo hilo halijajengwa la Mahakama ili aendelee kuhudumia wananchi kwa masuala ya sheria, ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru naomba nijibu swali moja la nyongeza la Mheshimiwa Nashon, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni dhahiri kwamba Makao Makuu haya ya Mgambo na Kalya kuna umbali zaidi ya kilomita 100 na wananchi wamekuwa wakipata tabu kufikia huduma hii. Mahakama yetu ya Tanzania inaridhia maombi ya Mheshimiwa Mbunge kwamba huyo Hakimu aliyeko Kalya aende sasa Mgambo walau tumtafutie Ofisi pale kwa Afisa Tarafa ili huduma,

iendelee kwa hiyo Mheshimiwa Mbunge tunalipokea jambo hili na tunalifanyia kazi na huduma itatolewa.*(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mrisho Gambo, swali la nyongeza.

**MHE. MRISHO M. GAMBO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa Jiji la Arusha limetenga eneo la ekari tano kwenye Kata ya Terrat kwa ajili ya ujenzi wa Mahakama mpya ya mwanzo; je ni lini Serikali itaanza ujenzi wa mahakama hii ya mwanzo kwenye Kata ya Terrat?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu kwa ufupi.

**NAIBU WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru naomba nijibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Mrisho Gambo, Mbunge wa Arusha Mjini kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka huu wa fedha ambao tunashukuru Bunge lako tukufu lilitupitishia bajeti ya zaidi ya bilioni 57 fedha za nje pamoja na bilioni 31 fedha za ndani, tumepanga kujenga mahakama zaidi ya 60 na miongoni mwa maeneo ambayo tutakwenda kujenga ni eneo hili la Terrat pale Arusha. Kwa hiyo, Mheshimiwa Gambo kuwa na amani mwaka huu tunajenga Mahakama katika eneo la Terrat.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Asia Halamga, swali la nyongeza.

**MHE. ASIA A. HALAMGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Je Serikali ina mpango gani wa kujenga Mahakama ya mwanzo eneo la Minjingu?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru kwa nafasi naomba sasa kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Asia Halamga, Mbunge wa Viti Maalum Mkoa wa Manyara, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mpango wetu huu wa bajeti ya mwaka huu miongoni mwa maeneo ambayo yanahitaji ujenzi wa Mahakama ni pamoja na eneo la Minjingu. Mheshimiwa Asia pamoja na wewe mmekuwa mkikumbusha jambo hili naomba niliarifu Bunge hili Tukufu na wananchi wa Babati Vijijini kwamba tutajenga Mahakama pale Minjingu ili wananchi wapate huduma.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Christina Mnzava, swali la nyongeza.

**MHE. DKT. CHRISTINA C. MNZAVA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante, kwa kuwa Mahakama za Usanda na Samuye katika Halmashauri ya Shinyanga zimejengwa toka enzi ya mkoloni. Je, ni lini Serikali itafanya ukarabati wa Mahakama hizo?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu kwa ufupi.

**NAIBU WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru nijibu swali la Mheshimiwa Mnzava Mbunge wa Viti Maalum kutoka Mkoa wa Shinyanga kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mpango wetu wa Mahakama mwaka huu tunakwenda kujenga Mahakama zaidi ya 38 za Wilaya, Mahakama 60 za mwanzo lakini pia fedha hizi ambazo tumetenga tunakarabati pia Mahakama.

Kwa hiyo, Mheshimiwa Mnzava nipokee Mahakama ambazo umezitaja tutaweka kwenye mpango wetu wa Mahakama ili tuzikarabati.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri nakushukuru sana kwa majibu ya Waheshimiwa Wabunge.

Tunaendelea na Wizara ya Habari, Mawasilano na Teknolojia ya Habari. Mheshimiwa Neema Kichiki Lugangira, Mbunge wa Viti Maalum, sasa aulize swali lake.

Na. 672

**Kuhuisha Sheria ya Makosa ya Mtandao na Ulinzi wa Taarifa Binafsi**

**MHE. NEEMA K. LUGANGIRA** aliuliza:-

Je, ni lini Sheria ya Makosa ya Mtandao na Sheria ya Ulinzi wa Taarifa Binafsi Pamoja na Malabo *Convention* vitahuishwa?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri Wizara ya Mawasiliano Mheshimiwa *Engineer* Kundo, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA HABARI, MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Neema Kichiki Lugangira, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali imekamilisha utungwaji wa Sheria ya Ulinzi wa Taarifa Binafsi *(Personal Data Protection Act, 2022)* iliyosainiwa Novemba, 2022 na kutangazwa katika gazeti la Serikali tarehe 2 Desemba, 2022. Sheria hiyo imeanza kutumika rasmi tarehe 1 Mei, 2023.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kuweka mazingira wezeshi zaidi ya utekelezaji wa masuala mbalimbali yanayohusiana na TEHAMA nchini ikiwemo kufanikisha kufikia azma ya uchumi wa kidijitali, Serikali kupitia mradi wa Tanzania ya Kidijitali *(DTP)* inaendelea na zoezi la mapitio ya Sera, Sheria, na Mikataba mbalimbali ya Kikanda na Kimataifa inayohusu TEHAMA.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sheria zinazofanyiwa mapitio kwa ajili ya kuhuishwa ni pamoja na Sheria ya Makosa ya Mtandao ya Mwaka 2015. Vilevile mikataba ambayo utaratibu umeanza kwa ajili ya kuridhiwa ni pamoja na Mkataba wa Malabo.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Neema Lugangira, swali la nyongeza.

**MHE. NEEMA K. LUGANGIRA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru pamoja na majibu mazuri ya Serikali naomba kuuliza maswali mawili madogo ya nyongeza.

Kwa kuwa, Malabo *convection* inaweka msingi wa Makosa ya Mtandao, Ulinzi wa Taarifa Binafsi pamoja na Biashara ya Mtandao, na kwa kutambua fursa zinazotokana na Soko Huru la Afrika la Biashara ya Mtandao; Je, ni lili sasa Serikali italeta azimio hapa Bungeni la kuridhia mkataba huu wa Malabo ili Tanzania isiendelee kuchelewa kupata fursa zinazotokana na soko huru hili la biashara Barani Afrika.

Swali la pili, kwa kuwa tayari Sheria ya Ulinzi wa Taarifa Binafsi imeanza kutumika. Je, ni lini sasa Serikali itatunga kanuni kwa ajili ya sheria hiyo ili kuendelea kulinda Ulinzi wa Taarifa Binafsi ikiwemo changamoto kubwa ya ukatili wa kijinsia mtandaoni? Ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA HABARI, MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Neema Lugangira kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nimpongeze sana Mheshimiwa Neema Lugangira ambaye amekuwa mdau mkubwa sana katika sekta yetu hii ya mawasiliano.

Kwanza kabisa nianze na swali dogo la pili kuhusiana na Kanuni za Ulinzi wa Taarifa Binafsi. Mheshimiwa Waziri tarehe 6 Mei, 2023 alisaini kanuni hizo ambazo ziko tayari kwa ajili ya kutumika. Kwa hiyo Mheshimiwa Mbunge anaweza akapata fursa ya kuzipitia na kuona namna gani zinaenda kujibu hoja baadhi ya maeneo ambayo Mheshimiwa Mbunge ameyataja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la kwanza ambalo Mheshimiwa Mbunge ameligusia kuhusu maazimio kuletwa Bungeni. Tayari tuko kwenye mchakato huo na mchakato una

hatua kadhaa lakini katika hizo hatua kuna hatua ya kuleta Bungeni. Nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge tuko katika hatua nzuri kabisa na zikishakamilika hatua hizo za awali pale ambapo itahitaji sasa kuileta Bungeni tutaileta kulingana na utaratibu unavyotuelekeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushuru sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Janeth Mahawanga, swali la nyongeza.

**MHE JANETH E. MAHAWANGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali dogo la nyongeza. Je, ni lini kanuni za *MSA (Media Service Act)* zitahuishwa na wadau kushirikishwa ipasavyo?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA HABARI, MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Janeth Mahawanga, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, wiki iliyopita tumepitisha marekebisho ya *Media Service Act* ambapo tunatarajia Mheshimiwa Rais akishasaini baada ya hapo Mheshimiwa Waziri atatangaza siku ya kuanza kutumika kwake, vilevile tutaanza mchakato wa kuhakikisha kwamba kanuni hizo ambazo zinaendana sambamba na mabadiliko hayo basi zitakuwa zimetungwa na zitapitia katika utaratibu uleule wa kuhakikisha kwamba tunahusisha wadau ili waweze kushiriki katika mchakato mzima na baada ya hapo kanuni zitakuwa tayari kwa ajili ya matumizi. Ahsante

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu ya Waheshimiwa Wabunge.

Tunaendelea na Wizara ya Kilimo, Mheshimiwa Moshi Selemani Kakoso, Mbunge wa Mpanda Vijijini, sasa aulize swali lake.

Na. 673

**Kukamilika Skimu za Umwagiliaji za Karema na Kabage-Katavi**

**MHE. MOSHI S. KAKOSO** aliuliza:**-**

Je ni lini Serikali itakamilisha ujenzi wa skimu za umwagiliaji za Karema na Kabage Mkoani Katavi?

**NAIBU WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI K.n.y. WAZIRI WA KILIMO** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Kwa niaba ya Waziri wa kilimo naomba kujibu swali la Mheshimiwa Moshi Selemani Kakoso, Mbunge Jimbo la Mpanda Vijijini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka wa fedha wa 2021/2022 Tume ya Taifa ya Umwagiliaji ilitenga kiasi cha shilingi 84,910,676 kwa ajili ya ukarabati wa mfereji mkuu wa skimu ya umwagiliaji Karema ambapo Mkandarasi amefikia asilimia 80 ya ujenzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali katika mwaka wa fedha 2022/2023 imetenga bajeti ya miradi hiyo ambapo mradi wa umwagiliaji Kabage upo katika hatua ya manunuzi na mradi wa umwagiliaji Karema upo katika hatua za mwisho za usanifu wa bwawa na miundombinu ya umwagiliaji. Ujenzi wa miundombinu katika skimu hizo utakamilika mwaka 2023/2024.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Moshi Selemani Kakoso, swali la nyongeza.

**MHE. MOSHI S. KAKOSO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nishukuru kunipa nafasi ya kuuliza maswali mawili ya nyongeza.

Kwa kuwa, mradi huu wa skimu ya umwagiliaji ya Karema umechukua muda mrefu zaidi ya miaka kumi na swali kama hili nimeliuliza hapa Bungeni zaidi ya mara tano.

Je, Serikali sasa ina mkakati gani wa kwenda kubomoa ile miundombinu ambayo waliiweka ambayo haiwasaidii wananchi na kabla ya kuweka mradi ule wananchi walikuwa wakinufaika wanapata mazao yao. Lini Serikali wataenda kubomoa ule mradi?

Swali la pili, kwa kuwa ndani ya miaka kumi wananchi wamekuwa wakilima wakipata hasara kwa sababu ya miundombinu iliyowekwa mibovu. Serikali ina mkakati gani wa kuwalipa fidia wakulima hao ambao wamelima kwa miaka kumi wakiteseka?*(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI K.n.y. WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Kwanza ninampongeza Mheshimiwa Mbunge kwa kufuatilia kwa ukaribu juu ya ujenzi wa mradi wa Karema wa umwagiliaji, lakini nimuondoe shaka kwamba ndiyo maana ukiona katika jibu la msingi tumeandika hapa kwamba mradi huu wa Karema ambao sasa hivi uko katika hatua za mwisho za usanifu wa bwawa pamoja na miundombinu ya umwagiliaji na tumeahidi kabisa hapa kwamba utakamilika katika mwaka wa fedha 2022/2023.

Kwa hiyo, nimuondoe shaka kwa sababu Serikali imeona hiyo kero ya wananchi na katika mwaka wa fedha unaokuja litatekelezeka kama ambavyo Wizara ya kilimo imeahidi na itafanya hivyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili kuhusu hasara ambayo wananchi wameipata kutokana na kushindwa kulima vizuri katika eneo lao, nimwambie tu kwamba ukweli ni kwamba hatuwezi kulipa fidia kwa hasara ambazo zilitokana na wao kulima eneo lile, lakini Serikali imekuwa ikizingatia umuhimu wa wakulima nchini na ndiyo maana umeona Serikali katika ku-*boost* kilimo ikawa imekuja na mradi wa kutoa ruzuku za pembejeo, yote hii ni kutaka kuwanufaisha wananchi ambao wanapata faida kutokana na ruzuku hizo. Kwa hiyo, tutaendelea kuboresha kilimo nchini ili kuhakikisha wananchi wetu wanaendelea kupata faida. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, naomba twende swali Na. 675 naomba nimuite Mheshimiwa Ally Juma Makoa, Mbunge wa Kondoa Mjini swali lake litaulizwa na Mheshimiwa Miraji Mtaturu kwa niaba yake. Mheshimiwa Miraji Mtaturu.

Na. 675

**Serikali kujenga majosho katika Kata za Kolo, Kingale na Bolisa - Kondoa Mji**

**MHE. MIRAJI J. MTATURU K.n.y MHE. ALLY J. MAKOA** aliuliza:-

Je, ni lini Serikali itajenga majosho katika Kata za Kolo, Kingale na Bolisa?

**NAIBU WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Kwa niaba ya Waziri wa Mifugo na Uvuvi, naomba kujibu Swali la Mheshimiwa Ally Juma Makoa, Mbunge wa Kondoa Mjini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali inaendelea na mpango wa ujenzi wa majosho nchini ili kudhibiti magonjwa yanayoenezwa na kupe. Katika mwaka wa fedha wa 2023/2024 Wizara ya Mifugo na Uvuvi, Sekta ya Mifugo, imetenga jumla ya shilingi bilioni 5.7 kwa ajili ya ujenzi wa majosho 246 katika Halmashauri 63 nchi nzima.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Jimbo la Kondoa Mjini jumla ya shilingi milioni 115,000,000 zimetengwa kwa ajili ya ujenzi wa majosho matano katika kata za Kingale Mitaa ya Msui na Tampori, Serya Mtaa wa Chandimo, Suruke Mtaa wa Tungufu na Kondoa Mjini Mtaa wa Tumbelo chang'ombe. Hivyo basi, ninamshauri Mheshimiwa Mbunge kuwasiliana na kujadiliana na Mkurugenzi wa Halmashauri ili kama kuna haja ya mabadiliko ya maeneo ya ujenzi wa majosho yaweze kufanywa kulingana na vipaumbele vya wananchi na Halmashauri. Ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Miraji Mtaturu, swali la nyongeza.

**MHE. MIRAJI J. MTATURU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Ninamshukuru sana Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu mazuri aliyotoa kwa niaba ya wananchi wa Jimbo la Kondoa, lakini ninayo maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu majosho haya yanalenga katika kuboresha afya za mifugo ambayo mwisho wa siku tunapata kitoweo kizuri. Ni nini mkakati wa Serikali kuhakikisha kwamba ujenzi huo unasimamiwa vizuri na majosho yale yakamilike kwa muda uliopangwa?

Swali la pili, kwenye Jimbo la Singida Mashariki katika Kata ya Siuyu tulikuwa na josho ambalo sasa hivi limeingiliwa na eneo la Kanisa la *RC* pale Siuyu na tuliomba lihamishwe liende eneo lingine kwa sababu linakosa sifa ya kutumika pale. Tumeshatenga eneo katika Kijiji cha Siuyu na tuliomba muda mrefu zaidi ya miaka mitatu sasa. Ni lini Serikali itajenga josho kwa ajili ya kutoa huduma ya mifugo katika Kata ya Siuyu. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu

**NAIBU WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Swali la kwanza la Mheshimiwa Mbunge ni kwamba amepongeza hii jitihada ambayo tumeifanya lakini vilevile ametaka kuona kwamba kunakuwa na usimamizi mzuri na kuhakikisha haya majosho yanakamilika ili kuimarisha afya ya mifugo. Kwa hiyo, nimuondoe hofu kwamba Wizara ya Mifugo na Uvuvi chini ya Waziri Ulega pamoja na mimi Msaidizi wake tunaahidi kabisa kwamba haya yote yaliyopangwa katika mwaka wa fedha unaokuja na yale ambayo hayajakamilika tutahakikisha katika mwaka wa fedha unaokuja yanakamilika kwa wakati kwa sababu hili ndiyo lengo letu na ndiyo lengo la Mheshimiwa Rais.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu ujenzi wa josho katika Kijiji cha Siuyu ambacho Mheshimiwa Mbunge amekitaja hapa basi naomba jambo hilo nilipokee kwa sababu nitaangalia katika orodha ambayo tunayo hapa kama tumelitenga katika mwaka huu fedha na kama halipo tuone namna gani tunatafuta fedha ili

kuliweka katika moja ya vipaumbele vyetu. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa kuchauka swali la nyongeza.

**MHE. ZUBERI M. KUCHAUKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza.

Wilaya ya Liwale ndiyo Wilaya katika Mkoa wa Lindi imepokea wafugaji wengi sana lakini hakuna miundombinu ya majosho wala malambo. Je Serikali iko tayari kutujengea majosho na malambo kwenye Kata ya Lilombe na Kata ya Ndapata, Kata ambazo ndizo zimetengwa kwa ajili ya kupokea wafugaji? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu kwa ufupi.

**NAIBU WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Wilaya ya Liwale ni miongoni mwa Wilaya ambazo zipo katika mpango wetu katika huu mwaka. Kikubwa tutaangalia katika orodha ili tuone maeneo gani ambayo tutayapa kipaumbele. Ahsante.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu ya Waheshimiwa Wabunge. Tunaenda Wizara ya Afya, Mheshimiwa Asia Abdukarimu Halamga, Mbunge wa Viti Maalum, sasa aulize swali lake.

Na. 676

**Uhakika wa kupatikana dawa nchi nzima**

**MHE. ASIA A. HALAMGA** aliuliza:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kuhakikisha kuwa dawa zinapatikana wakati wote katika hospitali, vituo vya afya na zahanati nchini?

**NAIBU WAZIRI WA AFYA** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Afya naomba kujibu swali la Mheshimiwa Asia Abdukarimu Halamga, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kuhakikisha dawa zinapatikana wakati wote kwenye vituo vya kutolea huduma za afya, Serikali inatekeleza na kusimamia yafuatayo:-

i. Kuiwezesha *MSD* mtaji ili iweze kufanya kazi kama bohari ya dawa badala ya kufanya kazi kama idara ya manunuzi,

ii. Utoaji wa fedha za kununua, kutunza na kusambaza dawa kila mwezi kiasi cha shilingi bilioni 16,

iii. Kuboresha utendaji wa *MSD* na kuiwezesha kuwa na mikataba ya muda mrefu ya ununuzi wa dawa,

iv. Kuboresha maoteo ya bidhaa za afya na kuchukua hatua kwa upungufu unaobainika,

v. Kufunga mifumo ya kielektroniki ili kuimarisha usimamizi wa dawa na kuwezesha dawa kutolewa kulingana na wagonjwa husika,

vi. Kusimamia Muongozo wa matibabu katika kuhakikisha dawa zinazonunuliwa, kutunzwa na kuandikwa na Madaktari zinazingatia muongozo wa matibabu,

vii. Kudhibiti mianya ya upotevu na wizi kwa kuwa na kaguzi za mara kwa mara ili kuhakikisha dawa zinakuwepo vituoni,

viii. Kuanzisha maduka ya dawa ya hospitali za umma yatakayokuwa na dawa muda wote kwa ajili ya wagonjwa wa ndani na nje ya hospitali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nichukue nafasi hii kuzielekeza Halmashauri na viongozi wote wa vituo vya kutolea huduma za

afya kuhakikisha wanatumia zaidi ya asilimia 50 ya mapato yao kununua dawa na bidhaa nyinginezo za afya.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Asia Halamga, swali la nyongeza.

**MHE. ASIA A. HALAMGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi ya kuuliza maswali mawili ya nyongeza. Kwanza nichuke nafasi hii kuipongeza Serikali kwa majibu mazuri, lakini pia nina maswali yangu mawili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali imekuwa ikinunua dawa *MSD* na inapokosa inanunua kwa mshitiri; je, Serikali inamkaguaje mshitiri ili kuwa na dawa za kutosha pale inapokosekana *MSD?*

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali langu la pili; ni hatua gani zinachukuliwa kwa watoa huduma wa vituo vya afya ambao wanathibitika na upotevu wa madawa? Ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu kwa ufupi.

**NAIBU WAZIRI WA AFYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nianze kwa kumshukuru Mheshimiwa Mbunge kwa maswali yake mazuri ambayo yanalenga kuboresha mifumo ya utoaji wa huduma. Ni kweli kama anavyosema Mbunge kwamba, wakati mwingine inapokuwa *MSD* hakuna dawa, basi watu wetu wanapewa *OS* na wanakwenda kununua kwa mshitiri, lakini kuna mikoa ambayo wamemweka mshitiri ambaye ni mmoja na wataalam wetu hawaruhusiwi kunua dawa nje ya yule mshitiri. Kwa hiyo, anapokuwa amekosa *MSD,* anafika kwa mshitiri, naye mshitiri akiwa hana dawa, kwa hiyo, inafika mahali watu wetu wanateseka hawana dawa na huku fedha wanazo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitumie fursa hii na hili swali la Mheshimiwa Mbunge kuagiza kwamba, kwanza tusilazimishe hospitali zetu kununua kwa mtu fulani dawa. Ni kwamba tutengeneze biashara huria, duka lolote lenye dawa ambalo limetimiza vigezo, watu wetu waweze kununua kwenye duka lolote la dawa bila kulazimishwa kununua kwa mtu fulani. Kwa sababu nayo hiyo ni aina ya ufisadi mwingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kumwambia Mheshimiwa Mbunge, hakika tutakapokuwa tunapita, tutashirikiana naye kushughulikia suala hilo, kwa sababu ukiona mtu mmoja analazimishwa kwenye mkoa mmoja kwamba yeye ndio auze dawa, hiyo ni aina mwingine wa ufisadi na tutausimamia na ku-*control*.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa…

**NAIBU WAZIRI WA AFYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, swali lake la pili kuhusu tunafanya nini kwa wale wanaobainika kwamba wameiba dawa, kwa kweli kuna sheria na taratibu za utumishi wa umma. Kama unavyojua, nasi ni Wabunge ambao tunatunga sheria hapa, kuna baadhi ya sheria tumetunga ambapo mwizi anakuibia mara moja, lakini ikifika mahali wakati wa kumshughulikia mwizi ambaye una hakika kwamba ameiba, inabidi ufuate taratibu na sheria.

Mheshimiwa Mwenyekiti, inabidi tutafakari kwa kina namna gani tutawashughulikia watu ambao wanafanya ufisadi kwa sababu wakati mwingine sheria zinawalinda sana.

**MWENYEKITI:** Ahsante Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu. Wizara ya Uwekezaji, Viwanda na Biashara, Mheshimiwa Justin Lazaro Nyamoga, Mbunge wa Kilolo, swali lake litaulizwa kwa niaba yake na Mheshimiwa Nancy Nyalusi.

Na. 674

**Sheria Kudhibiti Lumbesa Kwenye Mazao**

**MHE. NANCY H. NYALUSI K.n.y. MHE. JUSTIN L. NYAMOGA** aliuliza:-

Je, lini Serikali italeta Muswada wa Sheria Bungeni ili kudhibiti ujazo wa lumbesa kwenye mazao?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, Wizara ya Ardhi kwa niaba ya Waziri wa Viwanda, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI K.n.y. WAZIRI WA UWEKEZAJI, VIWANDA NA BIASHARA** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Kwa niaba ya Waziri wa Uwekezaji, Viwanda na Biashara, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Justin Lazaro Nyamoga, Mbunge wa Kilolo, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali kupitia Wakala wa Vipimo, inasimamia vipimo katika ununuzi na uuzaji wa mazao kwa mujibu wa Sheria ya Vipimo Na. 340 mapitio ya 2002 na marekebisho yake ya mwaka 2018, kupitia *The Weights and Measures Act (Amendment) Order, G.N. No. 725 of 2018*, iliyorekebisha Sheria ya Vipimo kufuta majedwali ya 10, 11 na 12 na kuingiza jedwali jipya la 10 ambalo chini ya kifungu cha 2 (2) (b) cha Jedwali hilo, mazao ya mashambani yatafungashwa kwa uzito usiozidi kilogramu 100. Hivyo, lumbesa ni ufungashaji wa bidhaa mbalimbali ndani ya kifungashio kwa uzito zaidi ya ule unaokubalika kisheria.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Nancy Nyalusi, swali la nyongeza.

**MHE. NANCY H. NYALUSI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Sheria imeweka wazi na inakataza lumbesa, lakini lumbesa bado inaendelea: Je, Serikali ina mkakati gani wa ziada kuhakikisha kwamba inakomesha ujazo wa lumbesa? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu kwa ufupi.

**NAIBU WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI K.n.y. WAZIRI WA UWEKEZAJI, VIWANDA NA BIASHARA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Napenda kujibu swali la Mheshimiwa Mbunge, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kweli lumbesa ni jambo ambalo siyo la kisheria. Nitoe wito tu kwa wasimamizi wa hizi biashara za vijijini hasa maeneo hayo ambayo wananchi wanakiuka utaratibu, hatua za kisheria zichukuliwe dhidi ya wale ambao wanaweka nje ya kipimo halisi na hasa kwenye mamlaka

hizo za Halmashauri ambako Maafisa Biashara wanasimamia mazoezi haya.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu ya Waheshimiwa Wabunge.

Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na Wizara ya Afya, tulisahau swali Na. 677, Mheshimiwa Husna Juma Sekiboko, Mbunge wa Viti Maalum, sasa aulize swali lake.

Na. 677

**Kulinda afya ya mjamzito na mtoto**

**MHE. HUSNA J. SEKIBOKO** aliuliza:-

Je, ni kwa namna gani Serikali inalinda afya ya mama mjamzito na mtoto mchanga?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Afya, Mheshimiwa Dkt. Godwin Mollel, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA AFYA** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Afya, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Husna Juma Sekiboko, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kulinda afya ya mama mjamzito na mtoto mchanga, Wizara inafanya yafuatayo:-

(1) Kila mama mjamzito anayehudhuria kliniki anapata vipimo muhimu ikiwemo vipimo vya wingi wa damu, shinikizo la damu na kipimo cha protini kwenye mkojo ili kubaini mapema matatizo ya ujauzito;

(2) Matibabu na huduma ya mama mjamzito na watoto chini ya miaka mitano yanatolewa bila malipo katika vituo vyote vya Serikali;

(3) Serikali imeimarisha upatikanaji wa vifaa tiba kwa ajili ya kutibu matatizo yatokanayo na uzazi kwa kufikia asilimia 50 kwa vituo vyote vya kutolea huduma; na

(4) Watoa huduma za afya ya uzazi wamejengewa uwezo ili waweze kutoa huduma stahiki kwa akina mama wanaopata changamoto za uzazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitoe rai kwa wananchi wote hasa akina mama wajawazito kuhakikisha wanahudhuria kliniki na pia kujifungulia katika vituo vya kutolea huduma, ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Husna, swali la nyongeza.

**MHE. HUSNA J. SEKIBOKO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana kwa majibu mazuri ya Serikali, lakini majibu haya ni tamko la sera, ni miongozo ya Serikali, lakini bado huko vijijini akina mama wajawazito wanaendelea kuagizwa kwenda na vifaa vya kujifungulia.

Je, Serikali inatoa tamko gani, kwamba hawa akina mama watakapokosa huduma hizi wachukue hatua gani? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili. Kwa kuwa Mheshimiwa Naibu Waziri amesema kwamba Serikali imeimarisha huduma na wanawake walio wengi vijijini wanapata hizo huduma.

Je, Serikali ipo tayari sasa kutuletea sheria (kwa sababu haya yote ni matamko na miongozo) Bungeni kwa ajili ya kusimamia huduma hizi za mama na mtoto ziweze kutolewa bure? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu kwa ufupi.

**NAIBU WAZIRI WA AFYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nampongeza Mheshimiwa Mbunge kwa swali lake hili zuri ambao ni ukweli unaogusa maisha ya akina mama wetu kila siku. Swali lake la kwanza kuhusu je, wanapokosa huduma tunafanyaje?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza niwaambie tu kwamba, sheria hiyo ipo. Nitoe tamko kwamba suala la akina mama

kupata huduma, mama mjamzito na watoto chini ya miaka mitano ni bure. Pia ni ukweli kwamba kile kipindi ambacho tulikuwa tunapitia kwenye upungufu wa vifaa tiba, pamekuwa pakitokea changamoto hizi ambazo amezisema hapa Mheshimiwa Mbunge. Kama ambavyo nimeeleza kwenye swali la kwanza linalohusu upatikanaji wa vifaa tiba na dawa kutoka kwa Mheshimiwa Halamga, tukiweza kusimamia yale ambayo nimeyasema hapa, nataka kuwahakikishia kwamba suala la akina mama kununua vifaa na vitu vingine havitawezekana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nawaomba tu Waheshimiwa Wabunge, Wakuu wa Wilaya na Wakuu wa Mikoa wote kwa pamoja tushikamane kuhakikisha kwenye Kamati zetu za Ulinzi na Usalama, suala la upatikanaji wa dawa na huduma za afya liwe ni ajenda ya kudumu ili tuijadili. Kwa sababu kwa kweli ikikosekana dawa, huduma zikiwa mbaya, watu watakufa. Kwa hiyo, pia ni suala la kiusalama, wote tulijadili kila wakati na kuhakikisha tunalisimamia kwa pamoja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali lake la pili la kwamba tutunge sheria ya kusimamia hili la akina mama kupata huduma, naomba nilichukue tukalitafakari tuone namna ya kufanya, lakini ninaamini Mheshimiwa Mbunge tukikubaliana pamoja sisi Wabunge na Watanzania wote, tukaja na Muswada wa Bima ya Afya kwa Wote, tunakuwa tumepata mwarobaini wa suala hilo. Maana yake kila mama atakapokuwa na bima yake ya afya, kila familia itakapokuwa na bima yake ya afya, basi matatizo haya mengine yatakuwa yameisha, ahsante.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu ya Waheshimiwa Wabunge.

Tunaendelea na Wizara ya Maliasili na Utalii, Mheshimiwa Antipas Zeno Mgungusi, Mbunge wa Malinyi, sasa aulize swali lake.

Na. 678

**Kuwatumia vijana wa JKT katika uhifadhi**

**MHE. ANTIPAS Z. MAGUNGUSI** aliuliza:-

Je, Serikali haioni haja ya kuwatumia vijana waliopata mafunzo ya JKT kutumikia Jeshi la Uhifadhi kwa mkataba wa muda mfupi?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, Maliasili na Utalii, Mheshimiwa Mary Masanja, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Maliasili na Utalii, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Antipas Zeno Magungusi, Mbunge wa Jimbo la Malinyi, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali kupitia Jeshi la Uhifadhi wa Wanyamapori na Misitu imekuwa ikiajiri Askari wenye taaluma kuu tatu ambazo ni Askari waliohitimu Astashahada ya Wanyamapori, Astashahada ya Misitu na Askari waliohitimu Jeshi la Kujenga Taifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na upungufu mkubwa wa watumishi hususan Askari, SUMA JKT wamekuwa wakiingia mikataba ambayo inawezesha vijana waliohitimu JKT kupata kazi za mikataba kwa shughuli mbalimbali za ulinzi wa maliasili (wanyamapori na misitu). Mfano, kwa sasa Wakala wa Huduma za Misitu Tanzania *(TFS)* wameingia mkataba na SUMA JKT kwa ajili ya kuongeza nguvu ya ulinzi wa misitu kwenye maeneo yenye upungufu mkubwa wa Askari.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Antipas, swali la nyongeza.

**MHE. ANTIPAS Z. MGUNGUSI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru. Nina maswali mawili ya nyongeza. Pamoja na nia njema ya kutumia SUMA JKT kwa ajili ya kuongeza nguvu kwenye

jeshi la uhifadhi na ninajua malipo yao kidogo ni makubwa ukilinganisha na watu ambao wana- *volunteer*; je, Wizara sasa haioni haja ya kutumia vijana ambao wapo kambini au mtaani lakini hawapo SUMA JKT? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili, vijana wetu waliomaliza elimu ya wanyapori kwa maana ya Mweka, Pasiansi na Olmotonyi ambao wapo mtaani kwa sasa, Wizara haioni haja ya kuwapa mkataba wa muda mfupi na kuwalipa posho? Ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu wa ufupi.

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nimtoe wasiwasi Mheshimiwa Mbunge, pamoja na kuwa ni Mhifadhi Mkuu na amekuwa akitumikia Serikali kwa miaka ya nyuma akiwa Mhifadhi, lakini kwa sasa hivi Serikali ilishaanza kuwatumia hao vijana wa JKT. Hivi ninavyoongea, tayari taasisi zinaajiri. Pia tumeanzisha makampuni ambayo vijana ambao hawajapata ajira za Serikali wanaingizwa kule na taasisi zetu zinachukua vijana kutoka kwenye makampuni hayo. Kwa hiyo, utaratibu huu tunaendelea nao. Wale waliopo kambini tunawatumia pia kwa ajili ya doria za muda mfupi pale ambapo inapojitokeza changamoto za wanyama wakali na waharibifu.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Tunaendelea na Wizara hiyo hiyo. Mheshimiwa Muharami Shabani Mkenge, Mbunge wa Bagamoyo, sasa aulize swali lake.

Na. 679

**Ukarabati wa majengo ya magofu ya Bagamoyo**

**MHE. MUHARAMI S. MKENGE** aliuliza:-

Je, lini Seriikali itafanya ukarabati wa majengo ya magofu ya Bagamoyo ili yasianguke na kuleta madhara?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Maliasili na Utalii, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Muharami Shabani Mkenge, Mbunge wa Jimbo la Bagamoyo, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na umiliki wa majengo mengi katika eneo la Bagamoyo kuwa chini ya usimamizi na umiliki wa mamlaka mbalimbali ikiwemo watu na taasisi binafsi, Wizara imeendelea kuwahamasisha wadau wote kufanya ukarabati usioathiri mwonekano au kuharibu historia hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hadi sasa tayari wadau wanne wamepewa vibali vya kufanya ukarabati wa majengo yao ndani ya Mji Mkongwe wa Bagamoyo. Aidha, Wizara kwa kushirikiana na Mamlaka ya Mji Mkongwe wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, ipo katika mpango wa kulifanyia ukarabati mkubwa jengo la Ngome Kongwe baada ya kufanyiwa uokoaji kwa kuliimarisha jengo hilo.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Muharami, swali la nyongeza.

**MHE. MUHARAMI S. MKENGE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, nina swali moja la nyongeza pamoja na ombi moja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali. Mheshimiwa Naibu Waziri amesema kwamba Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa kushirikiana na Mji Mkongwe watafanya ukarabati wa lile Jengo la Ngome Kongwe ya Bagamoyo; je, ni lini kazi hiyo itaanza rasmi kufanyika? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ombi. Wananchi wa Kaole na Wazee wa Kaole Bagamoyo wamenituma; wanashukuru sana kwa eneo lao kuwa eneo maarufu kwa utalii wa malikale, lakini ombi lao ni kwamba pale pana msikiti wa miaka mingi, kwa hiyo, wanaomba ule msikiti uhesabike kama misikiti mingine na watalii pamoja na watu wengine watakapokuja wavue viatu ili watakapoingia mle ndani ili kutunza mila na utamaduni wa misikiti katika Mji wa Kaole Bagamoyo. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, jibu swali moja la nyongeza.

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Mwenyekiti, awali nampongeza sana Mheshimiwa Muharami, Mbunge wa Bagamoyo kwa namna ambavyo anaendelea kutunza historia hususan ya malikale. Pia nawaomba wananchi wa Bagamoyo tuendelee kushirikiana kwa pamoja, kulinda na kuendeleza hizi malikale tulizoachiwa na waasisi wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala hili la lini kazi hii itafanyika kwa mashirikiano na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, niwaahidi tu wanachi wa Bagamoyo, kwa mwaka wa fedha unaokuja ambapo tayari bajeti tumeshapitishiwa, tutaanza ukarabati wa jengo hili. Kwa hili la msikiti natoa tu maelekezo hapa hapa kwamba Mkurugenzi wa Maliakale ashirikiane na viongozi walioko katika Wilaya ya Bagamoyo kuhakikisha anatoa maelekezo kwamba msikiti huu ni sawa na misikiti mingine na heshima zinazotakiwa kama msikiti watu waingie bila viatu, basi utekelezaji wake uanze mara moja, ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Wizara hiyo hiyo, Mheshimiwa Peter Cherehani, Mbunge wa Ushetu sasa aulize swali lake.

Na. 680

**Mgogoro wa mpaka kati ya Pori la *Usumbwa Forest Reserve* na Hifadhi ya Pori la Kigosi Moyowosi**

**MHE. EMMANUEL P. CHEREHANI** aliuliza:-

Je, lini Serikali itamaliza mgogoro wa mpaka wa Pori la *Usumbwa Forest Reserve* na Hifadhi ya Pori la Kigosi Moyowosi - Ushetu?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Maliasili na Utalii, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Emmanuel Peter Cherehani, Mbunge wa Jimbo la Ushetu, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Pori la *Usumbwa Forest Reserve* ambalo kwa sasa ni hifadhi ya Taifa Kigosi haina mgogoro wowote wa mpaka na wananchi wa Ushetu. Kwa sasa kilichopo ni wananchi wa Ushetu waliwasilisha maombi ya kumegewa eneo, ambapo Serikali inaendelea na tathmini na pindi litakapokamilika, wananchi watajulishwa. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Cherehani, swali la nyongeza.

**MHE. EMMANUEL P. CHEREHANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Kwa kuwa wananchi hawa walizoea kufanya shughuli zao za kibinadamu wakati pori hili halijaingizwa kwenye Hifadhi ya Taifa *TANAPA*; tathmini hii sasa itakamilika lini, kwa sababu nimekuwa nikiahidiwa kila mara, ili wananchi waweze kumegewa eneo lao waweze kuendelea kufanya shughuli za kibinadamu hasa katika Kata ya Ulewe, Kata ya Ubagwe na Kata ya Idahina? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali langu la pili. Kamishna wa Ardhi katika Mkoa wa Shinyanga kakamilisha tathmini katika Pori la Ubagwe *Forest Reserve* katika mpaka wa Kaliua ambapo sasa inahitajika gharama ya kwenda kuhakikisha wanaweka mipaka ili kuondoa mgogoro pia uliopo katika eneo hili. Serikali lini sasa itapeleka fedha ili mipaka hii iweze kuwekwa? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nampongeza sana Mheshimiwa Mbunge. Ushetu nilifika na nilizungumza na wananchi wa pale na tuliwaahidi kwamba migogoro hii tunaishughulikia. Kwenye upande wa eneo hili ambalo wananchi wanadai, nataka tu niwaambie wananchi wa Ushetu kwamba wakati *Usumbwa Forest Reserve* ikiwa kwenye hadhi ya msitu kwa maana ya Wakala wa Huduma za Misitu Tanzania wanalisimamia, pori hili lilikuwa

linaruhusu shughuli za kibinadamu na hadhi yake tulikuwa tunaruhusu ufugaji wa nyuki na wananchi walikuwa wanarina asali katika maeneo hayo. Ndiyo maana leo hii wananchi wanaona ni kama walinyang'anywa, lakini hadhi ya pori ilibadilishwa kutoka kwenye *forest reserve,* ikapanda kuwa *National Park. National Park* inazuia shughuli za kibinadamu ndani yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, kwa sasa hivi tunaangalia utaratibu wa kuyashusha hadhi baadhi ya maeneo ili wananchi waendelee kuanza kupata faida ya uhifadhi, na pia waendelee kufuga nyuki kwa ajili ya kurina asali. Kwa hiyo, niwatoe wasiwasi wananchi wa Ushetu, suala hili tunalishughulikia na Mbunge wao amekuwa akiliulizia mara kwa mara. Kwa hiyo, muda siyo mrefu tunatarajia kuleta azimio Bungeni. Nadhani kuna baadhi ya maeneo yatashushwa hadhi na wananchi wataanza kufaidika na urinaji wa asali. Kwenye suala hili la lini tutaweka mipaka, kwa kuwa tathmini tayari imeshakamilika ni wakati wowote tu kuanzia sasa. Kwa kuwa ni jukumu letu Wizara ya Maliasili na Utalii kuweka mipaka, basi tutaendelea kuainisha mipaka halisi, ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Bupe Mwakang'ata swali la nyongeza.

**MHE. BUPE N. MWAKANGA'ATA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali dogo la nyongeza. Kwanza kabisa nichukue nafasi hii kuipongeza Serikali kwa kumaliza mgogoro wa uwanda wa *game reserve* Mkoani Rukwa lakini nina swali dogo la nyongeza. Je, ni lini sasa Serikali itapunguza tozo za *token* ambazo wananchi wanalipa wanapoingia kuvuna na kutoka? Ni lini Serikali itapunguza hizo tozo? Ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu kwa ufupi.

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Mwenyekiti, niwashukuru kwa sababu mgogoro huu umeisha. Kwenye suala la *token* sasa tutaenda uwandani kuangalia ni jinsi gani tukae na wadau ili tuone bei ambayo ni nzuri zaidi kwa wao

na kwetu sisi twende sambamba na mahitaji ya wananchi, ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, ahsante sana kwa majibu ya Waheshimiwa Wabunge, tunakushukuru sana.

Waheshimiwa Wabunge, tumefika mwisho wa kipindi cha maswali na majibu, ninayo matangazo machache. Tangazo la kwanza ni wageni waliopo Bungeni asubuhi hii.

Kwanza ni wageni waliopo Jukwaa la Spika ambaye tunaye Mheshimiwa Juma Nhunga – Mbunge Mstaafu wa mwaka 1985 hadi 2010 ambaye pia ni Mjumbe wa Tume ya Utumishi wa Bunge na Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge ya Haki, Maadili na Madaraka ya Bunge. Vilevile alikuwa Katibu wa Wabunge wa CCM, ahsante sana, karibu sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, tunao wageni wa Waheshimiwa Wabunge; wageni sita wa Mheshimiwa Ummy Mwalimu ambaye ni Waziri wa Afya ambao ni baadhi ya wachezaji wa Timu ya *Young Africans* na viongozi kutoka Taasisi ya Wape Tabasam, karibuni sana. *(Makofi)*

Wapo wageni watano wa Mheshimiwa Abdallah Ulega, Waziri wa Mifugo na Uvuvi kutoka Kiwanda cha *Nannan Shoes International Company Limited* kilichopo Mkuranga, Mkoa wa Pwani wakiongozwa na mmiliki wa kiwanda hicho Ndugu Fu Wenhong, karibuni sana. *(Makofi)*

Wapo wageni watatu wa Mheshimiwa Jumanne Sagini ambaye ni Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi kutoka Butiama Mkoa wa Mara, karibuni sana. *(Makofi)*

Wapo wageni 73 wa Mheshimiwa Fredy Mwakibete, Naibu Waziri wa Uchukuzi ambaye ni watoto wa *Sunday School* kutoka Kanisa Kuu la KKKT Dodoma, ahsante na karibuni sana. *(Makofi)*

Tunao wageni 44 wa Mheshimiwa Profesa Patrick Ndakidemi ambao ni Sekretarieti ya CCM Wilaya ya Moshi na viongozi wa

CCM Kata, Makatibu wa Mbunge kutoka Moshi Mkoa wa Kilimanjaro, karibuni sana. *(Makofi)*

Tunao wageni 37 wa Mheshimiwa Angelina Malembeka kutoka Taasisi ya Chawa wa Mama kutoka Kinondoni Jijini Dar es Salaam, ahsante karibuni. *(Makofi)*

Tunao wageni 61 wa Mheshimiwa Ahmed Shabiby ambao ni Umoja wa Vijana wa CCM kutoka Gairo wakiongozwa na Mwenyekiti wa UVCCM Wilaya ya Gairo, karibuni sana. *(Makofi)*

Tunao wageni nane wa Mheshimiwa Abdul-Hafar Idrissa Juma ambao ni watoto wake kutoka Zanzibar Mjini Magharibi, karibuni sana. *(Makofi)*

Tunao wageni saba wa Mheshimiwa Flatei Massay ambao ni wadau wa maendeleo kutoka Mbulu Vijijini, karibuni sana. *(Makofi)*

Tunaye mgeni wa Mheshimiwa Asia Halamga ambaye ni mtoto wake kutoka Jijini Dar es Salaam, ahsante sana na karibu. *(Makofi)*

Wako wageni waliotembelea Bunge kwa ajili ya mafunzo, tuna wanafunzi na walimu 130 kutoka Shule ya Msingi *Royal Elite* ya Jijini Dar es Salaam wakiwemo watoto wa Mheshimiwa Janeth Mahawanga ambao ni Abdulrahman Pongolani na Raisa Pongolani, ahsante karibuni sana, sana. *(Makofi)*

Yuko Ndugu Germin Mathew kutoka Mbozi Mkoa wa Mbeya, karibu sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, kuna tangazo kutoka kwa Katibu wa Wabunge wa CCM anawatangazia Waheshimiwa Wabunge wote wa CCM kwamba kutakuwa na kikao maalum cha *party caucus* leo Jumanne saa 7.00 mchana katika Ukumbi wa Pius Msekwa baada ya shughuli za Bunge kuahirishwa wote mnatakiwa kufika bila kukosa katika kikao hicho muhimu.

Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na ratiba iliyo mbele yetu.

Katibu.

**NDG. RUTH MAKUNGU – KATIBU MEZANI:**

**MISWADA YA SHERIA YA SERIKALI**

**Muswada wa Sheria ya Fedha wa Mwaka 2023**
***(The Finance Bill, 2023)***

*(Kusomwa Mara ya Kwanza)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Waheshimiwa Wabunge, kwa mujibu wa Kanuni ya 96(1) Muswada wa Sheria ya Fedha kwa Mwaka 2023 umesomwa kwa mara ya kwanza. Hivyo kwa mujibu wa Kanuni ya 97(1) Muswada huu sasa utapelekwa kwenye Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Bajeti kwa ajili ya kufanyiwa kazi mara moja hivyo naelekeza Muswada huu kwenda kwenye Kamati ya Bajeti kwa ajili ya kufanyiwa kazi mara moja.

Katibu.

**NDG. RUTH MAKUNGU – KATIBU MEZANI:**

**HOJA ZA SERIKALI**

**Hali ya Uchumi wa Taifa kwa Mwaka 2022 na Mpango wa Maendeleo wa Taifa kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024**

**na**

**Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Serikali kwa Mwkaa wa Fedha 2023/2024**

*(Majadiliano Yanaendelea)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na mjadala ulio mbele yetu hoja ambayo ni Bajeti Kuu ya Serikali kwa

mwaka wa fedha 2023/2024. Hapa ninayo orodha ya Waheshimiwa Wabunge kwa ajili ya kuchangia. Tutaanza na Mheshimiwa Mashimba Mashauri Ndaki atafutatiwa na Mheshimiwa Bonnah Ladislaus Kamoli, Mheshimiwa Kenneth Ernest Nollo ajiandae.

**MHE. MASHIMBA M. NDAKI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kunipa nafasi ili niweze kuchangia bajeti ya mwaka 2023/2024. Kwanza nichukue nafasi hii kumpongeza sana Mheshimiwa Rais wetu Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa uimara wake katika kukuza uchumi wa nchi yetu kwa kuendelea kutekeleza miradi mbalimbali ya maendeleo ambayo inaendelea kwenye nchi yetu, lakini pia kuanzisha miradi mingine kwa ajili ya maendeleo ya nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia nimpongeze kwa ajili ya kuendelea kuhakikisha nchi yetu inakuwa salama na nchi yetu inaendelea kutawaliwa huku akijali sana utawala bora. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nichukue nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Waziri wa Fedha na Mipango kwa kututayarishia Bajeti hii ambayo kusema ukweli kama itakwenda kutekelezwa kama ambavyo imesomwa hapa baada ya marekebisho ya Waheshimiwa Wabunge nadhani itakuwa ni Bajeti tulivu na Bajeti ambayo ninaamini itapeleka nchi yetu mbele kwa mwaka ujao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niwapongeze pia Waheshimiwa Mawaziri wote chini ya Kiongozi na Jemedari wao Mkuu Rais wetu Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kuendelea kutekeleza majukumu yao ya msingi kuhakikisha nchi yetu na Watanzania kwa ujumla wanapata maendeleo kwa kusapotiwa na Serikali yao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka kuzungumzia suala moja tu siku ya leo na jambo lenyewe ninalotaka kuzungumzia ni bei za mazao hasa mazao ya kilimo. Nataka kuzungumzia jambo hili kwa sababu mazao yetu ya kilimo ni muhimu sana kwa nchi yetu, ni muhimu sana kwa wananchi, ni muhimu sana kwa maendeleo ya nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nichukue nafasi hii kumpongeza sana Mheshimiwa Waziri wa Kilimo Mheshimiwa Bashe kwa ubunifu wake na namna ambavyo anaendelea kutekeleza shughuli zinazohusiana na mambo ya kilimo kweye sekta yake. Serikali imefanikiwa kutoa ruzuku kwa mbolea, tunaipongeza sana lakini Serikali imefanikiwa kutoa viuatilifu kwa ajili ya wakulima wanaohitaji viuatilifu hivyo maeneo mbalimbali. Sisi kwa upande wetu tumepata viuatilifu kwa ajili ya zao la pamba na tumepewa bure, tunamshukuru sana Mheshimiwa Rais lakini tunampongeza sana Mheshimiwa Waziri wa Kilimo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia tunamshukuru sana Mheshimiwa Rais kwa kuongeza Bajeti ya Kilimo mwaka uliopita na hata mwaka ambao tunajadili Bajeti yake. Mwaka uliopita bajeti ilikuwa shilingi bilioni 920 hivi, mwaka huu ni shilingi bilioni 970. Tunaamini kama fedha hizi zitatolewa na Serikali zikaenda kutekeleza miradi ya maendeleo inayohusiana na kilimo tunaamini tutapiga hatua na pengine tutafikia lengo la kukuza uchumi kwa 5% badala ya 3% ambayo tumefikia sasa hivi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lengo la kufanya haya ni nini? Lengo la kufanya haya ni kuongeza uzalishaji wa mazao ya kilimo na mimi naamini kwa hatua hizi ambazo zinachukuliwa na Serikali uwezekano mkubwa kabisa wa kuongeza uzalishaji wa mazao ya kilimo upo. Inawezekana kabisa tukaongeza kwa sehemu kubwa sana. Sasa mazao yetu haya ya kilimo ni muhimu sana kwa mambo mbalimbali. Moja; yanaendelea kuajiri Watanzania. Pili; yanaendelea kutupatia kipato kama Watanzania, asilimia kama 65 tunapata maisha yetu kutoka kwenye mazao ya kilimo, kutoka kwenye kilimo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mazao haya ya kilimo pia ni muhimu kwa sababu haya ndiyo yanayotuletea fedha za kigeni hapa nchini kwetu. Tulikuwa na nakisi ya Serikali juu ya uagizaji na uuzaji wa mazao yetu nje kiasi cha dola milioni 5,000 hivi lakini mazao ya kilimo yametusaidia sana kutuletea fedha za kigeni ili kupunguza nakisi yetu kati ya biashara na nchi zingine. Hii inatusababisha tuwe na mfumuko wa bei kidogo pia tuwe na

fedha za kigeni zinazototosheleza kununua mahitaji yetu mbalimbali tunayoyahitaji kutoka kwa wenzetu nje. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano mwaka wa 2021 korosho imetuletea dola milioni 226.9, ongezeko kutoka dola 159 mwaka 2021. Katani mwaka 2021 imetuletea 127, mwaka wa 2022 imetuletea 178.5, pamba imetuletea dola 103.4 mwaka wa 2022 ongezeko kutoka dola milioni 81.3. Kwa hiyo, mazao haya yana umuhimu mkubwa sana kwa nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa tunapokuja kwenye bei wanazolipwa wakulima wetu hapa ndani ya nchi kusema ukweli bado kwenye eneo hili hatujafanya vizuri. Malipo wanayopata wakulima wetu ni malipo kidogo ukilinganisha na nguvu wanayoiweka kwenye hicho kilimo, ukilinganisha na gharama wanayoiweka kwenye hicho kilimo, ukilinganisha na muda wanaotumia ili kuvuna hayo mazao na hii wakati mwingine inaweza kuwa ni kwa sababu zilizo nje ya uwezo wa Serikali au nje ya uwezo wa mkulima wenyewe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatizo la bei linatatulika, mwaka 2020/2021 bei ya korosho kwa mfano, korosho mkulima aliuza kati ya shilingi 3,400 mpaka 3,600 mwaka 2020/2021 lakini 2021/2022 mkulima ameuza korosho yake bei ya shilingi 1,400 mpaka shilingi 1,800 anguko kubwa sana hili karibu linakaribia nusu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mkulima wa pamba 2021/2022 bei aliyouzia pamba yake ni shilingi kati ya 1,560 mpaka 2,200 bei ilikuwa nzuri lakini msimu huu 2022/2023 bei ya pamba ni shilingi 1,060 na hatujui kama itakwenda kupanda, anguko la nusu zaidi ya nusu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa hii inakatisha tamaa wakulima wetu, inakatisha tamaa wasilime tena msimu ujao lakini pia inafanya wawe na kipato kidogo na inawafanya waendelee kuwa wanyonge kwenye nchi ingawa mchango wao, mchango wa mazao wanayozalisha ni mkubwa na unaisaidia na kuifaidisha nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nilikuwa naomba Serikali iingilie kati kwenye bei za mazao haya kwa kuanzisha *price stabilization fund. (Makofi)*

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana.

**MHE. MASHIMBA M. NDAKI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naona umewasha kinanii chako, naomba nimalizie tu nusu dakika. Ianzishe *price stabilization fund* ili kuwasaidia wakulima hawa bei za mazao yao zinapoanguka na hili siyo wazo geni ni wazo linalofanywa na nchi zilizoendelea na maeneo mengine. Kwa hiyo, sisi hapa tunaweza kufanya hivyo pia tena kwa kuwachaji wakulima wakati bei za mazao haya zinapokuwa ziko juu lakini pia Serikali inaweza ikaweka ruzuku ili kufidia bei zinapoanguka. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa ahsante sana.

**MHE. MASHIMBA M. NDAKI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru ahsante sana naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Nimemtaja Mheshimiwa Bonnah Ladislaus Kamoli atafuatiwa na Mheshimiwa Kenneth Ernest Nollo, Mheshimiwa Selemani Jumanne Zedi ajiandae.

**MHE. BONNAH L. KAMOLI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante nami naomba nichangie hii Bajeti ya Wizara ya Fedha. Kwanza nichukue nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Rais wetu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan lakini pia nimpongeze Mheshimiwa Waziri kwa kazi kubwa ambayo ameifanya katika hii bajeti. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kutoa shukrani zangu za dhati kwa niaba ya Wananchi wa Jimbo la Segerea Kata ya Kipunguni kwa Mheshimiwa Waziri kuiweka Bajeti ya Malipo ya Fidia ya Kipunguni Kata ya Kipawa kwenye hii Bajeti, tunashukuru sana sana kwa sababu hawa wananchi wamekaa muda mrefu bila kupata malipo yao takribani miaka 30. Kwa hiyo, Mheshimiwa

Waziri tunakushukuru lakini tunaomba ulisema utapeleka wakaguzi ambao wanatoka Wizara ya Fedha tulikuwa tunaomba uwapeleke kwa haraka ili hawa wananchi waweze kupata fedha zao na ikiwezekana mwezi wa, huu tuko mwezi wa sita basi mwezi wa saba waweze kuanza kulipwa Mheshimiwa Waziri tutashukuru sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine nililokuwa nataka kuongelea ni kuhusiana na barabara. Barabara za *DMDP* ambazo nimekusikia Mheshimiwa Waziri umeziingiza kwenye Bajeti ya mwaka huu tunashukuru sana. Nimekuwa nikichangia hapa kwa muda wa miaka karibuni mitano kuhusiana na Barabara za *DMDP*. Mkoa wetu wa Dar es Salaam Mheshimiwa Waziri unategemea sana miundombinu na tunapata wawekezaji wengi kuja kuwekeza kwenye nchi yetu lakini lango kubwa ambalo wanatumia ni kwanza wanaingia Dar es Salaam na wanapitia katika *Airport* yetu, *Airport* ya Dar es Salaam *International Airport*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa ukiangalia mazingira ya Mkoa wa Dar es Salaam kuhusiana na miundombinu kwa kweli imekuwa hairidhishi. Kwa hiyo, kitu ambacho tunaomba pamoja na kwamba umeweka barabara kwenye hii Bajeti basi tunaomba ianze haraka kwa sababu kumekuwa kuna ucheleweshaji sana. Mfano kama mkitangaza hizi miundombinu au mkitangaza Bajeti kwamba kuna barabara zitajengwa hazianzi wakati huo huo zinakuwa zinachukua hata miezi sita Mheshimiwa Waziri au hata mwaka. Kwa hiyo, kwa sababu sasa hivi wananchi wetu wengi wamesikia kwamba kuna barabara sasa zinaenda kutengenezwa, barabara za *DMDP*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo tunaomba kwa kuwa Mheshimiwa Waziri mmetangaza na mmesaini, na kupongeze sana pia nimpongeze Waziri wa TAMISEMI. Waziri wa TAMISEMI Mheshimiwa Angellah Kairuki alikuja kufanya ziara katika Jimbo langu la Segerea. Unaweza ukaona Mheshimiwa Waziri kwamba Jimbo la Segerea lipo mjini lakini ukitembelea maeneo yake mengi ni barabara kama ziko vijijini. Kwa hiyo Mheshimiwa Waziri ameziona na ameona jinsi gani wananchi wanahangaika kutokana na barabara kuwa mbovu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo tunamuomba sana Mheshimiwa Waziri hii bajeti ambayo ameisoma na ameweka miundombinu tunaomba hiyo miundombinu iende ikatengenezwe kwenye Mkoa wa Dar es Salaam.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ambalo nataka kuongelea ni kuhusiana na wakandarasi wetu. Mkoa wetu wa Dar es Salaam miundombinu yake au jiografia yake ni kama unavyoiona. Inakuwaje barabara inatengenezwa na inakuwa mpya lakini mvua ikinyesha masaa mawili unashangaa maji yamejaa Dar es Saalam nzima na inaweza ikasababisha masaa matatu hakuna kitu chochote kinachofanyika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kwa hiyo tunaomba hata hawa wakandarasi ambao wanaenda kututengenezea sasa hizi barabara wazingatie jiografia ya Mkoa wa Dar es Salaam. Kwa sababu kuna sehemu nyingine kwa mfano Jimbo la Segerea kuna miinuko na milima mingi. Sasa tunaomba wakandarasi wawe wanaangalia sehemu ambazo wanaenda kutengeneza barabara ili sasa kuondoa yale matatizo, kwamba barabara ikishatengenezwa basi hayo maji yasijae.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ambalo nataka kuliongelea ni kuhusiana na taasisi hizi mbili ambazo zote ni za Serikali; maji pamoja na miundombinu. Unaweza ukashangaa barabara imejengwa haina hata miezi miwili nao watu wa *DAWASA* wanakuja wanchimba kwenye ile ile barabara ambayo imejengwa haina hata miezi miwili. Kwa hiyo mimi napendekeza; hizi taasisi zote mbili ni taasisi za Serikali, kwa hiyo kwa nini zisiwe zina mawasiliano ya karibu? Kwamba sisi sasa hivi tunataka kujenga hapa barabara je, kuna bomba lolote la maji ambalo linaweza kupita, kwa sababu linaleta usumbufu mkubwa sana. Na yale mashimo ambayo wanachimba watu wa *DAWASA* yanakaa muda mrefu sana na yanasababisha watu wanapata ajali. Kwa hiyo tunaomba barabara kama inajengwa watu wa *DAWASA* wawe wameshapita na kuweka mabomba yao, tunaomba sana. Hilo pia litasaidia hata Serikali kutokupata hasara kwa sababu barabara inapojengwa halafu tena inaenda inabomolewa ina maana kuna hasara ambayo inaongezeka hapo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ambalo nataka kuliongelea ni kuhusiana na *TARURA*. Tunashukuru sana *TARURA* kwa kipindi kirefu imekuwa ikipata hela bajeti ambayo si kubwa lakini sasa hivi naona mmeongeza bajeti. Kwa hiyo tunaomba hiyo bajeti ambayo imewekwa kwenye *TARURA* iende ikafanye kazi kwa haraka. Jambo lingine ni kuhusiana na fedha ambazo zinakusanywa na halmashauri, zile asilimia 10, tulisema kwamba kuna fedha ambazo zinaenda kwenye barabara. Sasa kumekuwa katika kipindi hiki cha kama miezi sita kuna hela ambazo zimepelekwa kwa mkurugenzi kwa ajili ya kutengeneza barabara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa hizi fedha ambazo zinapelekwa kwa Mkurugenzi, sasa hivi tangu imeanzishwa Taasisi ya *TARURA* mkurugenzi hana mainjinia, kwa hiyo kumekuwa kuna tatizo la ucheleweshaji wa barabara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano kwenye Jimbo langu la Segerea kuna barabara ambazo tulikuwa tumezitembelea tangu mwaka jana ambazo zilikuwa zimewekwa ili zitengenezwe na halmashauri kutokana na ile asilimia, lakini mpaka sasa hivi ninavyoongea hizo barabara hazijatengenezwa kwa sababu kumekuwa kuna ucheleweshaji kati ya *TARURA* na halmashauri. Halmashauri sasa hivi hawana mainjinia, kwa hiyo tunaomba hizi fedha ziendelee kupelekwa *TARURA*. Kwa sababu jambo hili unafuatilia halmashauri halafu ukifika Mkurugenzi anakwambia mimi sina injinia, kwa iyo inabidi urudi *TARURA*. Kwa hiyo kumekuwa na ucheleweshwaji sana. Kama mlikuwa mnapeleka hizi fedha *TARURA* basi tunaomba tu muendelee kupeleka *TARURA* hizi fedha ili watu waweze kuendelea kupata barabara kwa haraka pia *TARURA* waweze kufanya kazi yao vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ambalo nataka kuongelea ni mifumo ya halmashauri. Sasa hivi mwezi mzima hakuna kitu kinafanyika shughuli zimelala, mifumo yote haisomi. Kwa hiyo tulikuwa tunaomba, sijui ni jambo gani Mheshimiwa Waziri, naomba ulishughulikie. Kwa sababu kama mwezi mzima mifumo ikiwa haisomi ina maana hata itakapofunguliwa unaweza ukakuta kuna mapato yamepotea au kuna wizi umetokea mpaka mje mgundue inakuwa ni imechukua muda. Kwa hiyo tunaomba ulishughulikie jambo hilo ili mifumo iweze kusoma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ni kuhusiana na sheria za kodi. Nafikiri hizi sheria za kodi kama zingepitiwa upya hata kusingekuwa na migogoro ambayo inaenda kutokea, kwa mfano kama mgogoro uliotokea Kariakoo kuhusiana na wafanyabiashara, na Iringa. Napendekeza, kama inawezekana hizi sheria ziletwe Bungeni ili tuweze kuzipitia upya ili ziweze kuwa sheria rafiki. Hii ni kwa sababu hii migogoro itakuwa inaendelea kila siku. Nampongeza sana Mheshimiwa Waziri Mkuu kwenda kumaliza huu mgogoro ambao ulitokea Kariakoo. Kwa hiyo tunaomba sana sheria hizi uangalie Mheshimiwa Waziri ili ziweze kuwa ni sheria rafiki ili tuweze kuendelea na mambo mengine ambayo yanaweza yakatuingizia kipato kwenye nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ni kuhusu elimu. Nampongeza sana Mheshimiwa Rais Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa fedha ambazo zimekuja katika Jimbo letu la Segerea pia Mkoa wa Dar es Salaam mzima. Katika Jimbo langu la Segerea tumepata fedha nyingi sana kwa mwaka ambao umepita na tumejenga miundombinu mingi sana ya elimu. Na mpaka sasa hivi tunajenga maghorofa matatu kwa ajili ya sekondari. Pia tunajenga madarasa mengi kwa kutumia fedha ambazo zimekuja kwa ajili ya elimu. Kwa hiyo…

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana.

**MHE. BONNAH L. KAMOLI: …**tunamshukuru sana Mheshimiwa Rais pia tunakushukuru Mheshimiwa Waziri naunga mkono hoja.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana, nimemwita Mheshimiwa Kenneth Ernest Nollo atafatiwa na Mheshimiwa Selemani Jumanne Zedi, Mheshimiwa Simon Songe Lusengekile ajiandae.

**MHE. KENNETH E. NOLLO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, na mimi nikushukuru kwa dhati kwa kunipatia nafasi niweze kuchangia bajeti ya mwaka 2023/2024. Kwanza nianze kwa kumpongeza Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa namna ambavyo ameendelea kupambana na kuimarisha nchi yetu, hasa katika eneo zima la uchumi. Sote ni

mashahidi katika nchi za Afrika Mashariki ukiacha *indicator* zingine lakini sisi ndio tumekuwa na nafuu kubwa ya kuwepo na kiasi cha dola kwenye nchi yetu. Pamoja na miradi mikubwa tunayoifanya tumeweza kustahimili. Na kama nilivyosema, pamoja na upungufu tuna *reserve* ya dola kwenye nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitumie nafasi nimpongeze Waziri wa Fedha ndugu yangu Mwigulu Nchemba kwa namna ambavyo ameendelea na utekelezaji wa masuala mbalimbali ya kiuchumi, na nchi yetu imeendelea kustahimili na kuweza kuimarika katika maeneo mbalimbali ya kiuchumi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine nimpongeze sana Mheshimiwa Rais na Serikali kwa ujumla kwa kuamua kuirudisha Tume ya Mipango. Jambo hili limesemwa sana na Waheshimiwa Wabunge kipindi kilichopita. Kwa vyovyote vile, Tume ya Mipango ni kitu cha msingi, ni taasisi ya msingi katika kuangalia maeneo gani Serikali ifanye na kuangalia dira katika upana mkubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Tanzania inaongozwa na mama Samia, dira na maono ya nchi yetu yeye ndiye amevishikilia. Lakini ni wapi anaposhusha, anashusha pale kwenye Tume ya Mipango. Kwa hiyo mimi nataka niseme kwamba pamoja na kwamba sasa Tume ya Mipango imerejea utekelezaji wake uanze haraka. Kazi ya Tume ya Mipango ni kwanza kupanga, kufatilia na kufanya *evaluation,* kuona maeneo gani ambayo tunafanikiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilitaka niseme kwenye suala zima la upungufu wa dola, fedha za kigeni hapa nchini. Sote ni mashahidi kwamba tuna miradi mikubwa. Ni kweli kwamba tunatumia fedha nyingi kuagiza vifaa vya ujenzi. Lakini vilevile bado tuna tatizo la kununua vyakula na hata mafuta ya kula kutoka nje ya nchi. Tunanunua sana ngano kutoka nje ya nchi kwa kipindi kirefu, tunaagiza mafuta ya kula ya kutosha kutoka nje ya nchi, mbolea, dawa na vitu vingine vyote. Suala hili linasababisha kutozalisha sisi wenyewe ili tuweze kuzuia matumizi ya dola nje ya nchi. Vilevile hatuzalishi tuweze ku-*export* kile tunachokizalisha katika nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa naishauri sana Serikali; katika suala zima la uwekezaji tuendelee kuweka mazingira mazuri kwa kutoa *incentives* kwa wawekezaji wetu. Lakini kubwa zaidi bado ziko changamoto. Changamoto kubwa tulionayo kwenye uwekezaji ni suala zima la ardhi. Wanakuja wawekezaji wanataka kuwekeza lakini kinacholeta kikwazo ni kwamba *TIC* hana ardhia ambayo anaweza akampa mwekezaji, na bahati mbaya mifumo hii hai-*link*. Wizara ya Ardhi na *TIC* bado hawakai pamoja. *TIC* anamleta mwekezaji anamwahidi kuja kuwekeza lakini ikija hapa inachukua miaka mingi kuweza kulipa fidia kwa wakulima wetu au kwa watu walioshikilia ardhi. Kwa hiyo jambo hili tuliangalie.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine, zipo kampuni kubwa zenye uwezo wa kuzalisha hapa nchini katika baadhi ya maeneo ambayo ni nyeti, iwe katika eneo la vioo, *glass* na mambo mengine. Serikali inaweza kuongea nao, kwamba, je kama tukiwapa mtaji zaidi mnaweza mka-*double production?* Na tukaangalia, yapo maeneo tunaweza tukauza. Sisi katika nchi za *SADC* ni wazalishaji wakubwa katika maeneo mbalimbali. Masoko yetu tunayo; Congo ni soko letu kubwa. Tunafanyaje ili tuweze kuongeza uzalishaji na tuweze kupata fedha za kigeni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine, Serikali ilileta hapa Sheria ya *Local Content* lakini sheria hii haisimamiwi katika maeneo mbalimbali. Bado kuna *material* ya kwenye viwanda yanaagizwa kutoka nje ilhali katika nchi yetu yapo. Sasa kwa mfano kwenye *cement* tulikuwa tunatumia chuma ya hapa nchini. Imetokea gafla sasa viwanda vinaagiza *clinker* kutoka nje ya nchi. Mimi katika jimbo langu tulikuwa tunazalisha sana chuma ambayo tulikuwa tunatumia kwenye viwanda vya hapa nchini, sasa hatuzalishi halitoki hata lori moja. Sasa mambo kama haya tungeweza kuzuia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile yapo madini mbalimbali ambayo yanapatikana kwa wingi katika nchi yetu, bado nayo tumeruhusu viwanda vinaamua kuweza kuleta hapa nchini, jambo hili tuliangalie.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine nimelesema sana kwenye suala zima la nyama. Dodoma sisi tuna kiwanda cha machinjio ya Kizota, na bahati mbaya sisi baadhi ya nchi zimetufungia tusipeleke nyama kwenye nchi zao kwa sababu ya machinjio yalivyokuwa na uchakavu. Vipo viwanda viwili, vitatu vya wawekezaji lakini havikidhi matakwa ya kupeleka nyama kwenye nchi hizo. Lakini kiwanda hiki cha Kizota kinahitaji bilioni mbili kuweza kukarabatiwa. Mimi huu ni mwaka wa tatu naongea na Serikali, hadi naona huruma kama ningekuwa na bilioni mbili ningeweza kutoa mimi mwenyewe kukarabati pale. Sasa miaka mitatu *consecutively* bilioni mbili hatuwezi kukarabati pale

Mheshimiwa Mwenyekiti, na tatizo lililopo ni kwamba mimi nimewahi kufanya biashara ya nyama; hakuna sehemu ambayo inategemewa kama *central zone*. Na viwanda vingine siwezi kusema ambavyo vya watu binafsi, ukianza kupeleka kwake kuuza baadaye anachukua lile soko. Kwa hiyo wafanyabiashara wetu wanapata shida vilevile hatupati faida ya mifugo. Mheshimiwa Waziri wa Fedha nakuomba sana bilioni mbili tuweze kukarabati kiwanda kile, nakuomba sana sana sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ni kuhusu wakandarasi wetu katika nchi yetu. Naishukuru sana Serikali imetoa kipaumbele kikubwa kwa wakandarasi nchini. Shida iliyoko ni kwamba wanachelewa kulipwa malipo yao, jambo hili Serikali iliangalie.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ni kwamba, duniani kote mashirika ya bima *(insurance)* ndio yanayobeba riski katika biashara. Sasa siku hizi wakandarasi wetu wakienda kuchukua bima kwenye mashirika ya bima wanaambiwa watoe *collateral.* Sasa kwenye benki naambiwa nitoe *collateral* na kwenye shirika la bima nako naambiwa nitoe *collateral;* sasa kazi ya bima wanasema ni *risk aging.* Sasa bima nayo inataka nipeleke *collateral.* Na tunakoelekea kuna siku tutaona bima inatangaza kuuza nyumba ya mtu fulani ambacho duniani kote hicho hakipo. Sasa jambo hili kwetu unaambiwa kwamba lete *collateral* ili uweze kupata bima. Sasa *risk* anayoichukua mtu wa bima iko wapi? jambo hili naomba tuliangalie sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine tuna ushindani wa makampuni ya wakandarasi kutoka nje ya nchi. Wenzetu wanapewa mazingira mazuri, wana benki zao, lakini vilevile wana *risk company* zao ambazo ukilinganisha na kiasi ambacho tunawatoza wakandarasi wetu ni tofauti kubwa sana. Kwa maana hiyo unataka mimi nilyefungwa miguu wote tukimbie mita 100 ilhali mwenzangu hajafungwa miguu. Jambo hili kama tunataka kuinua wakandarasi wetu ni makusudi kabisa tufanye hivyo na kufanya hivyo kwamba fedha yetu itabaki hapa. Mheshimiwa Waziri naomba jambo hili tuliangalie.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine, kazi ya Serikali duniani kote ni kuhudumia wananchi wake, iwe katika eneo la afya na katika maeneo mengine. Tuna tatizo. Wapo wahisani wanatusaidia katika maeneo ya afya na katika haswa suala zima la maji…

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Malizia Mheshimiwa sekunde 30 muda wako umeisha.

**MHE. KENNETH E. NOLLO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka nimalizie; ni kwamba wahisani hawa wanavyoleta vifaa vya kuja kuleta miundombinu ya maji wanatozwa fedha kwa kodi na jambo hili linawavunja moyo. Kwangu nina mwisani ambaye ameleta takriban bilioni mbili ametoa kodi kama milioni 600, fedha ambayo ingeweza kutumika kujenga mradi mwingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikushukuru lakini nataka niseme kwamba Serikali iangalie namna ya kuweza kuondoa kodi kwa wahisani wanaoweza kutusaidia katika maeneo ya huduma za wananchi. Nakushukuru sana, ahsante sana.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana, Mheshimiwa Selemani Jumanne Zedi atafatiwa na Mheshimiwa Simon Songe Lesengekile, Mheshimiwa Luhaga Joseph Mpina ajiandae.

**MHE. SELEMANI J. ZEDI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi hii ili na mimi niweze kuchangia Bajeti Kuu ya

Serikali. Awali ya yote kwanza nitumie fursa hii kwa niaba ya wananchi wa Jimbo langu la Bukene. Nimshukuru kwa dhati Mheshimiwa Rais wa Awamu ya Sita Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa fedha nyingi za maendeleo ambazo zinaletwa kwenye Jimbo letu la Bukene ukilinganisha na kipindi kingine chochote kile.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitazungumzia mambo kadhaa, lakini la kwanza nitaanza na Hifadhi ya Taifa ya Chakula. Nimeona kwenye taarifa ya Mheshimiwa Waziri, ambalo ni jambo jema, kwamba Serikali itaendelea kutenga fedha kununua chakula kwa ajili ya Hifadhi ya Taifa ya Chakula, na makadirio mwaka huu ni kununua tani 400,000 hadi 500,000.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi ushauri wangu ni kwamba tani hizi hazitoshi na kama kuna uwezekano basi fedha zitafutwe ili angalau, najua hatuwezi kuwa na fedha za kutosha kununua tani nyingi kwa wakati mmoja lakini angalau hata tufike tani 700,000 kwa mwaka huu itapendeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, umuhimu wa hifadhi ya chakula unajulikana, hasa pale ambako hifadhi hii ya chakula inatumika ku-*stabilize price* kupunguza makali ya bei pale ambapo kunakuwa na uhaba mkubwa wa chakula. Hapa juzi juzi sisi tumepita kipindi kigumu sana, pale Jimbo langu la Bukene kuna wakati debe la mahindi lilifika mpaka 23,000. Lakini nipongeze Serikali kupitia Wizara ya Kilimo, niliomba Serikali na walileta mahindi, kwa maana ya Hifadhi ya Taifa ya Chakula na tukapunguza bei ya mahindi kutoka debe 23,000 mpaka 14,000 ambayo ikasaidia kuwavusha wananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitoe wito kwa Hifadhi ya Taifa ya Chakula, mara zote imekuwa ikitumia pale Bukene kama kituo cha kununua na kwa sababu kuna ma-*godown* makubwa yanayomilikiwa na Chama cha Ushirika cha Igembensabo. Kwa hiyo Hifadhi ya Taifa ya Chakula tunawakaribisha pale waje wakodi hayo ma-*godown* kutoka Chama cha Ushirika cha Igembensabo waweze kununua mahindi na kuhifadhi pale, yatatusaidia sana kwa sababu mwaka huu pia siyo mzuri sana

kihivyo. Kwa hiyo tunahitaji kuwa na hifadhi ya chakula kwa ajili ya usalama wa chakula. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ambalo napenda kuzungumzia ni kwamba ukiangalia ukurasa wa 147 wa Hotuba ya Mheshimiwa Waziri wa Fedha kwenye hatua za kikodi ambazo Serikali inapendekeza. Waziri wa Fedha amependekeza mojawapo ya hatua za kikodi ni kupunguza ushuru wa forodha kwa mafuta ya kula yanayotoka nje ya nchi kutoka asilimia 35 mpaka asilimia 25. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ushauri wangu ni kwamba, hatua hii ya kikodi ya kupunguza ushuru wa mafuta yanayotoka nje ya nchi ita-*discourage*, itavunja moyo wakulima wetu wa ndani hasa kwenye maeneo ya mazao ambayo yanazalisha mafuta ya kula. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumekuwa tukitumia jitihada kubwa sana mwaka uliopita kuhamasisha wakulima wetu walime alizeti kwa ajili ya kuzalisha mafuta ya kula ili kupunguza upungufu wa mafuta ya kula. Tunajua tuna *gap* kwamba mafuta ya kula tunayozalisha hayatoshi kwa matumizi yetu na kutokana na hilo kumekuwa na mkakati wa makusudi wa kuhamasisha kilimo cha mazao mbalimbali yanayozalisha mafuta ikiwemo alizeti. Sasa pendekezo hili la Serikali la kupunguza kodi, ushuru wa forodha kwa mafuta ya kula yanayotoka nje, litafanya mafuta hayo ya kula sasa ya kutoka nje yawe bei ndogo/bei nafuu na mafuta yetu ya alizeti yatakuwa ya bei kubwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa hili jambo litafanya kwanza wananchi ambao tunawahimiza walime alizeti watavunjika moyo, lakini tumehamasisha sana viwanda vidogo vidogo vya kusindika mafuta ya alizeti na vyenyewe vitavunjika moyo na hatimaye vitakufa. Kwa hiyo ushauri wangu, Mheshimiwa Waziri wa Fedha pendekezo hili la kushusha ushuru wa forodha tubakie pale pale badala ya kushusha kutoka thelathini na tano mpaka asilimia ishirini na tano tubakie na asilimia thelathini na tano hiyo hiyo ili kulinda viwanda vya ndani vya kusindika mafuta ya alizeti na wakulima wetu wadogo wadogo waweze kuendelea kulima alizeti. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine, naunga mkono ongezeko la bajeti kwenye Wizara ya Kilimo. Sisi ambao tunatoka majimbo ya vijijini asilimia kubwa wananchi wetu shughuli yao kubwa ni kilimo. Tunataka wananchi wetu waendelee kupata mbolea ya ruzuku, lakini tunataka tuendelee kuona skimu za umwagiliaji zikiendelea kujengwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nichukue fursa hii na naunga mkono bajeti kwa sababu nahitaji fedha kwenye skimu yangu kubwa ya umwagiliaji. Serikali imenipa skimu kubwa sana hekta 4,000, yenye thamani ya zaidi ya bilioni 40 kwenye Kata ya Sigili pale kijiji Lyamalagwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na kuendelea na skimu kubwa niishauri Serikali isiyaache kabisa mabwawa madogo madogo au skimu ndogo ndogo ambazo zimekuwepo kwa muda na ambazo sasa hivi zimejaa mchanga na hazifanyi kazi vizuri. Kwa mfano, kwangu pale kuna Bwawa la Ikindwa, Bwawa la Malolo, Bwawa la Ng'indo, Bwawa la Chamipulu maeneo ya Mambali kule ambako kuna mabwawa madogo madogo ambayo zamani tulikuwa tunayatumia sana kwa umwagiliaji, lakini muda umekuwa mrefu yamejaa mchanga na sasa hivi hayafanyi kwa ufanisi tunao utarajia. Kwa hiyo pamoja na kujikita kwenye skimu kubwa za umwagiliaji, lakini tusisahau hizi ndogo ndogo ikiwemo na Skimu ya Kamahalanga kwa maana ya kuzifufua na zifanye kazi kadri inavyokusudiwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono bajeti hii kwa sababu bado nahitaji fedha kwa ajili ya kuendelea kuboresha barabara za vijijini. Kazi kubwa sana imefanyika ukilinganisha na hapo nyuma. Barabara zetu za vijijini, *TARURA* wamefanya kazi kubwa sana, wamepasua maeneo ambayo hata hayakuwa na barabara kabisa, lakini kwa sababu hali haikuwa nzuri kazi ya kupasua barabara na kuimarisha barabara za vijijini bado inahitajika. Kwa hiyo, naunga mkono bajeti hii. Kwa sababu inaendelea kupeleka fedha kwa ajili ya eneo la uimarishaji wa barabara vijijini na huko vijijini ndiko uzalishaji uliko. Unaposema barabara za vijijini maana yake ni kwamba bei ya mazao kwa wananchi wa maeneo ya vijijini itaimarika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono bajeti hii kwa sababu inaendelea kupeleka fedha kwenye Miradi ya Maji, kazi kubwa sana imefanyika pale kwangu sasa hivi kuna kazi kubwa sana ya kuyatoa maji ya Ziwa Victoria, Nzega Mjini kuyapeleka Bukene, vijiji ishirini karibu 21 vinakwenda kufaidika…

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Zedi.

**MHE. SELEMANI J. ZEDI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, naunga mkono bajeti hii kwa sababu bado nahitaji fedha zipelekwe ili maji yafike kwenye vijiji vyote katika Jimbo la Bukene.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana na naunga mkono bajeti. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Mheshimiwa Simon Songe Lusengekile atafuatia na Mheshimiwa Luhaga Joelson Mpina na Mheshimiwa Aida Joseph Khenani ajiandae.

**MHE. SIMON S. LUSENGEKILE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nikushukuru kwa kunipa nafasi nami nichangie Bajeti ya Serikali kwa mwaka wa fedha 2023/2024. Nianze kwa kumpongeza sana Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa namna ya pekee sana alivyoendelea kushusha fedha kwenye majimbo yetu, lakini pia kuendeleza miradi mingi ya kimkakati ambayo imekuwa na bajeti kubwa lakini tumeona haijaweza kusimama. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimpongeze sana pia Mheshimiwa Waziri kwa kazi kubwa anazofanya katika Wizara ya Fedha pamoja na Naibu Waziri kwa kazi wanazofanya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mambo machache ambayo nataka kuchangia leo; jambo la kwanza nataka kumpongeza sana Mheshimiwa Rais kwa kuondoa ada kwenye Vyuo vya Elimu ya Kati. Hili jambo limepigiwa kelele muda mrefu sana, lakini leo sasa kwa bajeti hii wamekuja na muafaka wa wananchi wengi ambao walikuwa wakipiga kelele eneo hili. Tuwapongeze kwa

sababu wamekuja na *source* ya kutafuta fedha kwa namna ya pekee ambavyo sasa wanaenda kuyakabili haya ambayo wameyaleta kwenye bajeti hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimeona eneo ambalo wamekuja nalo katika mwaka huu wa fedha unaofuata kwa ajili ya bajeti ya mwaka unaofuata, wamekuja na kuongeza shilingi mia kwenye mafuta. Jambo hili ni jambo zuri na tuna imani kabisa kwamba sasa tunaenda kuona matokeo na shilingi mia itakavyoongezwa kwenye mafuta. Kwa mfano, Busega tuna barabara inayotoka pale Nyashimo kuelekea Dutwa kwa Mheshimiwa Kundo kule. Tunaomba hii barabara itengenezwe kupitia fedha hizi ambazo tumeziweka ili wananchi wa Jimbo la Busega waone matokeo ya shilingi mia kwenye mafuta na barabara hii ni barabara muhimu sana kwenye uchumi wa wilaya hizi mbili kwa maana ya Wilaya ya Bariadi pamoja na Wilaya ya Busega. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ambalo nataka kuzungumza, sijui kama wameishafanya *research* ya kutosha kwa nini watu wanakwepa kutoa risiti na kwa nini watu hawadai risiti? Jambo hili ni jambo la kutiliwa maanani sana. Tuendelee kutoa elimu kwa walipa kodi, tuendelee kutoa elimu kwa wafanyabiashara ili waendelea kutoa risiti na hawa wananchi ambao wananunua vifaa na wenyewe waendelee kuomba risiti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hapa nimekuwa nikifikiria, sijui kama mmeishafanya *cost benefit analysis* kwamba kiasi kinachopotea kwa kutokutoa risiti kwa maana ya mwananchi kutokudai risiti kile kiasi kinachopotea ukilinganisha na kiasi ambacho tunaweza kumpa mtu anapodai risiti kama *token* kwa yeye kudai risiti. Nilikuwa najaribu kufikiria, wanaweza kuunganisha mfumo wa risiti za *EFD* wakaunganisha na namba za simu za wananchi kwa sababu kila mwananchi ana namba ya simu, anapoenda kununua anataja namba yake ya simu, halafu kunakuwa na mfumo *TRA* na mwananchi anapokuwa amenunua na kupata risiti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ile risiti anapokuwa ameipata kwa mwezi mzima wanajua kabisa kwamba namba hii ya simu imepewa risiti kadhaa zenye thamani kadhaa wanam-*credit*

*bonus* kwenye simu yake. Kwa sababu ameomba risiti hili jambo linaweza likawa zuri, hili jambo linaweza likawa na tija kwa mwananchi kuomba risiti. Kwa sababu mwananchi akiomba risiti ndipo atakuwa amechangia mapato katika nchi yake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niwaambie wananchi wa Tanzania kutokuomba risiti siyo kwamba wewe ndiyo unayenufaika, ananufaika yule muuzaji, kwa sababu ile kodi umemwachia, ile kodi anakula yule muuzaji kwa sababu hataipeleka *TRA,* kwa sababu hakuikatia risiti. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wanaweza kufanya hata mambo mengine kwamba, ile pesa wanaweza waka-*credit* kwenye kadi yake ya bima, wanaweza waka-*credit* kwa mwananchi ambaye hana, hapati mshahara kwamba anakatwa bima kupitia mshahara wake wakam-*credit* kwenye simu yake ikatumika kulipa matibabu yake. Hii itamwongeza mwananchi kujua kwamba ana haki ya kuomba risiti lakini mwananchi huyu huyu atajua kwamba nikiomba risiti mwisho wa mwezi nitapata *credit* ya manunuzi ambayo nimefanya. *(Makofi)*

Mhesjhimiwa Mwenyekiti, kwa mfano, mtu amefanya manunuzi ya shilingi milioni tatu, mwisho wa mwezi akapata *credit* ya shilingi elfu hamsini, anajua kabisa kwamba ninapoomba risiti mwisho wa mwezi nitapata *credit* kwenye simu yangu ya shilingi elfu hamsini. Naamini mapato ambayo tunayapoteza kwa wananchi kutokudai risiti ni makubwa kuliko mapato ambayo tutatumia kumpa mwananchi kama *bonus* kwa yule atakayekuwa ameomba risiti. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niiombe sasa Wizara ikae itafakari ione kama inafaa, basi tuwe na mfumo wa makampuni ya simu, mfumo *TRA* na mfumo wa hizi risiti tunazotoa ili ziweze kuwa na *credit* kwa mtu anapokuwa amenunua apate *credit* mwisho wa mwezi ili aone thamani ya kuomba risiti. Kwa sababu sasa hivi muda mwingine hawaoni thamani ya kuomba risiti ameenda kwa mfanyabiashara anaambiwa hii bidhaa nitakuuzia laki tisa, lakini bila risiti nitakuuzia shilingi laki nane na sabini ana-*opt* kutokuchukua risiti, lakini akijua kwamba nimefanya manunuzi ya kiasi fulani na mwisho mwezi nipata *credit* kutoa kwenye Serikali

yangu, naamini kila mwananchi sasa atakuwa na morali ya kuomba risiti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa nasoma Ripoti ya *CAG* majuzi nikaona hata Serikalini. Serikali Kuu hawakuomba risiti yenye thamani ya bilioni 15, Mashirika ya Umma hawakuomba risiti za *EFD* milioni mia tano hamsini na siti, Serikali za Mitaa bilioni 10.08, jumla bilioni 25 hawakuomba risiti na ni watumishi wa Serikali. Hawa hawatufai, ni wahujumu uchumi kama wahujumu uchumi wengine, ni lazima sasa tuanze na Serikalini na wao wawe sehemu mojawapo ya kuhakikisha kwamba wanaomba risiti za *EFD* ili Serikali yetu ipate kodi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimeona kwenye Hotuba ya Mheshimiwa Waziri ameeleza sasa ameongeza wigo wa usajili wa *VAT* kutoka *turn over* ya milioni mia moja kwa mwaka hadi *turn over* ya milioni mia mbili. Hili ni jambo zuri. lakini sidhani kama wamefanya utafiti mzuri wakaona kwamba *turnover* kuwa ndogo litaleta tatizo kubwa sidhani, tatizo kubwa ni wafanyabiashara kukwepa kodi. Kwa sababu duka A yeye hajasajiliwa *VAT*, duka B amesajiliwa *VAT,* mauzo huyu *item* ile ile anauza shilingi elfu mbili na kwa sababu hajasajiliwa ile *VAT* anauza elfu mbili, aliyesajiliwa na *VAT* inabidi aongeze asilimia kumi na nane, atauza elfu mbili mia tatu sitini, lazima huyu atauza zaidi kuliko huyu, nini kinatakiwa kufanyika hapo? Hapa jambo siyo kuongeza tu…

**MHE. HUSNA J. SEKIBOKO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Taarifa.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Sekiboko, taarifa.

**TAARIFA**

**MHE. HUSNA J. SEKIBOKO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Simon ameweka mchango mzuri sana, lakini nimpe taarifa kidogo kwamba kuongeza wigo wa *VAT* kunam-*comfort* mfanyabiashara kutoa risiti ya *EFD* bila kuogopa kufikia ukomo wa milioni mia kwa mwaka. Jambo ambalo litaongeza mapato zaidi kwa Serikali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Simon, taarifa hiyo unaipokea?

**MHE. SIMON S. LUSENGEKILE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naipokea, lakini sidhani kama ni tija sana, ninachotafuta hapa, natafuta *fairness* ya wafanyabiashara. Kwa sababu *turn over* ya milioni 180 haina tofauti kubwa na *turn over* ya milioni 210. Huyu mwenye *turn over* ya milioni 210 anakuwa amesajiliwa na huyu mwenye *turn over* ya milioni 190 yeye hajasajiliwa, lakini unakuta wanauza *item* ile ile. Huyu anauza simu hii hii na huyu anauza simu hii hii, huyu lazima auze bei ndogo na huyu lazima auze bei kubwa sababu ana *VAT*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hapa kinachotafutwa ni kuwasababisha hawa wafanyabiashara kila mtu ajue kwamba kuna *fair* kwenye kodi. Nataka kumshauri Mheshimiwa Waziri, hapa ili kila mtu awe na *fairness* katika kulipa kodi wasajiliwe watu na *VAT* haijalishi *turn over* ni milioni 50 ili kila mtu sasa ajue kabisa kwamba hapa bei ya simu ni shilingi 200,000 na hapa bei ya simu ni shilingi 200,000, hakuna sababu ya kukwepa kutoa risiti kwa sababu wote mnauza bei sawa. Huyu anakwepa kutoa risiti kwa sababu anajua akitoa risiti itabidi aongeze asilimia 18 na mteja atamkimbia, ataenda kwa mtu ambaye hajasajiliwa na *VAT* kwa sababu anajua yeye hatachajiwa ile asilimia 18. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa ili kuwe na *fairness* naishauri Wizara itafakari na ifanye upembuzi yakinifu ikiona inafaa wasajiliwe watu wengi *regardless of the turnover* ili watu wengi waone kabisa kwamba *there is fair* katika biashara na waache kukwepa kodi. Ninachozungumzia hapa ni kuacha kukwepa kodi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimeona umewasha *microphone*. Naomba niunge mkono hoja, ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Mheshimiwa Luhaga Joelson Mpina, atafuatiwa na Mheshimiwa Aida Joseph Khenani na Mheshimiwa Jasson Samson Rweikiza ajiandae.

**MHE. LUHAGA J. MPINA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana kwa nafasi uliyonipa. Niipongeze sana Wizara ya Fedha,

Waziri wa Fedha na timu yake yote kwa namna ambavyo wametuletea taarifa muhimu kutuwezesha kujadili hotuba hii, lakini pia Kamati yako, Kamati ya Bajeti ambayo pia imetupa taarifa muhimu sana na ofisi zingine wezeshi kama *NBS* pamoja na *CAG*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumefanya vizuri tunaisoma taarifa na hatua mbalimbali ya utekelezaji wa miradi yetu tumetekeleza vizuri. Tunaona sasa hivi tunaanza na *LNG* ambao tuko kwenye hatua nzuri, lakini utekelezaji wa Mradi wa Bomba la Mafuta ambao tayari mchango wetu tumeshalipa bilioni 354, nusu ya fedha zinazotakiwa, lakini pia Mradi wa *SGR* tuko vizuri na Mradi wa Mwalimu Nyerere tunaendelea vizuri, sasa tuko asilimia 87. Kwa hiyo, ni mambo ambayo ni mazuri na tumepiga hatua. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa labda nianzie mambo ya masuala ya kiujumla. Kwanza, naunga mkono sana pendekezo la Kamati yako ya kuhakikisha kwamba *Finance Bill* inaletwa na kujadiliwa angalau katika kipindi cha mwezi mzima, kuacha ilivyo sasa leo umewekwa mezani ambayo ni siku saba tu itakuja kuamuliwa hapa Bungeni. Kwa hiyo, naunga mkono kabisa kwamba tupate mwezi mzima wa kujadili taarifa ya *Finance Bill*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili katika mambo ya kiujumla, nashauri lile bango kitita waliloshauriana lenye hoja kumi na saba zilizoibuliwa zingine ndani ya Bunge, lakini zingine kwenye Kamati, wangeleta hapa jedwali lile kuona Serikali imejibu nini na wa wamesema nini, badala ya kusema huko huko tu Kamati ya Bajeti walielewana sasa walielewana nini? Sisi tutajua nini hapa Bungeni?

Mheshimiwa Mwenyekiti, la tatu, katika yale maeneo ya kiujumla ni katika hotuba ya Waziri, katika hotuba ya Waziri wa Fedha, ibara nadhani ya 9, anapozungumzia Ibara ya 9 Mheshimiwa Waziri wa Fedha anazungumzia mwaka 2008 ambako Mheshimiwa Rais Samia Suluhu Hassan hakuwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Kwa hiyo, ukiweka ibara ya

namna hiyo kwa maelezo waliyoyaweka pale inakuwa ni kama matumizi mabaya ya jina la Rais.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la nne, katika haya mambo ya kiujumla ni pale ambapo katika Ibara ya 126 ambako Waziri anasema kupiga marufuku ufungaji wa biashara kwa sababu zozote zile. Ukiweka Ibara ya namna hiyo, unaweza kuleta mkanganyiko mkubwa, moja; kwanza mambo haya ni ya kisheria, yanafanyika kisheria, lakini la pili, kuna mambo ambayo yanalazimika biashara ifungwe. Kwa mfano, unakuta kiwanda au unakuta mgodi unatiririsha sumu kwenye makazi ya watu, unatiririsha sumu kwenye vyanzo vya maji, hizi Mamlaka za Usimamizi zifanye nini? *NEMC* wafanye nini katika mazingira ya namna hiyo kama siyo kufunga ili kuhakikisha kwamba wana–*rescue* maisha ya watu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine unaweza kukuta mtu anafanya biashara hana leseni, hana kibali chochote, anauza bidhaa bandia, anauza bidhaa *fake,* unamfanya nini? Kwa hiyo, tukiweka vifungu kama hivyo vinaleta mkanganyiko kwa wasimamizi wa sheria ambao tumetunga sheria sisi wenyewe na kuwaagiza katika maeneo hayo wafanye nini?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo ibara za namna hiyo aidha ziondolewe au Waziri azitolee ufafanuzi na mamlaka hizi zinazohusika na hizi kazi tujue kwamba zinafanya pia kazi nzuri sana ya ulinzi wa biashara. Kwa hiyo tusizikatishe tamaa kwa kuweka mistari mikubwa hivi kwenye hotuba ya Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu ya muda siwezi kuendelea kuzi–*mention,* lakini nadhani zinafanya kazi nzuri na zinahitaji kupongezwa, lakini pale ambapo mtumishi anaonekana ame–*violate* sheria za nchi ashughulikiwe na natamani watu wa namna hiyo atuambie kuwa amewachukulia hatua wangapi, lakini siyo kuzituhumu hizi taasisi za usimamizi na udhibiti ambazo zinafanya kazi nzuri sana hapa nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine la tatu ni ukusanyaji wa mapato. Nataka nizungumzie suala la ukusanyaji wa mapato na namna ambavyo hatujakusanya zaidi ya trilioni 15, kwa

sababu ya usimamizi mbovu wa ukusanyaji wa mapato hapa nchini. Moja, imeripotiwa hapa kufikia Aprili, 2023 hatujakusanya fedha ambazo ziko kwenye malimbikizo ambazo zimeshikiliwa za kikodi zaidi ya trilioni 7.35. Trilioni 7.35 hatujazikusanya. Kesi hizo ziko kwenye mahakama hizi za rufaa za kodi *TRAB* na *TRAT*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa unajiuliza mwaka mzima umeisha tumeshindwaje kuzikusanya fedha hizi? *TRAB* na *TRAT* hizi mamlaka zetu zina changamoto gani kiasi cha kushindwa kukusanya hizi fedha na ukiangalia uwezo wa *TRA* kushinda kesi katika haya mashauri ni asilimia 81, ina maana kwamba kwenye malimbikizo ya trilioni 7.35 tuna uwezo wa kukusnaya trilioni sita. Kwa hiyo, katika kipindi hiki tunaweza kukusanya trilioni sita kupitia hiki chanzo. Lakini tatizo ni nini tunashinda kuyakusanya hapa mapato? Nini kinachotukwaza kufanya hivyo? Tunaingia kwenye mikopo, tunaingia kwenda kuwa-*harass* wananchi wetu kuwawekea kodi ambazo hazina sababu za msingi, mapato yapo hayakusanywi kwa nini?*(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili hapa kwenye suala la ukusanyaji wa mapato ni utakatishaji wa fedha haramu, ufadhili wa ugaidi na ufadhili wa silaha za maangamizi. Taarifa ya *FIU* inaonesha miamala ya fedha taslimu na fedha zilizopitia katika miamala, zaidi ya trilioni 280 kuishia Aprili, 2023. Hivi utawezaje kukusanya kodi katika nchi ambayo ina miamala ya fedha haramu trilioni 280, halafu hauoni mikakati ya kushughulika na hizi fedha, hauoni mikakati iliyowekwa ya *FIU* kushughulika na hizi kesi na katika kipindi hicho kesi zilizosikilizwa au miamala iliyochambuliwa na *FIU* ni miamala 769 tu, kati ya miamala 16,035 iliyochambuliwa ni 769 peke yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo huoni mkakati wowote huwezi ukakusanya fedha, kodi katika eneo hili kwa sababu ukikuta miamala mingi namna hiyo maana yake ni kuna ukwepaji wa kodi uliopitiliza, maana yake kuna *a list financial flow* iliyopitiliza, maana yake kuna utoroshaji wa fedha nyingi nje ya nchi uliopitiliza, kuna *transfer pricing illegal* zinazofanyika zilizopitiliza. Utakusanyaje kodi katika mazingira haya? *FIU* ni kitengo tu mpaka leo, hakuna *mechanism* huioni, *DCI*

anashughulikaje? *PCCB* anashughulikaje? *DPP* anashughulikaje kuhakikisha kwamba hii miamala tunapata fedha?

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika hili eneo tu ni fedha nyingi sana zilizopotea, lakini bado Tanzania iko kwenye *financial action tax force* na nini na mambo mengine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine ni magendo, magendo katika mipaka na katika maeneo ya bandari. Tunazo bandari bubu 693. Tunashindwaje kuwa-*engage* vijana wetu wa JKT tukaweka *fence* kila mahala tukaweza kukusanya fedha nyingi tu katika hili eneo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, muda wangu una changamoto nyingi na mambo ni mengi niende kwenye mikopo, matumizi ya mikopo ya *ECF* na *LTP*. Kamati imetueleza bayana kwamba matumizi haya ya hizi fedha ni mikopo imeingiwa na Serikali. Serikali zaidi ya mikopo hii iliyoko kwenye hili eneo la *ECF* na *LTP* ni trilioni 2.75 na Kamati ya Bajeti inatueleza dhahiri kwamba hapa fedha hizi hazikwenda kwenye matumizi yenye tija, zaidi ya trilioni 2.75. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumekuwa tukiambiwa hapa tunakopa fedha kwa ajili ya miradi ya maendeleo, inaenda kwenye miradi ya maendeleo. Leo Kamati yako ya Bajeti ina-*prove* kwamba fedha nyingi hizi zimekopwa, trilioni mbili zitakopwa na kuelekezwa kwenye maeneo ya matumizi ambayo hayana tija, trilioni 2.75. Fedha hizi tumekuwa tukikopa tunasema tunapeleka kwenye miradi ya maendeleo. Leo deni letu la Taifa limekuwa kwa asilimia 13.9 *it is almost* asilimia 14.9 kutoka mwaka mmoja kwenda mwaka mwingine. Ni mikopo ambayo hatujawahi kukopa kwa kiwango hicho, lakini tumekuwa tukiambiwa fedha zinaenda kwenye miradi ya kimkakati, lakini tumekuwa tukiambiwa kwamba fedha hizo tumekopa kwa sababu tuna miradi mingi ya maendeleo na mpaka sasa hivi tuna hiyo hoja ya Mkaguzi kwamba zaidi ya trilioni 1.285 zimekopwa nje ya kibali cha Bunge hili lilivyoidhinisha kukopa katika mwaka husika wa fedha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa mikopo kama hii ikiendelea kuruhusiwa, Bunge hili likiendelea kuruhusu mambo kama haya yafanyike na mikopo hii ya *ECF* pamoja na *LTP* ambayo hata Bunge hili liliagiza ikajadiliwe kule na nimeona majadiliano mliyoyafanya inaonekana mmeshindana. Liletwe jedwali zima la fedha hizi trilioni 2.75 zinaenda kwenye maeneo gani na Waziri wa Fedha amepata wapi kibali cha kwenda kuidhinisha mikopo ya matumizi ya kawaida wakati msimamo wa nchi fedha zote zinakopwa kwa ajili ya miradi ya maendeleo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo Waziri wa Fedha yeye amepata wapi mamlaka ya kuruhusu fedha ya kwenda ku–*negotiate* mkopo ambao unaenda kwenye matumizi ya kawaida badala ya matumizi ya maendeleo? Lakini fedha nyingine nazungumza *EPC+F*. Hii *EPC+F* ni mfadhili anakuja na hela, anaajiri Wakandarasi yeye, anasimamia mradi yeye, anafanya *design* yeye, ananunua yeye. Mbona hatupewi maelezo ya kina Taifa linapata faida gani? Tutasimamiaje gharama? Tutasimamiaje ubora kwa Wakandarasi ambao hatuwalipi sisi? Lakini pia mikopo hii ni ndani ya mikopo yetu ile tunayokopa hapa nchini au ni mikopo mingine? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Luhaga, muda wako umeisha.

Nashukuru sana ahsante. Mheshimiwa Aida Khenani, atafuatiwa na Mheshimiwa Jasson Rweikiza, Mheshimiwa Lucy Thomas Mayenga ajiandae.

**MHE. AIDA J. KHENANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru na mimi kunipatia nafasi niweze kuchangia ndani ya Bunge lako tukufu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nianze kwa kuwapongeza Mheshimiwa Waziri na Naibu wake, nawapongeza kwa sababu ya usikivu, changamoto zipo kama binadamu lakini mkiendelea kusikiliza naamini hayo mengine ni ya kawaida katika shughuli zetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nianze kwa masikitiko makubwa sana kwamba ni namna gani tumeshindwa kuwekeza kwenye Ziwa Tanganyika. Nitaanza kwenye eneo moja tu. Ukiangalia mipango ya Waziri wa Kilimo ni mipango mizuri sana, leo tunapozungumzia mapinduzi ya uchumi yatakayotokana na kilimo lazima tuachane na kilimo cha mazoea tuende kwenye kilimo cha kisasa, unapozungumzia kilimo cha kisasa lazima uzungumzie umwagiliaji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Waziri wa Kilimo ameonesha ni namna gani anataka kuweka kipaumbele kwenye umwagiliaji. Changamoto inayojitokeza ni fedha. Kwa kuwa, Mawaziri wa kisekta wameshaonesha mipango yao leo tunachotaka ni kushauri Wizara ya Fedha, na jambo hili kama kweli tunategemea kilimo itakuwa ni mbadala wa ajira Tanzania, lazima tuwekeze kwenye kilimo, kwa sababu Waziri ameshaonesha mipango basi Wizara ya Fedha mpeni fedha, ili akija hapa tumlaumu yeye kwa suala la usimamizi. Fedha apewe kisha tuje tuangalie usimamizi wake ukoje. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili, Ziwa Tanganyika tunapakana na nchi tatu. Tunapakana na Congo, Burundi na Rwanda. Ziwa Tanganyika pamoj ana kujenga bandari, bandari Kigoma, bandari Kabwe, bandari Kalema, Kipili na Kasanga, lakini cha ajabu kwamba Serikali tulikwenda kuweka fedha tulikuwa tunataka ku–*achieve* nini? Kama Ziwa Tanganyika halina usafiri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, endapo kama fedha itawekezwa kwenye kilimo, wakulima wale wa eneo la Ziwa Tanganyika hawatalima mpunga mara moja kwa mwaka, watalima zaidi ya mara moja. Wakilima zaidi ya mara moja bandari zipo, kinachotakiwa ni usafiri wapeleke nchi za jirani. Tunakwama wapi? Haya mambo yanasikitisha, yanahuzunisha sana na ndiyo maana anasema siyo kwamba wote tunakataa mikopo ya Serikali, tunakopa kuwekeza kwenye vitu gani? Vina manufaa gani kwa Watanzania? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, endapo kama tumeamua kuwekeza, hivi leo kweli hatujui faida ya kuwekeza kwenye Ziwa

Tanganyika kuweka usafiri, tukateka biashara upande wa Congo, tunasubiri nini kwenye jambo hilo? Miaka mitatu Mheshimiwa Waziri, Waziri wa uchukuzi ameshaonesha nia, miaka mitatu anatenga bajeti kwa ajili ya ujenzi wa meli, miaka mitatu tunasoma tu hapa lakini hakuna fedha inakwenda. Kwa hiyo, changamoto siyo kutenga, changamoto ni kupeleka fedha. Niwaombe Waziri na Naibu wako, kwa kuwa kwenye Serikali kumekuwa na changamoto kubwa, yaani leo kusoma hapa kwamba tumetenga ni jambo moja, kupeleka jambo kubwa zaidi ambalo linahitaji msukumo ambao siyo wa kawaida, baada ya kupeleka kuna changamoto pia ya usimamizi wa huko mlikopeleka, mradi ukamilike kwa wakati lakini usimamiwe kwa ufanisi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, bado Ziwa Tanganyika hilo tunazungumzia suala la maji yaani ni kilio cha siku zote, miaka yote, shida ya maji wakati tuna Ziwa Kuu, Ziwa Tanganyika. Waziri wa Maji amesema anatamani na yeye kwa sababu suluhisho ni maji kutoa Ziwa Tanganyika, Mheshimiwa Waziri hiyo mikopo yako peleka huko sasa. Wakitoa maji Ziwa Tanganyika tunazungumzia sasa kwamba kutakuwa na manufaa kwa wakulima hawa. Hayo maji yatatumika kwenye matumizi ya binadamu, kwenye viwanda pamoja na kilimo. Mpe fedha Waziri wa Maji akamilishe mradi wa maji na sisi tukikaa sasa tuseme kwenye Ziwa Tanganyika tumetumia ipasavyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo ndani ya Ziwa Tanganyika kuna samaki wa mapambo. Wale Samaki wanavyochukuliwa hata wananchi hawajui huko wanakokwenda wanatumiwaje hao samaki, ni kwa sababu hatujawekeza kikamilifu. Lakini shida siyo masikini kwa hiyo lazima tu–*change mindset*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hapo hapo nataka nizungumze changamoto kubwa ya tozo ambazo ni kero kwa Watanzania. Hizi tozo nataka nianze na kwenye simu. Kwenye suala la miamala ya simu nazungumzia Mtanzania wa kawaida kabisa, achana na *data* huyu tu anayefanya miamala ambaye yule mama ameuza mahindi shambani, anataka kumtumia mtoto wake fedha anasoma *UDOM* na yeye anataka mtoto wake asome Chuo Kikuu. Anapotuma na yeye changamoto, mtoto mwenyewe

anayepokea changamoto, yule amefanya biashara gani? Tumeona hapa mmeonesha namna ambavyo mtakwenda kusaidia yule anayetuma asikatwe angalau yule anayepokea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa umesema tutasimamia usajili, tunajua kabisa kwamba huyu ni mwanafunzi huyu siyo mwanafunzi, kwani tulisajili kwa ajili ya nini? si mnajua lakini ile miamala inavyofanyika tunajua kwamba huyu siyo mfanyabiashara. Yale makato mwongozo utolewe na Serikali, kwa sababu hili suala ni kutengeneza gharama kwa mtanzania wa kawaida kabisa ambayo haiana sababu. Na hili jambo tuangalie pia mpaka kwenye *sim–banking*. Hivi akatwe na benki lakini akatwe tena na kampuni ya simu, kwa nini msikae na haya makampuni angalau makato yawe ya aina moja? Kwa nini akatwe mara mbili huyu mtumiaji wa simu? Hata kama mnataka kukusanya lazima tujue tukusanye bila kumuachia alama mbaya huyu mtanzania ambaye tunatamani kesho tena aendelee kutumia simu na aendelee kuona umuhimu wa hiyo miamala. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, jambo lingine ni vizuri Mheshimiwa Waziri na Kamati yako kaeni chini mpitie upya Sheria za Kodi pamoja na kanuni zake zina changamoto nyingi sana. Hakuna sababu ya kugombana na wafanyabiashara, kaeni nao wanafahamu umuhimu wa kodi lakini waone matokeo ya kodi wanazozilipa moja kwa moja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo jingine nataka kuzungumzia hizi gari za abiria. Gari za abiria na wao wamekuwa na changamoto nyingi, hizi gari za abiria wanapokwenda *stand* lazima wasimaishwe. Hivi si zinajulikana *trip* kwamba wanavyoingia kwenye zile *stand* kwa siku wanaingia mara ngapi. Kwa nini isipigwe hesabu kwa mwaka wanaingia siku ngapi gharama yake ni kiasi gani ili wakajumulisha yale mahesabu, kuondoa ususmbufu wa abiria kila wakati kusimamishwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka nizungumzie jambo lingine la kodi za forodha. Unajua inafikia mahali Halmasahuri nao wanatamani kwamba angalau wapate chochote, sasa yale matamanio yao wanatunga Sheria Ndogo ambazo zinaenda

kunyume kabisa na Sheria Mama. Matokeo yake tunaenda kufifisha hayo maeneo ambayo tulitegemea itakuwa ni mwarobaini, kwa hiyo ni vizuri na huko mkaangalia hata kama Halmashauri wanakuwa na kanuni zao, zile Sheria Ndogo ambazo wanakuwa na matamanio ya kukusanya wapitie kwanza Sheria Mama pamoja na kusudio lao la kutaka kukusanya ili wasiondoe hili suala ambalo lipo sasa hivi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni vizuri sana Mheshimiwa Waziri akiwa anakaa mara kwa mara na *cabinet* yake kupitia hizi changamoto ambazo hazina sababu ya kuleta hizi kelele kama ilivyotokea Kariakoo. Ile uliyoiona ni ya Karikaoo lakini ukiangalia nchi nzima kuna changamoto kubwa sana. Changamoto zinatokana na nini inawezekana sheria ikawa haina changamoto kubwa lakini zile kanuni zina changamoto nyingi sana. Pia shida inakuwepo kwenye usimamizi ambapo usimamizi huu uko chini yako lazima na wewe uliangalie Mheshimiwa Waziri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo jingine natamani kuzungumzia suala la sekta ya uzalishaji nimezungumzia upande wa kilimo lakini na upande wa maji. Nimeona hapa kwenye hotuba yako Mheshimiwa Waziri mmetenga fedha kwa ajili ya Katiba mpya. Mmetenga bilioni tano, ni jambo jema nawashukuru mmetenga, lakini kwa sababu Serikali yetu kutenga ni jambo moja na kupeleka fedha ni jambo jingine. Tunaomba fedha hiyo iende.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Katiba mpya tunayoisema leo kuna mambo mengi tunarekebisha hapa ndani lakini kuna mengine ambayo tutarekebisha hii Katiba iliyopo mpaka lini? Hii Katiba ni ya manufaa yetu sisi sote. Hatusemi Katiba hii itaenda kuwasaidia Vyama vya Siasa peke yake, Hapana! Ndiyo maana Katiba tunasema ni ya nchi yetu, imekuwa ya muda mrefu lakini itaendana na mazingira ya sasa. Nikuombe Mheshimiwa Waziri upeleke fedha, mchakato uanze, utakaozingatia utaratibu na maoni watakayoyatoa Watanzania ili yale yatakayopitishwa yaweze kutekelezeka na Watanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la mwisho Waziri wa Maliasili na Utalii changamoto aliyonayo sasa hivi ni kuhusu hawa

Wanyama, yaani ninapoamka asubuhi unasikia habari ya tembo. Leo tu asubuhi ninapokuja hapa Bungeni tembo wamekwenda mpaka kijijini. Mheshimiwa Waziri, tembo si tunawataka na wananchi tunawataka. Peleka fedha zijengwe *fence* kuzuia wale wanyama wakali ili waendelee kubaki na wanufaishe Taifa. Hayo ni maeneo muhimu kama tembo tunawapenda na binadamu tunawapenda. Upeleke fedha za kifuta jasho pamoja na kifuta machozi ili hawa wananchi ambao leo nimezungumza hapa alipokuwa anawasilisha Waziri. Haiwezekani mkulima ambaye amelima ekari zaidi ya tano, heka moja tembo wakila analipwa shilingi 25,000! Ni mambo ya kikoloni, ni mambo ya zamani, hayana maana yoyote tukitoa leo 25,000 huwezi kwenda kununua chochote. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa. Mheshimiwa Jasson Samson Rweikiza, atafuatiwa na Mheshimiwa Lucy Thomas Mayenga, Mheshimiwa Deo Kasenyenda Sanga ajiandae.

**MHE. DKT. JASSON S. RWEIKIZA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi na mimi nichangie katika bajeti hii kuu ya Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote naomba nitumie nafasi hii kumshukuru sana Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wetu kwa kazi kubwa anayoifanya na bajeti hii ni mfano mmoja wa muendelezo wa kazi zake za kuboresha maisha ya Watanzania. Nampongeza sana na kumshukuru.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimshukuru sana Mheshimiwa Mwigulu na wenzake wote kwenye Wizara kwa kutuletea bajeti hii ambayo ni ya viwango. Mwaka jana kwenye bajeti kama hii, Bajeti Kuu ya Serikali nilipata fursa ya kuchangia na nikazungumzia jambo nililoliita makambi ya kilimo ya vijana. Nikasema kwamba ningetamani kabisa kama vijana wangewezeshwa waanze kilimo cha makambi, kilimo kikubwa, wapewe nyenzo, wapewe matrekta, wapewe *power tiller,* wapewe pembejeo kama mbolea na mbegu, madawa na nini. Makambi yajengwe kwa majengo ya muda halafu kilimo kiwe kikubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nashukuru sana kwamba mpango huu umeanza Mheshimiwa Bashe nampongeza sana unaitwa *BBT*. Wameupa jina jingine *BBT (Building a Better Tomorrow),* napongeza sana kwa sababu mpango huu utaenda kuondoa shida ya ajira kwa vijana na kuongeza uchumi kwa sababu wanazalisha mazao mengi watauza ndani na nje ya nchi watapata pesa na kupata utajiri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa hofu yangu ni moja kwamba mpango ulivyokwenda umekuwa mno wa kutumia fedha, kingereza wansema *capital intensive*. Hii sina hakika kama itatusaidia, bahati mbaya tuna watu wengi ambao ni wezi. Wanakaa wameangalia pesa ilipo wadokoe. Sasa ndiyo maana mimi nikapendekeza kwamba, tungefanya utaratibu ule wa *labor intensive,* vijana wanapelekwa makambini, wanajengewa makambi yale wanapewa hata chakula, mahindi, unga maharage ya kuanzia wanapewa usimamizi, matrekta yale wanazalisha. Pesa kidogo sana lakini zaidi vifaa vile pembejeo na vifaa vingine ili watu wasipate mwanya wa kuiba hizi fedha, kazi ifanyike na matunda yapatikane. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa kwa mtindo uliopo vijana wanakaa kwenye vyuo pale kwangu Bukoba pale Maruku Chuo cha Kilimo, kuna vijana sijui wangapi wametoka sehemu mbalimbali za nchi. Semina ya miezi sijui mingapi, mimi naona ile haina tija. Tija ingekuwa ni kutafuta maeneo mazuri mashamba ambayo tunayo mengi nchi nzima imejaa maeneo yenye rutuba na mvua na mito ipo, kilimo hiki kikasonga mbele kwa sababu kwa kweli kikifanikiwa hiki tutapata tija kubwa sana. Kwa hiyo, tuwe macho sana na matumizi ya fedha kwenye mradi huu au mpango huu badala yake tutumie ile ambayo nilipendekeza, kwamba iwe ni kutumia vijana na nguvu zao na vifaa wapewe badala ya kuwapa fedha ambazo zitatuletea matatizo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, tuwe macho sana na matumizi ya fedha kwenye mradi huu au mpango huu, badala yake tutumie ile ambayo nilipendekeza kwamba, iwe ni kutumia vijana na nguvu zao na vifaa wapewe badala ya kuwapa fedha ambazo zitatuletea matatizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napongeza, hata kwenye Wizara ya Elimu tumeletewa mpango mpya hapa ambao baadaye kidogo, wanasema mwakani ikiwezekana itaanza utaratibu wa masomo ya sekondari ambapo kutakuwa na njia mbili. Kwanza ni masomo ya kawaida, mwanafunzi atasoma mpaka *Form Four,* lakini upande mwingine akipenda mwanafunzi anasoma masomo ya amali; ufundi, kilimo, ufugaji, na masomo mbalimbali. Hii nayo ni njia mojawapo ya kupunguza tatizo la ajira kwa vijana wetu ambao wanamaliza shule, japo itachukua muda mrefu. Kwa hiyo, ule mpango wa kwanza wa *BBT* ukiboreshwa utakuwa ndiyo njia ya kukomboa tatizo hili kubwa la kukosa ajira kwa vijana wetu na kuongeza uchumi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilipendekeza hata Wizara ya Biashara na Viwanda iwe na idara maalum pale Wizarani ya kutafuta masoko kwa mazao ya vijana hawa. Nilisema mazao ya muda kwanza ndiyo waanzenayo. Wakilima mazao kama mahindi, maharage, mtama, alizeti, ambayo yanavunwa haraka sana; miezi mitatu, miezi minne, lakini kuwe na kitengo maalum kwenye Wizara ya Biashara ambacho kitashughulika na kutafuta masoko ya ndani na nje ya nchi kwa ajili ya hawa vijana kwa mazao yao. Ziko nchi nyingi ambazo hawalimi kama kule Uarabuni, Afrika ya Kati hapa, Darfur, Sudani na wapi. Kwa hiyo, mazao haya kile kitengo kisaidie kutafuta masoko ya vina hawa na kuwapelekea mazao na kupata biashara nzuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nizungumzie kwenye Jimbo langu pale Bukoba Vijijini. Nimesema mara kadhaa kuna maeneo ambayo bado yana tatizo la maji. Kwa hiyo, naomba kwenye bajeti hizi haya maeneo yaangaliwe kwa jicho la huruma. Yako maeneo mengi ambayo yana shida kubwa sana ya maji, maeneo kama Umbweya pale kwangu, Kagarama, Vijiji vya Rugaze, Amani, Nsheshe na maeneo mengine kama Kanyangeleko na wapi, maji hayajafika. Kwa hiyo, bajeti ziongezwe kusudi maeneo haya nayo wapate majisafi, salama na ya kutosha kusudi shida ya wananchi katika maeneo haya ipungue.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pale Bukoba kumekuwa na tatizo la muda mrefu la umeme kuzimika mara kwa mara. Kwanza

napongeza umeme unasonga kwenye vijiji na vitongoji, kila siku kuna hatua inapigwa, lakini pamoja na hatua hiyo, umeme huu hauaminiki, unazimika sana. Ukizimika, sasa tija yake haionekani, na vifaa vinaharibika; kama ni taa, zinaungua, kama una *fridge* au nini, vinaungua mara kwa mara na wananchi wanapata shida kubwa sana. Ni hasara kubwa. Kwa hiyo, kazi kubwa inatakiwa ifanyike pale, bajeti iongezwe, kutafutwe njia ya kuondoa tatizo hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, najua kazi inafanyika, lakini kasi iongezeke. Njia sahihi ni kuweka ile gridi badala ya kutumia umeme wa Uganda, tutumie umeme wa Tanzania. Gridi isogezwe ifike mpaka Kagera na Bukoba yote ipate umeme huu wa gridi kusudi tatizo hili la umeme kuzimikazimika liwe ni historia, liishe na wananchi wafaidi umeme huu na hili tatizo la vyombo vyao kuungua liishe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimalizie na jambo moja la mwisho ambalo hivi karibuni Serikali imeruhusu tena mabasi ya abiria kusafiri usiku kucha. Mwaka 1987 nilikuwa nakaa Dodoma hapa nafanya kazi Wizara ya Serikali za Mitaa, lakini familia yangu ilikuwa inaishi Dar es Salaam. Kwa hiyo, nilikuwa nasafiri sana Dar es Salaam – Dodoma. Nilichokiona barabarani ni kitu kibaya sana. Usafiri wa usiku siyo mzuri. Hatujaweza kudhibiti madereva wetu kuwa na nidhamu ya kulala mchana wasafiri usiku. Mchana wanafanya kazi nyingine ya kubangaiza, usiku anaendesha gari. Ajali zilikuwa ni nyingi sana. Watu wanakufa, mabasi yanawachinja barabarani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Malecela akiwa Waziri Mkuu, ndiye aliyefuta mabasi kusafiri usiku mwaka 1994. Sasa leo tumerudisha, sifahamu tumejiandaaje na jambo hili. Tutapata tatizo la kupata ajali nyingi sana barabarani usiku, watu watakufa sana. Tujiangalie kama hatujafikia uwezo wa kuyadhibiti magari haya, tusifanye hivyo. Tuendelee kusafiri mchana na tuache kusafiri usiku. Kama tunaweza, basi tuendeleenalo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana. Naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Nimemwita Mheshimiwa Lucy Thomas Mayenga, atafuatiwa na Mheshimiwa Jenejelly James Ntate na Mheshimiwa Deo Kasenyenda Sanga, ajiandae.

**MHE. LUCY T. MAYENGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipatia nafasi ya mimi kutoa mawazo yangu kwenye bajeti hii. Nampongeza sana Mheshimiwa Waziri kwa bajeti nzuri ambayo kwa kweli, inatupa mwanga wa kile kinachokuja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikiwa nimesimama hapa leo, kwa kweli naomba kwa nafasi ya pekee kabla sijachangia bajeti hii, nipongeze Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya Tanzania ambayo kwa mara ya kwanza wamekamata *cocaine* pamoja na *heroin* kilo 250. Naipongeza mamlaka hii kwa sababu kazi hii inataka uzalendo wa hali ya juu. Nikisema uzalendo, unaweza ukawa mzalendo kwenye mambo mengine, lakini kwenye suala la pesa uko vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kweli, kazi hii inataka uzalendo uki-*base* kwenye kutokupokea rushwa. Ninaipongeza sana mamlaka hii na ninampongeza kwa nafasi ya kipekee Kamishna Mkuu wa Mamlaka hii Bwana Aretas Lyimo. Kwa kweli, ninampongeza sana, wamekamata bangi kavu magunia 978 ambayo ilikuwa tayari kusafirishwa. Wamekamata bangi mbichi magunia 5,495, wamefyeka ekari 1,093. Kwa kweli, taasisi hii ambayo iko chini ya jemadari wetu Mheshimiwa Jenista Joachim Mhagama, kwa usimamizi wenu, tunawapa pongezi nyingi sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wote tunafahamu, hapa tunazungumzia masuala ya bajeti kwa maana ya kile tunachopata pamoja na matumizi, lakini dawa za kulevya, athari zake ni kwamba, zikizidi kwenye nchi, hata uchumi kwanza unaharibika. Hakuna mtu ambaye ataweza kuwekeza kwenye sehemu ambayo uhalifu uko kwa kiwango kikubwa. Wahalifu wengi ni hawa ambao wanavuta bangi na kutumia dawa za kulevya. Kwa hiyo, uhalifu ukiongezeka, hakuna mtu; hata hao wawekezaji ambao leo hii tunawapigia kelele kuwaita, hawataweza kuja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile nijaribu kusema kwa sisi wanawake ambao hasa ndio walezi, *imagine* una mtoto wako ambaye pengine anaweza akawa mmoja au una watoto wako ambao unawapenda. Hakuna mzazi ambaye hampendi mtoto wake. Umemzaa mtoto wako, umemlea vizuri, umemsomesha; wakati unasema kwamba sasa ndiyo umefika wakati wa yeye kuwa angalau akulee wewe, anakuja kuangamia kwenye suala hili la dawa za kulevya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, kwa kweli nampongeza sana Mheshimiwa Rais kwa kufanya uteuzi wa watu makini. Kwa sababu, tumeona baadhi ya maeneo ambayo yalikuwa yamefyekwa haya madawa ya kulevya, kwa maana ya bangi, ni maeneo ambayo bangi ilikuwa inalimwa. Arumeru hapo Arusha kuna viongozi, kuna watu, kuna Wenyeviti. Kwa hiyo, yataka moyo wa kijasiri wewe kutoka pale ulipo kwa maana ya Kamishna Lyimo kutoka pale alipo kwenda kufyeka zile dawa. Ninampongeza sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili, nilikuwa naomba kwanza kuwapa hongera Waheshimiwa Wabunge kwa msimamo mliokuwanao. Wabunge wanawake asanteni sana kwa kura nyingi za kishindo mlizonipa za Ujumbe wa Baraza Kuu la UWT Taifa. Asanteni sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nizungumzie bajeti. Bajeti hii ni *pro-growth* kwa maana ya kwamba huko inakokwenda tunaona kabisa inakwenda kuinua uchumi, lakini zaidi ime-*base* kwenye biashara. Biashara ndiyo hazina kubwa katika maendeleo ya nchi yoyote ile. Serikali haifanyi biashara, lakini uzalishaji wowote ule, hata juzi kwenye taarifa ya Mheshimiwa Waziri wa Fedha wakati anazungumza, alikuwa anazungumzia kuhusu masuala ya biashara na jinsi ilivyo wakulima kule, viwanda, kiwango cha uchakataji wa mazao pamoja na kadhalika. Kwa hiyo, naomba kupongeza sehemu moja. Sehemu kubwa moja ambayo naomba kuipongeza ni suala zima la kuitoa *Capital Gain Tax* kwenye *share transfer* za makampuni yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nchi nyingine kama tunavyojua kwamba soko la hisa Afrika Mashariki liko wazi, hii itasaidia sana

kuweza kukaribisha wawekezaji wengi zaidi waweze kuja kwenye nchi yetu na kuwekeza wakijua kwamba hili suala la *Capital Gain Tax* ni *zero rated.* Kwa sababu, hapo zamani ilikuwa ni asilimia 10, lakini napata mashaka kidogo, huu utaratibu wa kuileta *Finance Bill* dakika za mwisho *(last minutes),* mapendekezo ambayo sisi kama Wabunge tunayabadilisha, ni wakati gani yanapata nafasi ya kuingizwa kule kwenye mabadiliko? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama tunavyojua, bajeti inaanza utekelezaji tarehe 01 Julai. Kama ni hivyo, leo tarehe 20, tunapiga kura tarehe 27, tarehe 28 pengine ni *Finance Bill,* tarehe 30 hapo hapa katikati *Finance Bill* isomwe, mabadiliko yafanyike, Rais asaini. Ni muda mfupi sana. Kwa hiyo, sana sana ambacho naweza kukisema hapa kutokana na *timeframe,* naomba sasa tuwe wazalendo, yale ambayo tunayapendekeza kubadilishwa yaweze kubadilishwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, kutokana na hilo, muda ni mfupi. Baadhi ya nchi za wenzetu wameweza kufanya mabadiliko kwamba, bajeti inasomwa, *Finance Bill* inakuja kusomwa baadaye au wengine wanasoma kabla. Mabadiliko mengi ambayo yanakuja kuwekwa, watu wanaweza kuyaona, lakini hivi hivi unakuwa hujui kipi kitakwenda kusainiwa na kipi kitakwenda kufanyiwa kazi. Kidogo inaleta shida. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nampongeza pia Mheshimiwa Waziri kwa suala zima la kuondoa ada kwa watoto wetu, lakini changamoto kubwa ambayo naiona kwenye nchi yetu na hasa kwenye nchi nyingi za kiafrika ni ongezeko la watu *(population)*. Hivi hatua hizi tunazoendelea kuzifanya, mwisho lini? Au tutazifanya kwa kiwango gani? Kwa sababu idadi ya watu ni kubwa. Yaani wakati hawa wengine wanamaliza, tunachukua *measures* hizi, bado kuna wengine wanazaliwa, bado kuna wengine wako vyuoni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nadhani hatuna budi kukaa chini na kuangalia matumizi ya Serikali, ili fedha ambazo zinapatikana na zinaminywa ziweze kwenda kusaidia kwenye vitu kama hivi. Naomba sana kwa sababu kelele nyingine za watu huko nje, siyo wakati mwingine labda ni kwa sababu ya jambo

fulani, lakini watu wanataka waone fedha zinakwenda kule ambako kunatakiwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ambalo napenda kuchangia ni kuhusu suala zima la bandari. Yapo mengi yamesemwa. Suala hili limekuwa lina mambo mengi sana, lakini mimi nilikuwa naomba kusema hivi, nyakati kama hizi ambazo kila mtu anakuwa na ya kwake ya kusema, hatuna budi sisi kama Wabunge kukaa chini na kutafakari yale ambayo yanasemwa na kuangalia ni kitu gani tunaweza kuki-*push* ili Serikali iweze kufanya kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nasema hivi kwa sababu, mimi kwa imani yangu na ninafahamu kwamba ni imani ya wengi, kwanza kwenye hili suala kuna *mistake* ilitokea *somewhere*. Kuna vitu ambavyo huwa inatakiwa sisi…

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Lucy muda wako umeisha. Malizia mchango wako, nakupa sekunde 30.

**MHE. LUCY T. MAYENGA:** Eeh, amesemaje?

**MBUNGE FULANI:** Muda umeisha. *(Kicheko)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa unga mkono hoja.

**MHE. LUCY T. MAYENGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja. *(Makofi/Kicheko)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Mheshimiwa Janejelly James Ntate, atafuatiwa na Mheshimiwa Deo Kasenyenda Sanga na Mheshimiwa George Joseph Kakunda, ajiandae.

**MHE. JANEJELLY J. NTATE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante, nami nashukuru kwa kupata wasaa huu wa kuweza kuchangia kwenye bajeti ya Serikali. Nianze kwa kumpongeza Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa mambo ambayo anayafanya na maono ambayo ameyaweka mbele ya kugusa

kila sekta. Niendelee kumtia moyo na kumwambia asitoke kwenye ujasiri wake kwa kila anachokiamini kwamba kinaenda kuliendeleza Taifa la Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nampongeza Waziri wa Fedha, Naibu Waziri na Menejimenti nzima ya Wizara ya Fedha kwa jinsi walivyokuja na bajeti ambayo ni nzuri, inayogusa wananchi wa Tanzania. Pia nampongeza sana Waziri wa Fedha, siyo rahisi mtu kupunguza mipaka yako ya utawala, lakini umekubali kubeba maono ya Mheshimiwa Rais, kujipunguzia mipaka ya utawala, kukubali ile Idara ya Mipango basi irudi kuwa Tume ya Mipango. Hongera sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nasema hivyo kwa kufurahi kwa sababu ile idara, ile rasilimali iliyo pale na rasilimali watu ya wafanyakzi waliokuwa pale walikuwa hawatumiki ipasavyo. Ni kama walikuwa *dormant* fulani. Sasa nina hakika wataalamu wataenda kutumika vizuri na kuongeza uchumi wa Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nijikite kwa mliyofanya kwa watumishi wa Tanzania. Nawapongeza sana, pale Ukurasa wa 36 mmeorodhesha vitu mlivyofanya, lakini naomba niende kushauri sehemu ya madeni au malipo ya watumishi ambayo siyo ya kimshahara. Mmesema mmelipa, lakini naomba mwongeze juhudi, hasa kulipa likizo za walimu, watumishi wa afya walio kwenye Halmashauri zetu Tanzania. Nawapongeza kwa sababu sasa mmeamua stahiki za Wakuu wa Idara zilipwe na Serikali kupitia TAMISEMI. Hilo litaleta heshima iliyo bora kwa wale watumishi na kuongeza hadhi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika bajeti iliyopita Mheshimiwa Waziri alisimama hapa tukamshangilia sana. Wakaweka posho ya shilingi 100,000 kwa Watendaji wetu wa Kata, lakini posho hii badala ya kujenga, imeenda kubomoa. Watumishi hawa hawalipwi posho hizi ipasavyo. Wengine wanadai mwaka, wengine wanadai miezi mitano; humu nina *message* nyingi sana, wanasema, Mbunge wetu leo hilo lisemee. Naiomba Serikali, mje na utaratibu mzuri wa kulipa hizo stahili zao ambazo mlikaa hapa zikapotishwa kwenye bajeti ya Serikali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna wastaafu wetu. Kila Mbunge amesimama hapa amesema, kabla mtumishi hajastaafu hupewa barua ya miezi sita kwamba unaenda kustaafu. Sasa kwa nini Serikali msichukue jukumu la kuangalia ni nini kinachodaiwa kwenye mifuko mkakipeleka, kuliko huyu mstaafu sasa? Ameshastaafu na anaanza kuhangaika kufuatilia makato yake, kufuatilia malipo yake kwenye mifuko na wakati ule hana wanaomjua tena Serikalini. Hilo tuliangalie kwa ufasaha zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ni upande wa elimu. Nampongeza sana Mheshimiwa Waziri kwa bajeti aliyokujanayo iliyoangalia mtoto wa mkulima ambapo sasa vyuo vya ufundi wanaenda kusoma bila ada na vyuo vya kati wanaenda kupata mkopo. Hongereni sana. Pia nashukuru kilichofanyika jana, tumeona kwenye mitandao. Tumeruhusu wanafunzi wa Sudani kuja kumalizia masomo Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa unyenyekevu kabisa nitumie nafasi hii kuiomba Wizara ya Elimu na Serikali, tuna watoto wetu ambao walirudi kwa ajili ya vita kutoka Ukraine. Mpaka sasa hivi hatujafanya utaratibu warudi kwenye vyuo. Leo tumeleta hawa wa nje, hivi hawa wa hapa wanajisikiaje? Naiomba sana Serikali, na Waziri wa Elimu waangalie wazazi waliokuwa na watoto Ukraine ambao wengine ni madaktari, walikuwa wanakuja kuisaidia nchi, wengine ni wahandisi, wengine wanasomea taaluma nyingine mbalimbali, basi nao warudishwe kwenye vyuo wakaendelee na masomo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nirudi sasa kwenye utendaji wa Serikali. Nawapongeza sana, kwani kumekuwa na ushirikiano wa kutosha kwa Mawaziri wetu, mmekuwa wanyenyekevu, tunapowafuata kuuliza tunavyotaka kuuliza, tunapata majibu. Wengine hata tukiwapigia simu saa nane usiku mnapokea. Nawaomba mwendelee na ushurikiano wa aina hiyo, mwendelee kumsaidia Mama, mwendelee kuyakuza maono ambayo yeye ameyaweka mbele, bila kuogopa inasema nini, bila kuogopa miluzi inayopigwa, lakini msimame kwa maslahi ya Watanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nirudi tena kwenye afya. Vituo vya afya vimejengwa, lakini nashauri kwamba hakiwezi kuwa kituo cha afya bila wafanyakazi na vitendea kazi. Tunashukuru juhudi za Serikali wameendelea kuajiri, lakini naomba tuwe na mkakati basi kwamba, wakati huu tujikite kuajiri wataalamu wa afya ili vile vituo visije vikageuka magofu. Naomba sana vituo vingi havina wataalam, vituo vingi havina vifaa tiba, basi tuweke nguvu yetu kule tuweze kuendeleza maono ya Mama Samia Suluhu Hassan ambayo ameyaweka mbele maslahi ya Watanzania, ambaye amejitoa usiku kucha akitupigania Watanzania. Basi na sisi tumuunge mkono kwa kuweza kufanya yale maono yake yaonekane.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, naunga hoja mkono. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana.

Waheshimiwa Wabunge, kuna wageni waliopo Bungeni muda huu, tunao wageni wa Waheshimiwa Wabunge; kwanza ni wageni wa Mheshimiwa Jenista Mhagama, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, Sera, Bunge na Uratibu ambao ni wanachama 15 kutoka Chama cha Menejimenti ya Kumbukumbu na Nyaraka Tanzania wakiongozwa na Mwenyekiti wao, ahsante sana, karibuni sana. *(Makofi)*

Wageni watano wa Mheshimiwa Maryprisca Mahundi, Naibu Waziri wa Maji ambayo ni familia yake, wakiongozwa na baba yake mlezi, Ndugu Michael Ukwaya, karibuni sana. *(Makofi)*

Mgeni wa Mheshimiwa Dkt. Angeline Mabula, Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi ambaye ni mtoto wake kutoka Jijini Dar es Salaam, ahsante na karibu sana. *(Makofi)*

Wageni 47 wa Mheshimiwa Anthony Mavunde, Naibu Waziri wa Kilimo ambao ni walimu na wanafunzi wa Shule ya Msingi Amani ya Jijini Dodoma, karibuni sana. *(Makofi)*

Wageni 11 wa Mheshimiwa Kavejuru Felix ambao ni makada wa Chama cha Mapinduzi kutoka mikoa mbalimbali, karibuni sana. *(Makofi)*

Wageni 42 wa Mheshimiwa Dkt. Pius Chaya ambao ni wachungaji wa Dayosisi ya *Rift Valley* na wake zao kutoka Manyoni, Mkoa wa Singida, karibuni sana. *(Makofi)*

Wageni 28 wa Mheshimiwa Dkt. Ritta Kabati ambao ni Kwaya ya Mtakatifu Bikira Maria Afya ya Magonjwa kutoka Ilole – Kilolo, Mkoa wa Iringa, karibuni sana. *(Makofi)*

Wageni wanne wa Mheshimiwa Nicodemas Maganga kutoka Mbogwe, Mkoa wa Geita, ahsante na karibuni sana. *(Makofi)*

Wageni watatu wa Mheshimiwa Munira Mustapha Khatib kutoka Kusini Pemba, karibuni sana. *(Makofi)*

Wageni wangu 12 kutoka Babati Vijijini Mkoa wa Manyara ambao ni wanafunzi kutoka Chuo cha Elimu ya Biashara *(CBE)*; ahsante na karibuni sana. *(Makofi)*

Wageni 27 wa Mheshimiwa Emmanuel Cherehani ambao ni walimu kutoka Halmashauri ya Ushetu, wakiongozwa na Katibu wao, Ndugu Julius Lugobi, karibuni sana. *(Makofi)*

Wageni 33 wa Mheshimiwa Rashid Shangazi ambao ni waratibu wa vipindi vya *Mbunge Live* kutoka Jijini Dar es Salaam, wakiongozwa na Ndugu Aidan Eyakuze ambaye ni Mkurugenzi wa TWAWEZA, ahsante na karibuni sana. *(Makofi)*

Wageni 99 wa Mheshimiwa Anna Lupembe ambao ni Wachungaji na Wanamaombi kutoka Jijini Dodoma, karibuni sana. *(Makofi)*

Wageni 32 wa Mheshimiwa Dkt. Ritta Kabati ambayo ni Kwaya ya Uamsho kutoka Kanisa la Anglikana Veyula, ahsante na karibuni sana. *(Makofi)*

Ahsante. Nilimwita Mheshimiwa Deo Kasenyenda Sanga, atafuatiwa na Mheshimiwa Joseph George Kakunda, Mheshimiwa Josephat Sinkamba Kandege ajiandae.

**MHE. DEO K. SANGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi na mimi niweze kuchangia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nianze kwa kuishukuru sana Serikali ya Awamu ya Sita, inayoongozwa na Dkt. Samia Suluhu Hassan, kwa bajeti nzuri sana iliyolenga kuwakomboa Watanzania yenye mahela mengi, yenye ma-bi na ma-bi na ma-tri. Kwa hiyo tunampongeza sana Rais wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, tumpongeze Mheshimiwa Waziri, Dkt. Mwigulu, kwa bajeti aliyoiwasilisha nzuri, Mheshimiwa Dkt. Mwigulu, Naibu Waziri na timu yako, pamoja na Katibu Mkuu na wataalamu wako; tunakupongeza sana kwa kazi nzuri ambayo unaifanya ndani ya Wizara hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nina mambo machache ya kuchangia katika bajeti hii. Kwanza nitoe shukrani kwa fidia ambayo tumekuwa tukizungumzia pale Makambako inayohusiana na polisi; tunakushukuru sana kwa kutupa fidia ile, wananchi wale sasa wameweza kufaidika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini ziko fidia mbili ambazo bado, fidia ya kwanza ni watu wa umeme wa upepe; watu hawa wamesumbuka zaidi ya miaka 20, hatimaye hatujui nani mwekezaji anayewekeza, maeneo yao yamezuiliwa kwa muda mrefu. Tunaiomba Serikali kama haiwezekani basi wananchi hawa waweze kuendelea na maeneo yao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, fidia ya pili inahusu Wizara ya Viwanda na Biashara ambayo walishalipa fidia, kuna baadhi ya watu 18 ambao bado uhakiki wao ulikuwa haujakamilika. Tuombe wakakamilishe uhakiki wao ili waweze kulipwa fidia zao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ni mapendekezo au masuala yaliyokuwa yanawahusu wafanyabiashara. Tunaishukuru Serikali kwa bajeti hii imewajibu mengi mazuri. Lakini nizungumzie

mambo mawili; moja ni hili la *VAT* ambalo lilikuwa linapendekezwa za *VAT* kutoka shilingi milioni 100 Serikali imejibu sasa itakwenda milioni 200. Ombi langu; fedha milioni 200 kwa sasa ni ndogo, twende mpaka milioni 300 tutakuwa tumekusanya wafanyabiashara wengi ili waweze kujiunga na suala la *VAT*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili linahusiana na faini; faini ilikuwa shilingi milioni nne na ushee. Tunaishukuru Serikali imekubali kupunguza maombi ya wafanyabiashara ambayo sasa faini yake wameiweka shilingi milioni tatu. Bado idadi kubwa ya wafanyabiashara hawa, zaidi ya asilimia themanini na kitu, hawana elimu; ombi langu, faini hii ya shilingi milioni tatu bado ni kubwa, siyo suluhisho. Tunaomba angalau sasa iwe milioni moja. Ikiwa milioni moja angalau kwa sababu milioni tatu hela hizi ni nyingi sana kwa faini ya mfanyabiashara ambaye ni mlipa kodi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna baadhi ya vitu vinafanyika bila mfanyabiashara kujua kwamba hili amelifanya ni kosa. Kwa sababu kama nilivyosema, wafanyabiashara walio wengi hawana elimu lakini ndiyo idadi kubwa ya wafanyabiashara ambao wako katika nchi yetu. Kwa hiyo, tunaomba bei hii iweze kupunguzwa kutoka *amount* iliyowekwa sasa iende shilingi milioni moja, ikiwezekana ishuke zaidi, kwa sababu nia ya Serikali siyo kukusanya faini, ni kukusanya kwenye uhalisia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la tatu ni wakulima wa zao la ngano; bajeti hapa anaelezea Mheshimiwa Waziri alipokuwa anawasilisha *HS Code* 1001.99.10 na 1001.99.90. Sisi kule Njombe Mheshimiwa Mkuu wa Mkoa Mtaka, amehimiza wananchi juu ya kulima ngano, Wilaya za Wanging'ombe na Ludewa ni wakulima wa ngano wakubwa ambao wameitikia, na kwa sababu Waziri wa Kilimo, Mheshimiwa Bashe, alihimiza sana kwamba ngano sasa inatakiwa ipatikane kupitia nchini Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa ukienda Arusha wenzetu wa Arusha nao wameitikia wanalima ngano; ukienda Manyara vilevile wanalima ngano. Sasa kwa kupunguza kodi ngano

inayotoka nje kutoka 35 kwenda 10 unawafanya hawa wakulima wa ndani sasa waone hauna umuhimu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninadhani hii bei 35,000 ya kutoka nje ibaki palepale ili kusudi hawa watu wa viwanda wanunue ngano inayozalishwa hapa, tutakuwa tumewatendea haki wakulima wetu sana. Kwa hiyo, ninaomba sana kwamba Serikali, Mheshimiwa Dkt. Mwigulu, ulione sana jambo hili. *(Makofi)*

**MHE. FESTO R. SANGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Taarifa.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Deo Sanga, kuna taarifa kutoka kwa Mheshimiwa Festo Sanga.

**TAARIFA**

**MHE. FESTO R. SANGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru. Hiki anachokizungumza mzee wangu, Mheshimiwa Sanga, ni jambo sahihi kabisa kwa sababu Mheshimiwa Rais, mama Dkt. Samia Suluhu Hassan, kwa Wilaya ya Makete tu ametoa ngano bure kwa wakulima iweze kulimwa kwa ajili ya kusambaza viwandani. Kwa hiyo, kitendo cha kushusha kodi kinakwenda kusababisha kwamba wakulima wetu wawe *stranded* kwa maana ngano wanayolima sasa itakwenda kukosa soko. Kwa hiyo, hili lazima Wizara ya Fedha iangalie kwa sababu tayari Mheshimiwa Rais ameshachukua hatua ya kushusha na kusambaza ngano bure kwa wakulima nchini, ikiwemo Makete.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Deo Sanga, unaipokea taarifa hiyo?

**MHE. DEO K. SANGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naipokea kwa mikono miwili kwa sababu nia ya Serikali ni nzuri, kwamba tuhimize watu wetu ngano izalishwe kwa wingi kupitia Nchini Tanzania, na wakulima wameitikia, na sisi kule Njombe kupitia Mkuu wetu wa Mkoa amehimiza jambo hili, na hata Iringa nao wanalima ngano sana sasa, wameitikia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ninaomba kwamba Serikali, Mheshimiwa Dkt. Mwigulu, jambo hili liangalie mara mbili,

na utakapokuja kwenye majumuisho lazima utupe majibu ili wananchi nchini waweze kujua Serikali imechukuaje hatua juu ya jambo hili ambalo wanategemea kuuza ndani ya nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la mwisho; niishukuru Serikali kupitia Waziri mwenye Dhamana ya Viwanda na Biashara, Mheshimiwa Dkt. Ashatu, kwa kuweza kulipa fidia ya Liganga na Mchuchuma kule Njombe; tunaishukuru sana Serikali sisi kule Njombe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ombi letu kwamba sasa fidia imeshalipwa na ni hela nyingi, ombi letu kwamba sasa mradi huu ni lazima Serikali muhakikishe unaanza ambavyo wananchi wa Mkoa wa Njombe na Tanzania kwa ujumla wategemee kwamba Liganga na Mchuchuma sasa inakwenda kuanza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine la mwisho; tumepitisha bajeti *hapa* za kisekta, Wizara mbalimbali; ombi langu kwamba tuhakikishe sasa fedha hizi zinakwenda kwa wakati ili zikaweze kufanya kazi iliyokusudiwa ya maji, barabara, elimu, afya n.k. Kwa hiyo, naomba sana sasa fedha zianze kwenda ili mradi kule wananchi wanategemea sana, na sisi tutakapokwenda kwenye ziara mara baada ya mwisho wa bajeti hii sasa Wabunge nina imani tunakwenda kufanya ziara kwenda kuwaeleza wananchi tulichopitisha hapa fedha za ma-B nama-B na ma-T. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi, ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Mheshimiwa Joseph George Kakunda, atafuatiwa na Mheshimiwa Josephat Sinkamba Kandege, Mheshimiwa Aloyce John Kamamba ajiandae.

**MHE. JOSEPH G. KAKUNDA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa nafasi hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kwa maneno ambayo aliyatamka Mheshimiwa Waziri wakati anawasilisha hotuba yake, alisema; Mheshimiwa Rais wetu, mama yetu Samia Suluhu Hassan,

apewe maua yake. Na mimi narudia hivyo; apewe maua yake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Rais tangu aingie madarakani amefanya maamuzi makubwa yenye manufaa makubwa kwa nchi hii. Kwanza alikuja na kauli inayosema kazi iendelee; maana yake nini, alikuwa anamaanisha kwamba miradi mikubwa ambayo ameirithi kutoka kwa mtangulizi wake ambayo ni ya kimkakati kwa ajili ya maendeleo ya nchi hii; Mradi wa Bwawa la Mwalimu Nyerere, Mradi wa *SGR* na miradi mingine ya aina hiyo, kwamba iendelee kutekelezwa. Ameendelea kuisimamia, inaendelea kutekelezwa. Hakuna mradi hata mmoja ambao umesimama; apewe maua yake kwa kazi hiyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ameongeza jambo moja kubwa vilevile, wakati ule tulikuwa tunatekeleza miradi mingi tu ya huduma za jamii, yeye ameiongezea fedha miradi ya sekta za elimu, afya, barabara vijijini, yote hiyo ameiongezea fedha kwa nia ya maendeleo ya wananchi wa Tanzania; apewe maua yake kwa sababu hizo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, yako mambo ambayo yanazungumzwa sana katika nchi hii, ningependa kutoa ushauri; Watanzania wote hata kama tuna maoni mazuri namna gani tulenge katika kuitunza na kuilinda amani ya nchi yetu, amani ya nchi yetu ni lulu. Ndiyo maana unaona kwamba kuna wanafunzi kutoka Sudan wamekuja kusoma Tanzania kwa sababu nchini kwao imekosekana amani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba sana viongozi wa vyama vya upinzani, viongozi wa dini, kama wana jambo lolote kwa umoja wao wanaweza wakaandaa mkutano wakaomba kukutana na Mheshimiwa Rais, kama kuna ufafanuzi wowote Mheshimiwa Rais hatakataa kuonana nao, ataonana nao, watazungumza na wataelewana ili manufaa ya Taifa letu yaendelee kusonga mbele.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nipongeze sana vipaumbele vya bajeti ya mwaka huu, 2023/2024, vizuri kabisa. Cha kwanza kabisa kuongeza ushiriki wa sekta binafsi kwenye uwekezaji na biashara.

Hili neno uwekezaji limelihesabu katika hotuba ya Mheshimiwa Waziri, amelitaja mara 57, uwekezaji. Maana yake ameonesha msisitizo kwenye kipaumbele hiki. Nampongeza sana Mheshimiwa Waziri na timu yake yote, lakini haya najua amefanya kwa maelekezo ya Mheshimiwa Rais; apewe tena maua yake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kipaumbele kikubwa cha pili; kupanua wigo wa vyanzo vya mapato ili kukusanya mapato mengi zaidi, ikiwemo kutoka kwenye masoko ya fedha ya kimataifa kwa nia moja kwamba tukipata mapato mengi zaidi tuyapeleke kwenye miradi ya kimkakati kwa ajili ya maendeleo ya nchi hii; apewe maua yake Mheshimiwa Rais. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, vipaumbele hivi viwili vinategemeana; ili sekta binafsi iwekeze inategemea sana uwekezaji wa sekta ya Umma. Ili sekta binafsi iwekeze inategemea sana Serikali iwekeze kwenye maeneo ambayo yanatoa huduma kuihudumia sekta binafsi. Nilisema siku ile ya mradi wa bandari nilivyochangia; nilisema kwamba ili sekta binafsi iwekeze inahitaji gharama nafuu za umeme.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ndiyo maana Serikali inaelekeza fedha nyingi zaidi kwenye kulipa kwa ajili ya kuwekeza kwenye Bwawa la Mwalimu Nyerere, lakini kwa ajili ya kuwekeza kwenye gesi, na kwa ajili ya kuwekeza kwenye vyanzo vingine vya umme na nishati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo kule kwenye Bwawa la Mwalimu Nyerere wako Wamisri; kule kwenye *LNG* kuna mataifa mengine tunayoingia nayo mkataba; kule kwenye vyanzo vingine kuna mataifa mengine tunaingia nayo mkataba. Sasa kama kila mtu ataanza kuhoji kwa nini tunaingia mkataba na nchi nyingine, kwa nini tusiboreshe ujuzi wa watu wetu; ni mpaka lini tutaboresha ujuzi wa watu wetu? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunataka twende kwa haraka ndiyo maana tutakutana na mataifa mengine kwa ajili ya kushirikiana nao. Wenzetu wamesha-*advance,* ili watusaidie na sisi tuweze kukimbia badala ya kutembea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunahitaji gharama nafuu za usafiri na usafirishaji, ndiyo maana tunawekeza kwenye *SGR,* tunawekeza kwenye viwanja vya ndege, tunawekeza kwenye barabara za lami na madaraja makubwa, tunawekeza kwenye vivuko, tunawekeza kwenye miradi mingine kama hiyo ya bandari. Tunahitaji kukimbia badala ya kutembea ili tuweze kuwafikia wenzetu ambako wamefikia tunahitaji *linkages. (Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili wafanyabiashara wawekeze kwenye sekta binafsi wanahitaji Serikali iwekeze kwenye uzalishaji wa malighafi. Ndiyo maana hii miradi ambayo inakuja kupitia sekta ya kilimo nayo ni muhimu sana ili waweze kupata malighafi kwenye viwanda, viweze kufanya kazi kwa mwaka mzima ambapo vitatoa ajira kwa vijana wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile Serikali inawekeza kwenye kuzalisha ujuzi. Wafanyakazi wenye ujuzi watapatikana kwenye vyuo vyetu vya kati na vyuo vya ufundi. Hapo napo lazima Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan apewe maua yake kwa uamuzi wake wa kuondoa adha kwenye vyuo vya ufundi, lakini vilevile kuondoa adha kwenye vyuo vya kati. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hatuwezi kuendelea bila kupata nguvu kazi yenye ujuzi. Uwekezaji huo ambao unawekwa na Serikali ni jambo la muhimu sana la kuunga mkono.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nirudi kwenye majimbo yetu. Kwenye majimbo yetu iko miradi muhimu ambayo inaendelea kutekelezwa kwa muda mrefu. Ninaiomba na kuishauri Serikali, ninaomba sana Mheshimiwa Waziri wa Fedha, kule kwenye Baraza la Mawaziri kuna miradi ambayo inaendelea kutekelezwa hapa nchini kwa muda mrefu, naomba ipewe kipaumbele.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano ile barabara namba T8 ambayo inatoka Mwanza – Shinyanga – Nzega – Tabora – Ipole – Rungwa mpaka Mbeya kupitia Chunya, hiyo barabara ikikamilika ni *linkage* kubwa sana katika ku-*supply* vitu mbalimbali kwa ajili ya maendeleo ya nchi hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kipande cha Ipole – Rungwa hakina mkandarasi; kipande cha Rungwa – Itigi hakina mkandarasi; kipande cha Rungwa – Makongorosi hakina mkandarasi. Ni jambo muhimu sana kuweka kipaumbele kwenye barabara hiyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna barabara namba T9 ambayo inatoka Biharamulo inapita Nyakanazi nakwenda Kasulu, ikifika Kanyani mpaka Uvinza haina Mkandarasi na kutoka Uvinza mpaka katikati pale kabla hujafika Mpanda hakuna Mkandarasi; inakwenda mpaka Tunduma, hiyo nayo ni muhimu sana ipate kipaumbele.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna miradi ya maji ambayo nayo haijakamilika kwa muda mrefu. Kule kwangu kuna mradi wa Bwawa la Igumila kwa ajili ya kusambaza maji kwenye kata za Kitunda na Kireli lakini kuna *extension* ya mradi wa maji wa Ziwa Victoria nao bado haujafika kwetu, naomba *speed* ikamilike.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna miradi ya *REA* ambayo inatakiwa ikamilike *by* mwezi Disemba mwaka huu. Nayo Serikali iendelee kuweka kipaumbele ili ikamilike kama ratiba ilivyotangazwa kwa wananchi. Tusicheleweshe kabisa miradi ya umeme ambayo ni muhimu sana kwa maendeleo ya nchi hii. Baada ya hapo kipaumbele kiendelee kuwekwa kwa ajili ya umeme kwenye vitongoji ambao mwaka huu unaanza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la mwisho kwenye sekta ya kilimo; siku ya bajeti ya kilimo nilitaja hapa madeni ambayo wakulima wangu wa Sikonge bado wanadai mpaka leo, kwa muda wa miaka miwili, mitatu. Nilipendekeza siku ile kwamba Serikali illipe hayo madeni halafu yenyewe ndio iendelee kubanana na hizo kampuni. Lakini baadaye nikasikia Mheshimiwa Waziri wa Kilimo ametoa maelekezo kwenye hii Kampuni ya *TCJE* ambayo iko badala ya *Apex* ya ushirika. Kwamba hii kampuni ya *TCJE* walipe hayo madeni kwa kukata kwenye utaratibu wa pembejeo na nini. Mimi namuunga mkono Mheshimiwa Waziri, lakini nilikuomba naomba sasa…

**MHE. EMMANUEL P. CHEREHANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Kakunda kuna taarifa kutoka kwa Mheshimiwa Cherehani.

**TAARIFA**

**MHE. EMMANUEL P. CHEREHANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Nampa taarifa mzungumzaji, naomba tu Mheshimiwa Waziri wa Fedha aondoe kodi kwenye *duty twine, hessian cross* ili kampuni hii ya *TCJE* iweze kupata faida kubwa na iende kumalizia madeni ya wakulima wa Tumbaku ambao hawajalipwa kwenye Mikoa yetu.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Kakunda taarifa unaipokea?

**MHE. JOSEPH G. KAKUNDA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naipokea taarifa na ninamini Mheshimiwa Waziri wa Fedha na Mheshimiwa Waziri wa Kilimo wameisikia hiyo taarifa, na wataifanyia kazi ili wakulima wetu waweze kulipwa madeni ambayo wanadai kwa muda mrefu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya hoja hiyo kwa mara ya mwisho, nampongeza sana Mheshimiwa Waziri wa Fedha kwa jinsi ambavyo ameandaa bajeti vizuri na akawasilisha vizuri. Zile mwembe alizokuwa anatupa hapa vilikuwa ni vionjo ambavyo vimewafanya Watanzania wamwelewe vizuri na waielewe bajeti yote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja, ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Kakunda, ahsante sana. Mheshimiwa Josephat Sinkamba Kandege atafuatiwa na Mheshimiwa Aloyce John Kamamba, Mheshimiwa Vedastus Manyinyi Mathayo ajiandae.

**MHE. JOSEPHAT S. KANDEGE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi na mimi niwe miongoni mwa

wachangiaji wa leo. Naomba kipekee nimpongeze Mheshimiwa Waziri wa Fedha na Mipango pamoja na timu ya wataalam wake; na wewe Mheshimiwa Mwenyekiti ni shuhuda; kwa jinsi ambavyo wamekuwa wasikivu wakisikiliza maoni ya Kamati ya Bajeti lakini pia maoni ambayo yaliletwa na wadau, Mheshimiwa Waziri hongera sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni ukweli usio pingika kwamba sheria ikitungwa Bungeni, pale inapoenda kutekelezwa vizuri mafanikio yake yanakuwa ya kwetu sisi sote. Hivi karibuni imezuka tabia kwa wafanyakazi wa Serikali hasa wa *TRA* pale ambapo wanapokwenda kutekeleza Sheria ambayo sisi tumeitunga vizuri, wanapoenda kufata kanuni katika kutoza kodi likija baya inakuja upande wa Kamati ya Bajeti lakini pia na Bunge kwamba ni Bunge ndilo ambalo limetunga Sheria hii. Si vizuri na inakatisha tamaa, likiwa zuri la kwetu na likiharibika lote liwe la kwetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nichukue nafasi hii kumpongeza kipekee Mheshimiwa Rais kwa kazi nzuri na ubunifu mkubwa ambao ameufanya, kwa kuja na ubunifu mkubwa sana wa kuja na filamu ya *Royal Tour*. Filamu hii inaleta watalii wengi sana na tumeambiwa wataendelea kumiminika kwa kadri siku zinavyokuja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni ukweli usiopingika kwamba sisi kama Taifa, tukilinganisha na majirani zetu tunaupungufu wa mahoteli na vitanda. Lakini katika bajeti ambayo imeenda kusomwa na Mheshimiwa Waziri sijaona hatua za makusudi ambazo zinatakwenda kuchochea ujenzi wa hoteli kwa ajili ya watalii ambao tunatarajia watakuja. Ni vizuri wakati mnaenda kuhitimisha muje na vivutio vya kikodi na visivyo vya kikodi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wewe ni shuhuda, kuna kipindi ambacho tulikutana na benki, inaonekana katika sekta hii pamoja na kuonesha kwamba kuna *appetite* lakini benki haziko tayari kukopesha watu wanaokwenda kuwekeza katika *industry* hii. Ni vizuri Serikali mkajiuliza, kwamba, pamoja na fursa iliyopo ya kwenda kutengeneza fedha kwa nini benki haziko tayari kupeleka kwenye maeneo hayo? Inawezekana ni sheria zetu, sheria za ardhi. Je, mtu anapokuja kutoka nje anapotaka kuleta mtaji

wake, sheria zetu za ardhi zinasemaje? Atakuwa tayari kuwekeza? Kwa hiyo ni vizuri mkalitazama kwa mapana yake ili hao watalii ambao Mheshimiwa Rais amefanya kazi kubwa ya kuwaleta iende kuwa na manufaa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nichangie eneo lingine la pili, kwenye kilimo. Ipo taarifa ambayo na mimi naiunga mkono, Serikali imetangaza kwamba lazima kuwe na *control* kuhakikisha kwamba chakula hakiuzwi kiholela, ni jambo jema. Lakini ni vizuri Serikali mkafanya tathmini; bei ambayo mwananchi wa Kalambo, bei ambayo mwananchi wa Namtumbo alikuwa akiipata kabla ya tangazo hili gunia lilikuwa limefika elfu sabini, leo hii tunavyoongea gunia liko shilingi elfu arobaini, shilingi elfu thelathini na tano. Je, kwa haya yanayofanywa na Serikali yanatoa motisha kwa mwananchi mwaka unaofata kwenda shambani kwenda kulima ilhali anajua kwamba kitu anachoenda kulima hakina maslahi kwake yeye.

**MHE. BONIPHACE M. GETERE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

**MWENYEKITI:**Mheshimiwa Kandege kuna taarifa kutoka kwa Mheshimiwa Boniphace Getere.

**TAARIFA**

**MHE. BONIPHACE M. GETERE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kweli kwa hali halisi ya nchi yetu kuna maeneo bei ya gunia inafika laki na ishirini mpaka laki moja kwa hiyo pale wanapouza elfu arobaini wapeleke Mkoa wa Mara hasa kwenye Jimbo langu.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Kandege taarifa hiyo unaipokea?

**MHE. JOSEPHAT S. KANDEGE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naongelea wananchi wa Jimbo la Kalambo ambao alikuwa anapata gunia kwa shilingi elfu sabini leo ukimwambia apate elfu thelathini hatakuwa *motivated* kulima mwaka mwingine. Kwa hiyo ni vizuri Serikali wakajiuliza na kujibu maswali yafuatayo;Pale ambapo wamesema kwamba mahindi yasipelekwe nje, Je,

wanafedha ya kutosha kununua mahindi katika vijiji vyote? Je, wananunua kwa bei gani?

Mheshimiwa Mwenyekiti, na kwa bahati nzuri Mheshimiwa Waziri alishawahi kusema, ni vizuri ukiyasema uyakumbuke. Ulisema kwamba si kazi ya mwananchi kutunza mahindi kwa ajili ya Serikali. Kwa hiyo lile jambo lilokuwa zuri kwa ajili ya mwananchi naamini bado haijabadilika. Serikali mjipange…

**WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Taarifa.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Kandege kuna taarifa kutoka kwa Mheshimiwa Waziri wa Kilimo.

**TAARIFA**

**WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kumpa taarifa Mkulima Kandege na wakulima wote wa nchi hii. Serikali imezuia kupeleka mazao ya kilimo nje ya nchi kinyume na utaratibu. Anayefuata utaratibu uliowekwa na Serikali atapata *export permit*, ilimradi awe na *business license* awe na *tin, short of that* hatutaruhusu mazao ya kilimo kutoka nje ya nchi kinyume na utaratibu.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Kandege unaipokea Taarifa?

**MHE. JOSEPHAT S. KANDEGE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naipokea taarifa na ni vizuri wananchi mkajua kwamba Serikali haijazuia mahindi kwenda nje na msubiri bei zitapanda muuze katika hali ambayo itakuwa na tija katika kilimo chetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kueleza eneo hilo, na bahati nzuri napata *response* nzuri kutoka Serikalini kwa hiyo wananchi wa Kalambo msubiri msiwe na haraka ya kuuza mahindi, mtauza mahindi katika bei ile ambayo inaleta tija ili na mwakani mrudi kwenda kulima mkijua kwamba kilimo ni tija.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niende eneo jingine la pili. Teknolojia haiongopi na namba haziongopi. Ni ukweli usipingika

kwamba Serikali kwa kutofanya maamuzi kwa wakati wakati mwingine wanajikosesha fedha wao wenyewe. Kuna utaratibu ambao ulikuwa umeanzishwa ambao ulikuwepo tangu zamani juu ya kuwepo kwa bahatinasibu ya Taifa. Jambo hili tangu mchakato wake umeanza ni muda mrefu Serikali inajikosesha mapato. Hebu mtuambie mchakato wa kuianzisha umefikia wapi? Kwa sababu tusipokuwa na bahatinasibu ya Taifa ni kwamba watu wetu wanakwenda kucheza *off show* hakuna chochote ambacho kinapatikana ndani ya Serikali na sisi tungetaka fedha zipatikane ili mwananchi wa Kalamba afaidike na kujengwa kwa madarasa na kupelekwa lami.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pia kama hiyo haitoshi kama ambavyo nimesema namba haziongopi; wakati walipokuja wenzetu wa *Sport Betting* waliiambia Serikali kwamba kwa kushusha kodi kwa mwananchi ambaye ana *win* tafsiri yake itaenda kuongeza watu wanaoshiriki na wananchi watajua kwamba wanapata fedha. Ni ukweli usiopingika kwamba hadi leo tunavyoongea kufika mwezi Mei Serikali imeweza kuvuka malengo kwa asilimia 12, na kufika mwezi Juni hakika inaweza kufika asilimia 20.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo niombe Serikali ni vizuri mkawasikiliza wadau wawape takwimu, kile wanachoahidi kwamba kinaweza kupatikana kikapatikane na Serikali mwe tayari kukubali matokeo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niongelee zao la pamba. Nilimsikia Mbunge anayetoka eneo ambalo pamba inalimwa, lakini ni ukweli usiopingika kwamba sisi kama Taifa tunategemea zao hili kwa ajili ya kuingiza fedha za kigeni. Ni ukweli usiopingika pia kwamba pamoja na kutegemea zao hili haina tija pale ambapo pamba inaenda kuuzwa nje ikiwa haijaongezwa thamani yoyote. Kama Serikali naomba mjiulize na mtoe majibu, kwa nini asilimia 75 ya pamba inakwenda ikiwa pamba ghafi lakini wakati huo tunaambiwa eti kuna viwanda ambavyo vinatengeneza nguo? Tupate majibu, je, nguo hizo ambazo zinatengenezwa ni zile ambazo ni za *standard* ya leo? Je, vinaanzia kuanzia pamba kuchambua na hadi kuja kutoa nguo?

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni vizuri Serikali mkaweka mazingira ya kuhakikisha kwamba Viwanda vinakuwepo vya karne ya 21 ambavyo hakika hata ukienda sehemu ambayo wafanyakazi wanafanya kazi unasema wako katika mazingira yaliyo bora. ni vizuri pia mkatafuta namna ya kuweza kutoa vivutio ambavyo vitasaidia watu waje wajenge viwanda na si kubabaisha kuna viwanda wakati hakuna viwanda kwenye uhalisia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nawapongeza Serikali wameliona hili. Watu wetu walikuwa wanataabika juu ya uingizaji wa vitenge, vinakuja vitenge ambavyo vinakuja Tanzania, vinaenda nje ya nchi halafu vinarudi Tanzania tunakuja kuuziwa tena Tanzania…

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Kandege muda wako umeisha.

**MHE. JOSEPHAT S. KANDEGE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Mheshimiwa Aloyce John Kamamba atafuatiwa na Mheshimiwa Vedastus Manyinyi Mathayo, Mheshimiwa Kunti Yusuph Majala, ajiandae.

**MHE. ALOYCE J. KAMAMBA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi ya kuchangia kwenye hoja iliyo mbele yetu. Kwanza nimpongeze na kumshukuru Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kutuletea miradi mingi katika maeneo mengi sisi wananchi wa Wilaya ya Kakonko, tunamshukuru na kumpongeza sana Mheshimiwa Rais.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini nipongeze Wizara ya Fedha, Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri na Watendaji wote wa Wizara kwa kazi nzuri. Nipongeze kwa bajeti nzuri ambayo inakwenda kuwagusa wananchi wetu wa kawaida hasa kwa kuweza kutoa mkopo kwa wanafunzi katika vyuo mbalimbali hasa vyuo vya kati. Tunaipongeza sana Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jicho sasa linapaswa lipelekwe kwenye vyuo vya kati hasa wale wanaosomea elimu amali ambao wanaweza wakawa ni wale wanaosomea useremala, wanaosomea ushoni, wanaosoma uuguzi na kadhalika; hawa wanasomea kazi. Tunategemea kwamba ndani ya muda mfupi wakikopeshwa watamaliza masomo yao na wataweza kujiajiri na hivi ni rahisi kwao kurudisha fedha ambazo Serikali imewakopesha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nirudi katika eneo la kuchangia kwenye bajeti. Ili bajeti iwe endelevu lazima kuwe na vyanzo mbalimbali kwa ajili ya kui-*support* bajeti hii, na maeneo ambayo yanapaswa kusupotiwa *(to be supported)* ni pamoja na kuongeza vipato ambavyo vinatokana na wananchi wanaoingia na kutoka kwenye mipaka ya nchi yetu. Upo mpaka kama wa Mlongo katika Wilaya ya Kyerwa, upo mpaka wa Mabamba katika Wilaya ya Kibondo, upo mpaka wa Mnanila katika Wilaya ya Buhigwe lakini kwa Wilaya ya Kakonko tunao mpaka wa Mhange. Mpaka ule nilisha mwambia hata Mheshimiwa Waziri kwamba hebu tuwekeze katika mpaka wa Mhange, tupeleke wataalam tuweke forodha pale. Nina uhakika kupitia mpaka ule Serikali itaweza kupata fedha.

**MHE. CONDESTER M. SCHWALE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Aloyce Kamamba kuna taarifa kutoka kwa Mheshimiwa Condester Schwale.

**TAARIFA**

**MHE. CONDESTER M. SCHWALE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru. Nataka kumuongezea taarifa mzungumzaji anayeongea kwamba ni kweli mipaka mingi ambayo tumeona kuna mageti ya forodha ndiyo imekuwa ni chanzo kikubwa sana cha mapato. Mfano Boda ya Tunduma, Namanga, Holili, sehemu zote hizi na nchi yetu imebahatika kuwa na mipaka mingi sana, kwa hiyo Mheshimiwa Mbunge anachokiongea ni sahihi kama eneo lake kuna mpaka akiongezewa geti la forodha kitakuwa ni chanzo kingine kizuri sana cha mapato kwenye nchi yetu.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Mheshimiwa Aloyce taarifa unaipokea?

**MHE. ALOYCE J. KAMAMBA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa ninaipokea na ninaomba basi Mheshimiwa Waziri aweze kutuboreshea mpaka wetu wa Mhange kwa kupeleka wataalam, kwa kupeleka majengo pale na tupelekewe fedha kwa ajili ya ujenzi wa barabara ya kutoka Kakonko kwenda Kinonko, kwenda Gwarama mpaka mpaka wa Mhange. Nina uhakika natumia maneno mengi kumwomba Mheshimiwa Waziri lakini akichukua ushauri huu iko siku atatumia muda mwingi kushukuru ushauri huu. Naomba sana ushauri huu uchukuliwe, waboreshe mipaka yetu nina hakika kwamba matunda yanaweza yakapatikana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, zipo ahadi za viongozi wetu, zikiwepo ahadi za Mheshimiwa Rais, Makamu wa Rais na Mheshimiwa Waziri Mkuu. Waheshimiwa Wabunge wengi wamekuwa wakiuliza katika maswali ya msingi lakini muda mwingine katika kuchangia kwao. Ahadi ni deni. Zipo ahadi ambazo Serikali imeweka kwa wananchi wetu katika maeneo mbalimbali ikiwemo Wilaya ya Kakonko. Katika mji wa Kakonko tuliahidiwa kilometa tatu na Hayati Rais Magufuli, tumejengewa kilometa 0.63, tuombe kilometa zilizobaki, kilometa mbili na ushee hivi zikamilishwe ili mji wetu wa Kakonko nao uweze kuwa na hali nzuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika bajeti ambayo imewekwa mwaka huu kuna ujenzi wa Hospitali ya Kanda katika Mkoa wa Kigoma na vile vile kuna ujenzi wa Chuo Kikuu Kishiriki cha Muhimbili. Nina uhakika fedha zikipelekwa na ujenzi ukafanyika, wananchi wa nchi jirani za Burundi, Congo, Zambia wataweza kupata matibabu katika hospitali hizo. Kwa hiyo pamoja na kwamba tutakuwa tunatoa huduma ya matibabu lakini itakuwa ni chanzo cha fedha kwa nchi yetu. Niombe sana fedha zitengwe, ardhi Kigoma tunayo ili ujenzi huo wa hospiatli ya rufaa pamoja na Chuo Kikuu Kishiriki cha Muhimbili, ujenzi uweze kuanza katika maeneo hayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kigoma tuna Ziwa Tanganyika lakini katika ziwa letu ukiangalia maziwa mengine kuanzia Bahari ya

Hindi meli zipo, Ziwa Victoria meli zipo, Ziwa Nyasa meli zipo lakini Ziwa Tanganyika ni tatizo. Usafiri katika Ziwa Tanganyika ni tatizo, meli hatuna. Tuna miaka mitatu fedha zinatengwa lakini fedha haziendi. Tuombe katika bajeti ya mwaka huu kama ni kuteseka Mkoa wa Rukwa, kama ni kuteseka Mkoa wa Katavi, tumeteseka kwa muda mrefu sana. Tuombe kwenye bajeti hii fedha ambazo zimetengwa kwa ajili ya kuwahudumia wananchi wa mikoa hiyo mitatu katika ziwa Tanganyika, tuletewe fedha meli ambazo ni za kukarabatiwa zikarabatiwe lakini na meli mpya ziweze kupelekwa katika maeneo hayo ili miji yetu ichangamke.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia panapaswa kuwa na boti za kusafirisha abiria kutoka mji wa Kigoma kwenda Katavi huku chini, kutoka Kigoma kwenda katika miji ya Congo, kutoka Kigoma kwenda Burundi. Tukiwa na mchanganyiko wa wananchi wanaotoka na kwenda jirani, wanaotoka jirani kuja katika miji yetu nina uhakika biashara itakuwepo na uchumi wa wananchi wetu utaongezeka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, zipo barabara ambazo ni za kuunganisha Mkoa wa Kigoma na mikoa mingine. Tunashukuru Serikali inaendelea kulifanyia kazi hilo; lakini bado kuna shida ya umaliziaji wa barabara inayounga Kigoma na Katavi pamoja na Kigoma na Rukwa. Kipo pia kipande ambacho kiko katikati ya Kibondo na Kasulu, pale bado pana tatizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, juzi uliona kwamba kulikuwa na picha inazunguka kwenye mitandao, lakini ule sio udongo wa Kigoma na Mheshimiwa Mkuu wa Mkoa amekwishazungumzia hilo. Yote hiyo inatokana na changamoto ambayo tunaipata kwenye barabara. Tuombe, zile fedha ambazo zinapungua na hazijapelekwa kwenye maeneo hayo, zipelekwe na ujenzi uweze kukamilika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kigoma inatengenezwa kuwa ni eneo la uwekezaji katika Kanda ya Magharibi, lakini hatuna uwanja wa ndege ambao unaweza ukaruhusu ndege kuingia na kutoka muda wote. Tuombe Uwanja wetu wa Ndege wa Kigoma upelekewe fedha za kutosha, thamani ambayo inahitajika ikamilishwe ili ujenzi unapokamilika nina hakika tutakuwa na

uwezo wa kuwapokea wasafiri kutoka Nchi jirani za Burundi, Congo, Zambia kwa sababu ni rahisi kutokea upande ule wa maeneo yale. Hivyo, Kigoma kama Mkoa utakuwa na nafasi ya kufanya biashara nzuri zaidi na hivyo kuongeza mapato ya nchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikushukuru tena kwa kunipa nafasi na naunga mkono hoja. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Mheshimiwa Vedastus Manyinyi Mathayo, atafuatiwa na Mheshimiwa Kunti Yusuph Majala, Mheshimiwa Dkt. Pius Chaya ajiandae.

**MHE. VEDASTUS M. MATHAYO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi ili niweze kuchangia kwenye bajeti hii ya Wizara ya Fedha.

Kwanza nichukue nafasi hii kumshukuru sana Mheshimiwa Rais, kwa namna alivyoweza kutupatia fedha nyingi. Pia, kusema kweli kwangu Musoma Mjini kwenye upande wa huduma za jamii sina lawama na Serikali kwa sababu imenipa fedha zaidi ya asilimia 90. Nampongeza sana.Mheshimiwa Waziri

Mheshimiwa Mwenyekiti, nasema hivyo kwa sababu ukiangalia kwenye upande wa elimu tumepata fedha za kutosha na hata kwenye ujenzi wa vyumba vya madarasa vipo vya kutosha. Vilevile kwa mwaka huu yale makali ya uchangiaji kwa wananchi yamepungua kwa maana hawakuweza kuchangia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye upande wa afya namshukuru sana Mheshimiwa Rais kwa maana ya kwamba tulitoa ombi la sisi kama Manispaa kupewa ile iliyokuwa hospitali ya mkoa na Serikali imekubali. Hata hivyo, kama hiyo haitoshi tulipata fedha milioni 500 tukaomba kwamba walau itumike kujengea uzio wa hospitali hiyo tuliyopewa, Serikali imekubali. Vile vile, tuliendelea kuomba kupata eneo kwenye ile Hospitali ya Rufaa kama hekari 20 kwa ajili ya ujenzi wa Chuo Kikuu Serikali imekubali. Kwa upande wa maji Musoma Mjini tuna zaidi ya asilimia 100. Hilo ni pongezi kubwa ambayo tunaendelea kuipa Serikali ya Mama Samia Suluhu Hassan. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama hiyo haitoshi, hata kwenye upande wa umeme Serikali imekubali kunipa umeme wa *REA* katika zile kata za pembezoni. Kwa hiyo, ndio maana leo nasema, leo naendelea kuipongeza sana Serikali ya Mama Samia Suluhu Hassan, kwa kazi kubwa ambayo imeendelea kutupatia fedha kwa ajili ya huduma za wananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na hizo huduma nzuri ambazo tumeendelea kuzipata, bado nina maombi machache. Leo ukizungumza tatizo kubwa kwa wananchi wa Jimbo la Musoma ni uchumi kwa maana ya kwamba mzunguko wa fedha ni mdogo sana. Kwa sababu mzunguko wa fedha ni mdogo sana yako mambo ambayo Serikali imeyafanya lakini bado hayajawasaidia wananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, moja, Serikali imetengeneza Sera nzuri za kuhakikisha kwamba mikopo ya gharama nafuu inawafakiwa wananchi. Pia, mikopo hiyo inatolewa na Benki kama *NMB, CRDB, TADB* pamoja na *TIB*. Kwa mfano, Serikali ilisema kwamba fedha hizo zilenge kwenye uvuvi, ufugaji, kilimo pamoja na biashara ndogondogo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, shida iliyopo ni kwamba zile benki au taasisi hizo za fedha sio rafiki kwa ajili ya wale wajasiriamali wadogo. Bado masharti yanayofuatawa ni yale yale ambapo yule mjasiriamali mdogo anahitaji atoe *security* kwa maana ya hati ya nyumba. Kwa kweli hili sasa linawapa wakati mgumu sana wale wananchi ambao wana uwezo mdogo ambao wanahitaji kuendelezwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ningeishauri Serikali kupitia kwa Mheshimiwa Waziri, waone namna gani tunaweza kuwasaidia wale wananchi wa wadogo, wale Machinga ambao wanahitaji fedha ili waweze kufanya biashara zao. Pia, kwa bahati mbaya sana ushirika mpaka sasa umeshindwa kufanya vizuri na hiyo ndio iliyokuwa njia pekee ambayo ingeweza kuwasaidia wale wafanyabiashara wadogo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ombi langu kwa sasa ambalo Serikali ingeendelea kulifanya; kwanza, wamesimamisha

hata zile fedha ambazo zilikuwa ni asilimia 10 kwa ajili ya akinamama, vijana pamoja na watu wenye ulemavu ambazo walikuwa wanapata kidogo na sasa Serikali imesimamisha na haijulikani ni lini itaweka utaratibu madhubuti ili wananchi hawa waweze kukopa na fedha hizo ziwasaidie.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa, kama hivyo ndivyo, ombi langu ni kwamba, hivi ni kwa nini Mheshimiwa Waziri asitoe fedha tukapeleka kwenye maeneo ya masoko. Kwa mfano pale Musoma, wale watu wangu wa Mwigobero, Soko Kuu, Nyasho na Soko la Saa Nane pamoja na masoko mengine wangeweza kupewa fedha wakaunda aina fulani hivi ya ushirika ambao wangeendelea kuwakopesha wale watu wao ambao ni wafanyabiashara wanaowafahamu na wanazo biashara kwenye yale maeneo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, tunadhani kwamba kwa kufanya hivyo ingeweza kuwasaidia sana ili na wao wakaendeleza maisha yao kuliko hivi sasa tunasema Serikali imemwaga fedha, imepeleka fedha lakini wale wananchi wenye uwezo wa chini hizo fedha hawazioni. Kwa hiyo, kwenye upande huo bado kwetu kuna tatizo kubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ombi lingine, tunaishukuru Serikali kwa kuingia makubaliano na Serikali ya Dubai hasa kwenye maeneo ya Bandari. Ombi langu hapo ni moja tu kwamba, Mheshimiwa Waziri baada ya ile awamu ya kwanza ambayo inahusu Bandari ya Dar es Salaam, basi kwenye awamu ya pili na ile bandari yetu ya Musoma nayo iwekewe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia tumezungumza hata katika ilani kwamba tutajenga reli ya kutoka Arusha kwenda Bandari ya Musoma. Ni matumaini yangu kwamba ukizungumza Musoma iko Karibu sana na Uganda ambako iko mizigo mingi ingependa kwenda Uganda. Kwa sababu ile Bandari ya Musoma imekufa basi na yenyewe tukiwapa hawa wawekezaji na hiyo reli ikijengwa itasaidia sana kuchangamsha uchumi wa Musoma na watu wetu wataendelea kupata ajira. Kwa hiyo, nadhani na hilo nalo mkumbuke kwenye hiyo awamu ya pili itakayofuata, basi na sisi tuweze kuwemo humo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sambamba na hilo naipongeza Serikali kupitia kwa Mheshimiwa Waziri wa Kilimo kwenye huu Mradi wa *BBT.* Mradi huu ni mzuri ambao unawagusa vijana katika kuinua uchumi wao. Hata hivyo, ombi langu hapo, Serikali ingefanya kitu kimoja, pamoja na Wizara kuendelea na Mpango huo ili uende kwa *speed* kubwa, ni vizuri fedha hizo vile vile zingetolewa kwa kila mkoa. Yaani sisi pale Mara tungepewa kama ni bilioni mbili, maeneo tunayo yangetengwa na vijana wetu wengi wangepata mafunzo pale pale na wakaweza kujenga uchumi wao kupitia kilimo. Tunadhani kwamba kwa kufanya hivyo ingewasaidia vijana wetu wengi kupata ajira na maisha yao yakaenda vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sambamba na hilo liko tatizo ambalo watu wetu linawasumbua. Serikali iliweka mpango mzuri wa zille fedha za *TASAF*. Zile Fedha za *TASAF* ni fedha ambazo zinawasaidia wale watu ambao uwezo wao ni mdogo (kaya maskini), lakini leo hii ninavyoongea sijui kwa mikoa mingine lakini kwa Musoma imeleta kero kubwa. Leo huwezi kuamini tangu mwezi wa Kwanza mpaka sasa wameendelea kusubiri na wapo watu bado hawajalipwa fedha za *TASAF*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa kutokana na hali hiyo kwa kweli imekuwa ni kero na tuone namna ya kumaliza hilo tatizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hilo, nakushukuru sana na naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Kunti Majala na Mheshimiwa Dkt. Chaya ajiandae.

**MHE KUNTI Y. MAJALA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nikushukuru nami kwa kunipatia wasaa niweze kutoa mchango wangu kwenye Bajeti Kuu ya Serikali ya 2023/2024.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nianze na suala la sekta ya uzalishaji na nitaomba nianze na Sekta ya Kilimo; kwenye Sekta ya Kilimo nitazungumuzia uzalishaji wa zao la mafuta ya kula ya alizeti. Mwaka 2021 Serikali ilikuja na mpango mkakati mzuri sana wa kwenda kupunguza ama kuondoa kabisa gharama kubwa

tunayoitumia kama nchi ya kuagiza mafuta ya kula kutoka nje. Ikatuletea wananchi mpango wa kwenda kuzalisha zao la alizeti na ikateua mikoa mitatu ya kimkakati ili wananchi wa mikoa hiyo waweze kuzalisha kwa wingi ili tuweze kuona ni namna gani tunakwenda kuondokana na wimbi kubwa la upungufu wa mafuta ya kula ndani ya nchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali pia iliingia gharama ya kuhakikisha inawapatia wakulima mbegu ambazo zitakwenda kuwasaidia kuzalisha zao hili. Hata hivyo, pamoja na dhamira hii njema ambayo awali ilioneshwa na Serikali, lakini kwa sasa naanza kuiona Serikali ikirudi nyuma kwenye dhamira hii njema waliyokuwa nayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo Waheshimiwa Wabunge wenzangu wamesema mwaka 2022, Mheshimiwa Waziri wa Fedha kwa mafuta ya kula aliweka tozo ya asilimia 35, leo anakwenda kupunguza unaweka asilimia 25. Mheshimiwa Waziri, anachokitaka kukipata hapa ni nini? Leo wakulima wa alizeti wa Mkoa wa Singida, Mkoa wa Dodoma na Mkoa wa Simiyu tuna alizeti ya tangu mwaka 2022 ipo, mwaka 2023 tumeanza kuvuna, alizeti iko majumbani mwa wakulima.

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo Serikali wameamua kupunguza kodi kwenye mafuta ya kula, wazalishaji ama wachakataji wa zao la alizeti wamefunga viwanda, wameamua kuagiza mafuta, wanauza mafuta ambayo yanatoka nje na yana gharama nafuu, ambayo hawatumii umeme na wameondoa wafanyakazi kwenye viwanda. Mwisho wa siku, changamoto tuliyokuwa tunataka kuondokana nayo ya kupunguza wimbi la uingizaji wa mafuta ndani ya nchi tunakwenda kurudi kule kule tulikotoka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, mwananchi waliyempa imani kwamba alime zao la alizeti inayojenga uchumi wa kwake binafsi…

**MHE. COSATO D. CHUMI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Taarifa.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Kunti, kuna taarifa kutoka kwa Mheshimiwa Cosato Chumi.

**TAARIFA**

**MHE. COSATO D. CHUMI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka nimpe taarifa mzungumzaji Mheshimiwa Kunti kwamba, katika hotuba ya Mheshimiwa Waziri ukurasa wa 50, katika kuhakikisha kwamba tutakuwa hatupungukiwi na dola, mojawapo ya mikakati ni kuongeza uzalishaji ili kuongeza mauzo ya bidhaa zetu nje ya nchi. Sasa, kwa hili analolisema Mheshimiwa Kunti, maana yake badala ya kuuza nje sisi sasa tunataka tuagize nje zaidi kitu ambacho kama Serikali tutaji–*contradict*. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Mheshimiwa Kunti, unapokea taarifa?

**MHE. KUNTI Y. MAJALA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naipokea kwa mikono 36. Serikali wakati mwingine wanatuchanganya Watanzania. Leo ninavyozungumza hapa mwaka 2022 gunia la alizeti ni shilingi 27,000 na mwaka 2023 wananiambia ni shilingi 20,000 mpaka shilingi 25,000. Hivi ni mkulima gani tena atalala aote ndoto mwakani aende akalime alizeti? Hivi ni kweli Serikali ndio dhamira yao kwamba tunakwenda kuondokana na hilo wimbi kubwa la uagizaji wa mafuta ndani ya nchi? Mbona tunarudi kule kule. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimwombe Mheshimiwa Waziri ili tuweze kufikia hilo lengo hii asilimia 25 aliyoiweka tunaomba aiondoe, tena hata hiyo asilimia 35 aliyokuwa ameiweka, safari hii nilikuwa nimekuja aweke asilimia 50 ili wawekezaji wa viwanda vyetu vya hapa ndani waweze kuchukua malighafi zilizoko ndani hapa ili waone akiagiza nje na akichukua za ndani ni heri achukue ndani kuliko nje. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili, sio zao la alizeti peke yake, tuna zao la mchikichi ambalo Serikali pia walifanya mkakati, Mheshimiwa Waziri Mkuu alikwenda Kigoma kuzindua zao la chikichi, wakulima wa Kigoma leo wamelima michikichi, Serikali

inaendelea kuondoa kodi kwenye mafuta, wanachotaka ni nini? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, achana na mchikichi, tuna pamba. Mimi nimeishi Mwanza, tulikuwa tunatumia mafuta ya pamba, leo mafuta ya pamba hayajulikani yalikofia ni wapi, wakati mbegu za pamba zipo na wakulima Mwanza wanalima pamba? Kwa hiyo, niishauri Serikali Wizara ya Fedha na Wizara za kisekta kwa maana ya Wizara ya Kilimo, waende wakutane wazungumze pamoja wawe kitu kimoja ili wanapokuja hapa wawe wanazungumza lugha moja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo Waziri wa Kilimo anahamasisha watu huko kulima mazao ya kuzalisha mafuta, Waziri wa Fedha anakwenda kuondoa tozo kwenye mafuta. Sasa ni kitu gani hiki wanachofanya? Wanatuchanganya, hatuwaelewi shida yao ni nini? Wazungumze, waje wakiwa na kauli moja ili tuweze kuokoa Taifa letu kwenye suala zima la uchumi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba pia nizungumzie suala zima la mbolea kwenye Sekta hiyo ya Kilimo. Msimu uliopita mbolea ya kupandia ilichelewa sana katika maeneo mengi. Nimwombe Mheshimiwa Waziri, tunaomba mwaka huu fedha itolewe mapema, mbolea ya kupandia ifike mapema ili wakulima wetu waweze kuondokana na adha kubwa ya kuchelewa kulima bila mbolea. *(Makofi)*

**WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Taarifa.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Kunti kuna taarifa kutoka kwa Waziri wa Fedha na Mipango, Mheshimiwa Mwigulu.

**TAARIFA**

**WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na mchango mzuri ambao Mheshimiwa Mbunge anachangia na Wabunge wengine wamechangia, nataka nitoe taarifa kwamba, tunapokea maoni yanayotuelekeza tupandishe kodi, lakini nilichotaka kutoa taarifa ni kwamba sio kwamba

tumeshusha. Kwenye mafuta tumebakiza kodi iliyokuwepo mwaka 2022, kwa maana hiyo kwa kuwa maoni ya Wabunge tupandishe sisi tunalipokea hilo. Hata hivyo, tulibakiza kama ilivyokuwa mwaka 2022 kwa ajili ya kukabiliana na gharama za maisha. Kwa hiyo, kwa kuwa maoni ni kwamba tupandishe tumelipokea, lakini sio kwamba tumeshusha. *(Makofi)*

**MWENYEKITI**: Ahsante. Mheshimiwa Kunti, unaipokea taarifa?

**MHE. KUNTI Y. MAJALA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru, naomba azingatie hilo. Ni kweli apandishe ili viwanda vyetu nchini viweze kufanya kazi, kodi iweze kulipwa hapa ndani ya nchi ili vijana wetu na Watanzania wenzetu waweze kupata ajira.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa nazungumzia suala la mbolea. Tunamwomba Mheshimiwa Waziri, fedha itoke mapema ili tuweze kuagiza mbolea, iletwe wakati wa msimu wa kupandia kwa ile mikoa inayopanda mapema, waweze kupata mbolea ya kupandia kuliko misimu hii ya nyuma iliyopita.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nizungumzie pia tozo ya shilingi 100 kwenye lita ya *petrol* panoja na *diesel.* Tuna kama miezi kadhaa huku nyuma ambapo Serikali iliamua kuweka ruzuku kwenye mafuta *diesel* pamoja na *petrol* kutokana na wimbi kubwa la Vita ya Ukraine. Mheshimiwa Waziri, sasa naona hapa ametuletea ongezeko la tozo ya shilingi 100.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni dhahiri kuwa unapoongeza kodi kwenye mafuta ya *diesel* na *petrol* unapandisha nauli za usafiri, lakini gharama za vyakula pia zitapanda na kila kitu nchini kitapanda. Sasa namuuliza Mheshimiwa Waziri, hivi ni kweli tumekosa vyanzo vingine vyote vilivyopo mpaka twende tena kwenye mafuta ambayo miezi michache huko nyuma tumeweka zaidi ya shilingi bilioni nne kwa ajili ya kwenda kupunguza makali ya maisha kwa wananchi wetu? Hiki kitu anachokifanya Waziri hapa kinakwenda kuleta maisha magumu zaidi kwa wananchi wetu kwa sababu kila kitu kitapanda kutokana na suala zima la ongezeko la mafuta. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niende kwa haraka haraka dakika zangu zinakwenda. Kwenye hotuba ya Mheshimiwa Waziri kuna kodi ya shilingi 1,000 kwenye mfuko wa *cement*. Ujenzi ni gharama kubwa sana, bati gharama, nondo gharama, mchanga gharama, leo tena na *cement* wanaendelea kuongeza. Mheshimiwa Mwigulu, hahitaji wananchi wake wa pale Iramba wenye nyumba za udongo *full suit* chini na juu waweze kuwa na nyumba zenye matofari mazuri ya *block* waweze kuishi kwenye maisha mazuri anakwenda kuongeza tena kodi kwenye *cement,* kwenye nondo huku hapakamatiki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimwombe kama alivyoridhia kwenye suala zima la tozo ya mafuta, halikadhalika kwenye hili suala la tozo ya *cement* ya shilingi 1,000 kwa kila mfuko aende akaiondoe ili *cement* iweze kushuka na tuweze kupata nyumba bora kwa Watanzania wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kitu kingine…

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Kunti, ahsante sana muda wako umekwisha, nakushukuru sana.

**MHE. KUNTI Y. MAJALA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mchangiaji wa mwisho mchana huu ni Mheshimiwa Dkt. Pius Chaya.

**MHE. DKT. PIUS S. CHAYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nami nashukuru sana kwa kunipa nafasi hii ya kuwa mchangiaji wa mwisho kwenye Wizara hii ya Fedha. Kipekee nimshukuru sana Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan, kwa kazi kubwa anayoendelea kuifanya katika Taifa letu. vile vile, nimshukuru Dkt. Mwigulu, Waziri wetu wa Fedha pamoja na Naibu Waziri na timu yako yote kwa kazi kubwa ambayo wanaendelea kuifanya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo nitachangia katika maeneo makubwa mawili. Eneo la kwanza nitachangia kuhusu mifumo ya

ukusanyaji mapato hususani katika Serikali za Mitaa, lakini muda ukiniruhusu nitachangia kuhusu miradi mikubwa ya maendeleo na jinsi ya utoaji wa fedha kwenye hii miradi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wote tunatambua kwamba Serikali imefanya mageuzi makubwa sana katika ukusanyaji wa mapato hususani katika Serikali za mitaa. Huko nyuma tulikuwa na mfumo ambao ulikuwa unaitwa *Local Government Revenue Collection Information System* ambao ulikuwa unatumika kwa ajili ya kukusanya mapato. Hivi karibuni watu wa TAMISEMI wameboresha ule mfumo wamekuja na mfumo unaitwa *TAUSI*. Nataka nianze kujikita kwenye ule mfumo wa mwanzo ambao tunakwenda kuu–*phase out* iwe *lesson* kwa ajili ya jinsi gani tunakwenda ku–*take off* na ule mfumo wa *TAUSI* ambao tunakwenda kuanza nao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri anajua kwamba katika mfumo wetu huu wa *Local Government Revenue Collection Information System* ulikuwa na changamoto nyingi sana. Changamoto ya kwanza ilikuwa ni suala la kutoa zile *control number* na hili nitatolea mfano kwenye ukusanyaji wa mapato. Naomba nitumie *case study* ya Manyoni. Katika Jimbo langu la Manyoni Mashariki tuna wakusanya mapato ambao wameajiriwa na halmashauri. Wale wakusanya mapato wanapokusanya ili waweze ku–*bank* wanapewa *control number*. Kuna changamoto kubwa sana kwenye huu mfumo wa kukusanya mapato hususani kwenye *control number*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, changamoto ikoje? Kuna wakati kijana amekusanya milioni tano anakwenda na milioni tano mkononi, anapewa *control number* yenye thamani ya milioni moja. Tukiwauliza watu wa *ICT* wanakwambia mfumo upo *down* hauwezi ku-*take up* taarifa zote. Hili ni tatizo kubwa sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna baadhi ya Waheshimiwa Wabunge hapa wamechangia kwamba mwezi mzima mfumo uko chini malipo mbalimbali hayafanyiki. Kwa kweli tunatambua umuhimu wa mfumo huu wa ukusanyaji wa mapato, lakini na mfumo ambao unatumika kwenye malipo. Hata hivyo, nimshauri Daktari, nadhani sasa anahitaji kuja na mkakati rasmi wa

kuhakikisha kwamba tunawezaje kuboresha huu mfumo wetu kwenye malipo na kukusanya mapato.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine kuhusu huu mfumo wetu, mfumo huu ni mzuri sana, lakini nadhani kuna sehemu ambazo *mess up*. Inakuwaje wiki mbili mfumo uko *down* lakini hatuwezi kulipa? Kwa hiyo Mheshimiwa nimwombe Waziri akae na watu wake wa Wizara ya Fedha, watu wa *IT* kwa kushirikiana na *BOT* watuambie, tunawezaje kuufanya mfumo huu uwe *user friendly* na watu walipe kwa wakati?

Mheshimiwa Mwenyekiti, hawa vijana wanapokusanya mapato hawatakiwi kukaa na fedha nyingi. *Risk* ikoje? Kijana amekusanya milioni tano anapokwenda kuomba *control number* aka–*bank* zile fedha anatolewa *control number* ya milioni moja, milioni nne anarudi nayo.  *What happened* kwa Manyoni? Ilifika kipindi sisi tulikuwa na *defaulters* zaidi ya milioni 100 kwa mwaka. Watu ambao ukiwauliza hii hela mbona unadaiwa haamini kama anadaiwa. Kumbe kipindi kile alitolewa *control number* yenye *value* ya chini akajua labda hawa watu wamesahau ile milioni nne akaa nayo, muda ukaenda akaamua kuitumia. Hili ni tatizo kubwa. Kwa hiyo, namshauri Mheshimiwa Waziri, kwenye huu mfumo wa kukusanya mapato ambao wmeuanzisha sasa hivi wa *TAUSI* namshauri waende wakafanye maboresho.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niwapongeze TAMISEMI na Waziri wa Fedha, wameboresha huu mfumo wa zamani wa kukusanya mapato wamekuja na huu mfumo mpya ambao unaitwa T*AUSI* ambao halmashauri nyingi zimeanza kuutumia, lakini bado kuna changamoto moja. Mfumo huu unahitaji elimu itolewe kwa wananchi. Kwa mfano sasa hivi, *business license* zote zinatolewa kwenye mfimp wa *TAUSI* kila kitu, mfanyabiashara, fundi anatakiwa ajisajili kwenye mfumo wa *TAUSI,* ni wangapi wanaujua huu mfumo? Tunahitaji kutoa elimu kwa wananchi ili waujue huu mfumo na iwe rahisi ku–*take off* tunapoanza ile Julai kwa zile halmashauri ambazo bado hazijaanza kuzitumia ili ziweze kuutumia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine kwenye huu mfumo wa kutoa *control number,* kama kijana anaweza akakusanya milioni

tano anapokwenda anakuta *system* iko *down* au inatoa bili ambayo iko chini, ningeshauri watengeneze *back up system* kuliko hawa vijana kukaa na hela muda mrefu, inakuwa ni *very risk* kwao. Matokeo yake tunawaingiza kwenye *risk* ya kudaiwa na tunakuwa na *defaulters* wengi. Kwa hiyo nashauri waandae *back up system* ambapo kama mfumo uko down hawa vijana wasikae na fedha nyingi nyumbani tuwe na mfumo ambao tunaweza kwenda ku–*bank, then* wakafanya *reconciliation*. Lengo ni kuhakikisha kwamba tunapunguza *misuse* za fedha, lakini pia tunapunguza upotevu wa hizi fedha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la pili ambalo nataka kuchangia ni kuhusu miradi mikubwa ya maendeleo. Niishukuru sana Serikali, kwa Manyoni tumepata fedha nyingi sana. Tumepewa bilioni nne za Ujenzi wa Shule ya Wasichana ya Mkoa. Vile vile, tumepewa zaidi ya bilioni moja kwa ajili ya Ujenzi wa Chuo cha *VETA*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Dkt. Mwigulu anatambua Daraja la Sanza. Kwenye kila Ilani ya Uchaguzi huwa Daraja la Sanza linawekwa. Nafahamu sasa hivi lipo kwenye mchakato wa manunuzi. Nimwombe Waziri mwaka unapoanza sasa, huyo mkandarasi akapatikane na ujenzi wa daraja la Sanza uweze kuanza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili na Mheshimiwa Waziri anatambua kuna Mradi pale Mwahalala, Kituo cha Pamoja cha Ukaguzi wa Magari. Ule Mradi wa zaidi ya bilioni 30 ulisimama tangu mwaka 2016. Pale kuna majengo yanaendelea kuoza. Sasa ningeshauri kwenye bajeti hii ingawa sijaona anapoelezea, naomba Waziri anapokuja ku–*wind up* atuambie, nini mpango wa Serikali kuuendeleza ule mradi ambao umesimama tangu mwaka 2016.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pale kuna nyumba, tunashauri kama Serikali imeacha huu mradi waturuhusu zile nyumba zitumiwe na watumishi. Tuna Shule za Sekondari, Shule za Msingi, zahanati, nyumba zile zinaweza zikatumika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la mwisho, kuna huu Mradi wa Mji wa bilioni 12 wa Kintinku-Lusilile. Kwanza, namshukuru sana Waziri wa Fedha, kwa kweli kwenye huu mradi ametusaidia sana na sasa hivi mkandarasi yuko *site* ameanza kazi. Hata hivyo, bado mkandarasi anadai zaidi ya bilioni tano ili aweze kukamilisha huu Mradi. Kwa hiyo nimwombe Mheshimiwa Waziri, kwenye huu mradi ambao unakwenda kwenye vijiji 11 ambao una zaidi ya miaka 15 haujakamilika, atusaidie ili uweze kukamilika kwa wakati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, niendelee kumpongeze sana Mheshimiwa Rais, lakini nimpongeze Mheshimiwa Mwigulu na timu yake na naomba kuunga mkono hoja. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Dkt. Pius Chaya.

Waheshimiwa Wabunge tunawashukuru sana kwa michango ya mchana huu. Sasa ninayo matangazo machache.

Tangazo la kwanza, Katibu wa Bunge anawatangazia Wabunge wote kuwa Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI) inaendelea na zoezi la ukusanyaji wa maoni ya ujenzi wa Ofisi za Waheshimiwa Wabunge katika Majimbo ya Tanzania Bara. Katika kukamilisha zoezi hilo TAMISEMI, imeandaa dodoso la ujenzi wa ofisi hizo ili kupata maoni kutoka kwa Waheshimiwa Wabunge ili kusaidia kufanya maamuzi ya suala hilo. Dodoso hilo litagawiwa kwa kila Mbunge na baada ya kuujaza lirejeshwe kupitia Wahudumu wa Ukumbini. Waheshimiwa Wabunge wote wa Tanzania Bara mnaombwa kujaza dodoso hili muhimu.

Waheshimiwa Wabunge, naendelea kuwakumbusha Waheshimiwa Wabunge wote wa Chama cha Mapinduzi kama nilivyotangaza asubuhi, Katibu anawatangazia Waheshimiwa Wabunge wote wa CCM kikao maalum cha *Party Caucus* leo Jumanne saa saba baada ya kusitisha shughuli za Bunge. Kikao hicho kitafanyika katika ukumbi wetu wa Pius Msekwa.

Waheshimiwa Wabunge, watakaoanza kuchangia jioni ni Mheshimiwa Dkt. Christine Ishengoma, Mheshimiwa Ramdhani

Ighondo, Mheshimiwa Dkt. Oscar Ishengoma Kikoyo na orodha inaendelea.

Baada ya kusema haya, nasitisha shughuli za Bunge hadi saa kumi na moja kamili jioni.

*(Saa 7.05 Mchana Bunge Lilisitishwa hadi Saa 11. 00 Jioni)*

*(Saa 11.00 Jioni Bunge Lilirudia)*

*Mwenyekiti (Mhe. Najma Murtaza Giga) Alikalia Kiti*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, tukae. Katibu.

**NDG. RUTH MAKUNGU-KATIBU MEZANI:**

## HOJA ZA SERIKALI

### Hali ya Uchumi wa Taifa kwa Mwaka 2022 na Mpango wa Maendeleo wa Taifa kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024

**na**

### Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Serikali kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024

*(Majadiliano Yanaendelea)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na majadiliano yetu, tutaanza na Mheshimiwa Dkt. Christine Ishengoma, Mheshimiwa Ramadhani Ighondo na Mheshimiwa Dkt. Oscar Kikoyo ajiandae.

**MHE. DKT. CHRISTINE G. ISHENGOMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipatia nafasi ili niweze kuchangia bajeti ya Waziri wa Fedha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa namshukuru na nampongeza Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa mambo anayoyafanya sana miradi anaisimamia na ametoa hela

nyingi kwenye bajeti hii. Ni kweli bajeti hii imemgusa kila mmoja kwenye kila nyanja kweli tunamshukuru Mheshimiwa Rais.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hapa ninapoanza kuchangia nianze na ukusanyaji wa mapato. Naomba sana Serikali inakusanya mapato na ina njia ambayo imetumia ya kukusanya mapato lakini nilikuwa nashauri kuwa ifanye utafiti mzuri ambao utaweza kukusanya mapato. Mimi ni mmojawapo nikienda dukani kununua kitu naomba risiti, mmoja mmoja atakupa risiti lakini wengi watakuambia kuwa *EFD machine* zimeharibika hazifanyi kazi, kwa hiyo unakuta Serikali tunapoteza sana mapato kwa kutodai risiti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ushauri wangu, kuna viongozi wengi ambao wako Wilayani, ambao wako Mkoani, ambao wako kwenye Halmashauri naamini tukiwa-*task* waweze kufuatilia Maafisa Biahsara wataweza kufuatilia na kuwachukulia hatua hao wafanyabiashara ambao hawataki kutoa hela zetu kusudi tuweze kupata mishahara pamoja na wale watu wafanyakazi waweze kupata mishahara yao pamoja na miradi ya maendeleo iweze kutimilika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ni kuwa mapato tunapata lakini kuna Wakandarasi, Wakandarasi kwa kweli wana shida wanafanya kazi zao lakini hawalipwi. Kwa hiyo, nilikuwa nashauri Mheshimiwa Waziri wa Fedha waangalie hawa Wakandarasi wanaishi maisha mabaya na huku wameshafanya kazi. Kwa hiyo, naomba muwaangalie walipwe hela zao ili kusudi waweze kuendelea na kazi zingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naongelea kuhusu asilimia kumi ya mapato ya Halmashauri. Hii asilimia 10 ambayo akina mama pamoja na vijana pamoja na wenye ulemavu ambayo wanatengewa ni nzuri sana, lakini kwa sababu ya changamoto Serikali imesema kuwa bado wanaifanyia kazi. Naomba na ninashauri kuwa kwa sababu ni jambo muhimu sana ambalo linawakomboa sana hasa wanawake wakiwepo na wanawake wa Morogoro na wanawake wote waliokuwa wanapata mikopo hii, naomba muifanyie haraka sana kusudi tuweze kupata ufumbuzi wake, waweze kuendelea na mikopo yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ambalo naongelea ni reli ya mwendokasi. Naipongeza Serikali nampongeza Mheshimiwa Rais kwani anafanya mambo mazuri sana. Tumeambiwa kuwa kipande cha Dar es salaam mpaka Morogoro ambacho kina kilomita 300 karibu kinakamilika kina asilimia 98.14 ambayo sasa hivi kinakamilika na mabehewa ninyi mmeyaona mabahewa ya ghorofa ambayo yameletwa, vichwa ambavyo vimeletwa naaamini kuwa hivi karibuni na kama sikosei labda mwezi ujao kipande cha Dar es salaam mpaka Morogoro kitaanza safari zake. Kwa hiyo, naomba na ninatoa ushauri kwa wananchi ambao watatumia hii reli waitunze, tuzidi kuitunza kusudi iweze kuendelea vizuri sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakuja kwenye barabara, Mheshimiwa Rais ameunganisha barabara, Mkoa kwa Mkoa na ameunganisha mpaka nchi yetu na nchi jirani. Kwa hiyo, licha ya kumpongeza naomba barabara ya kuanzia Kibaha hadi Morogoro ambayo ina njia nne ingawaje imefanyiwa usanifu, hela zikitengwa iweze kukamilika kwa ni kuna foleni ya malori. Nanyi ni kweli mnasafiri kwenye barabara hii mnaiona hiyo foleni ya malori inavyosumbua, kwa hiyo naomba sana hiyo barabara kwenye bajeti hii iweze kufanyiwa kazi ili kusudi tuweze kupata usafiri ambao unaeleweka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna barabara ambayo huwa tunaisemea mara kwa mara ya Bigwa mvua inakwenda kwenye Bwawa la Mwalimu Nyerere, tunayo barabara tunaisema Ubena - Zomozi mpaka kwenda mpaka Bwawa la Mwalimu Nyerere ndiyo kwenye mpango ilikuwepo, lakini naomba itengenezwe kwa sababu ni muda mrefu tumeiongelea hii barabara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niongelee kuhusu kilimo. Kilimo kinaajiri wananchi ambao ni asilimia 65.5 na zaidi. Kwa hiyo, kilimo ukitaka watu waweze kutoka kwenye umaskini ni sekta za uzalishaji ambazo sekta za uzalishaji ni kilimo. Kwa hiyo, kilimo namaanisha uvuvi, mifugo ambazo zinaweza kuwakomboa wananchi. Kwa hiyo, fedha zilizotengwa huko huko wakati mwingine tunatenga fedha hazitoki, kwa hiyo, tutakapopitisha hiyo bajeti naomba fedha tutakazozitenga zitoke na hasa kwa ajili

ya kilimo cha umwagiliaji kutokana mabadiliko ya tabianchi ambacho kitaweza kumkomboa mwananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana na nampongeza Mheshimiwa Rais kwa bajeti ambayo imetengwa ambayo tunaiongelea sasa hivi bilioni 98.8 kitu kama hicho, hiyo bajeti ni kubwa sana. Bilioni 970.8 ambayo ndiyo bajeti ya kilimo, naamini ni kubwa sana ikisimamiwa vizuri sana itaweza kumkomboa mwananchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, natoa angalizo kuwa hiyo hela ambayo imetengwa naomba kadri bajeti zinapokuja hizi zinazokuja mbele mwaka kwa mwaka tuweze kupata bajeti zaidi ya hii ili tuweze kufikia Azimio la Malabo na Maputo ambayo ni asilimia kumi ya bajeti nzima iende kwenye kilimo. Kwa hiyo, naamini Mheshimiwa Rais anayependa kilimo na kukipa kipaumbele naamini atafanya hivyo, Mama ni mzuri Mama anafanya vitu vizuri anafanya kazi nzuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niongelee kuhusu mazingira. Nampongeza sana Mheshimiwa Makamu wa Rais kwa kuisimamia hiyo kampeni ya kupanda miti. Naomba sana wananchi, itaendelea kutenga fedha zinazotengwa kwa mambo ya Maliasili na Mazingira, tuweze kusimamia hiyo miti tuipande ambayo kila Halmashauri, kila Wilaya ni 1,500,000 inapandwa lakini ikipandwa tuweze kuifuatilia kuwa kweli inastawi na haikauki, hayo tunaweza kwa sababu ya mazingira. Pia licha ya kupanda miti tumehamasisha, wanahamasishwa, tuwahamasishe wananchi waweze kutumia nishati mbadala hasa kwa kupika, ili kusudi tuweze kupunguza kutumia mikaa pamoja na kuni tuweze kwenda vizuri kutunza mazingira yetu na yatatutunza naamini tukiweza kutunza haya mazingira.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niongelee kuhusu elimu. Tunamshukuru Mheshimiwa Rais, tunaishukuru Serikali ya Awamu ya Sita kwa mambo inayofanya ambayo ni wanafunzi wetu watasoma mpaka kidato cha sita bila ya malipo ya *school fees,* pia imetoa mambo ya vyuo vya kati itayafanyia vizuri sana. Pia na Vyuo Vikuu inatoa mikopo ya kutosha kwa hiyo naamini

itaendelea kutoa mikopo kwa kila mwanafunzi kwa sababu hapo baadae wataweza kurudisha mikopo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niongelee kuhusu umeme, tunashukuru Serikali yetu, ni kweli watu walikuwa hawajui umeme lakini miaka hii umeme umesambaa kila mahali na tunaamini tunakwenda kwenye vitongoji kila mmoja anayeweza kuweka umeme kwa shilingi 27,000 huko vijijini ataweza kuweka umeme. Kwa hiyo, tunampongeza mama anafanya kazi kubwa. Lakini naomba kuna Kata za Morogoro, Mgeta, Tarafa ya Mgeta ambayo bado Kata nzima vijiji vyote Kata kama nne hazijapata umeme. Kwa hiyo nashauri, namuomba Mheshimiwa Waziri anayehusika, aweze kuliona hilo jambo kuwa vijiji vyote vya Kata nzima havina umeme, Kata, Tarafa ya Mgeta vijiji vya Kata nne na zingine kwenye Wilaya ya Mvomero.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nisemee kuhusu barabara. Barabara za Mkoa wa Morogoro hasa za vijijini zikiwepo zinazosimamiwa na *TARURA* naomba ziangaliwe. Nakuomba sana ziweze kuangaliwa ziweze kutengenezwa ziweze kukamilika watu wa *TARURA* waweze kuona wana jukumu la kuweza kuona hizo barabara zinatengenezwa kwa sababu tuweze kwenda vizuri maendeleo ni maendeleo namshukuru Mama Samia namshukuru Rais wetu anatupenda na sisi tumpende.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana nakushukuru na nasema ubarikiwe na Mwenyezi Mungu, ahsante sana, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Dkt. Christine Gabriel Ishengoma. Nilimtaja Mheshimiwa Abeid Ramadhani Ighondo atafuatiwa Mheshimiwa Dkt. Oscar Ishengoma Kikoyo na Mheshimiwa Benaya Kapinga ajiandae.

**MHE. ABEID R. IGHONDO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa na mimi fursa walau nichangie katika hotuba hii ya Mheshimiwa Waziri ya Bajeti Kuu ya Serikali, kwa mwaka wa fedha 2023/2024.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nianze kwa kumpongeza Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa uchapaji kazi wake mzuri, pia nimpongeze Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri pamoja na timu yake nzima iliyochakata bajeti hii ambayo hivi sasa tumeiona imetupa vipaumbele vikubwa kadhaa ikiwemo kwanza kilimo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kilimo kimepewa kipaumbele namba moja na hasa hasa kwenye maeneo ya umwagiliaji pamoja na pembejeo za kilimo. Hapohapo ile miradi mikubwa ya kimkakati ambayo ndio tunasema inaenda kukomboa uchumi wa nchi yetu Bwawa la Mwalimu Nyerere, *SGR*, haya mambo kwa kweli tunayo kila sababu ya kumpongeza Rais wetu Samia Suluhu Hassan ambaye tunasema ndiye mbeba maono ya nchi yetu kuelekea 2025. Nimuombee Rais wetu afya njema na tumpe moyo, tumtie moyo Rais wetu kwa kazi hii anayoifanya ili aendelee kututumikia Watanzania wenzake kwa moyo na kwa upendo wa dhati. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili nilete shukrani zangu kwa Mheshimiwa Waziri wa Fedha Dkt. Mwigulu Nchemba, siku ile nilipoomba barabara ile ya Singida - Ilongero nimshukuru Waziri wa Ujenzi aliahidi kunipa kilomita 10 za lami, lakini na yeye Waziri wa Fedha akaniambia bwana tunaenda kutafuta fedha kwa barabara nzima iwekwe lami, hiyo ahadi tunaishukuru wananchi wa Singida Kaskazini lakini tunatarajia sasa tuone utekelezaji. Tunatarajia tuone utekelezaji kuanzia mwaka huu wa fedha kama Waziri Mbarawa alivyosema lakini hata wewe Mheshimiwa Waziri wa Fedha kama ulivyoahidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hotuba yangu kubwa ya leo pamoja na mazuri mengi niliyoyaona kwenye bajeti hii ikiwemo suala la wanafunzi wa elimu ya vyuo vya kati kusoma *for free* kwa mikopo kutoka Serikalini, kwa kuondolewa ada lakini pia kwa kuendelea kutoa ruzuku kwenye mbegu kwenye mbolea na pembejeo za kilimo. Nina mambo machache ambayo ningependa kuyawasilisha kwa ajili ya kuyafanyia kazi:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kuna suala la ule mfumo wa *electronic stamp (ETS)*. Mfumo huu ni mzuri lakini umekuwa na

malalamiko kutoka kwa wadau kwamba una gharama kubwa, yule mwekezaji anayetoa hii huduma imekuwa kidogo ina malalamiko kutoka kwa wadau. Kwa hiyo, niombe Serikali ichukue fursa ya kukutana na yule mdau ili kupunguza zile gharama ili wale wananchi wanaopata hii huduma wapate huduma hii kwa urahisi.

Pili, zile *stamp* zilizopo kwenye chupa za maji kwenye soda na kadhalika zimekuwa zina malalamiko kwa hiyo niombe Serikali ikae na yule mwekezaji waweze kuondoa zile gharama ziwe za kawaida kwa ajili ya kupunguza hata gharama pia za maji kwenye matumizi ya kawaida. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niseme moja kubwa leo kwenye eneo la kilimo hususani zao la alizeti. Wenzangu wamezungumza sana wanaotoka Mikoa ya Kati, alizungumza sana Mheshimiwa Yahaya Massare jana amezungumza pia Mheshimiwa Kunti Majala asubuhi ya leo lakini na Wabunge wengine wanaotoka kwenye maeneo yanayozalisha Alizeti. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuanzia mwaka wa fedha 2021/2022, 2022/2023 Wizara ya Kilimo, Waziri Mkuu kwa ujumla wake wametuhamasisha sana kulima alizeti, tunashukuru tumeona pembejeo za kilimo, tumeletewa mbolea, mbegu zenye ruzuku lakini hatua hizo zimewezesha kwa kiwango kikubwa kuongeza tija kwenye uzalishaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, alizeti imelimwa kwa kiwango kikubwa sana nchini, kuanzia Iringa, Singida Kaskazini, mpaka kule Maluga, Kiomboi kule ndani kule Shelui wanakolima alizeti, wamelima sana alizeti na sasa hivi pale barabarani tunakopita pale Maluga unaona alizeti ni nyingi kweli kweli, ukienda Iramba ndani kule Mkoa wamelima sana alizeti kwa wingi, nyingi kwelikweli nawapongeza sana wa Singida, Wanasingida, Watanzania kwa ujumla wanaozalisha alizeti. Niwapongeze na watu wa Ilongero, Mudida na kule kwingine kote walioitiia wito wa Serikali kwa kulima na kuzalisha alizeti kwa wingi, wameipokea kauli mbiu wamepokea kauli za viongozi wao kuhakikisha wanazalisha sana alizeti. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, shida inakoanzia ni wapi? Kwa masikitiko makubwa sana, kwa majonzi makubwa sana, sasa hivi tunavyoongea hapa bei ya gunia moja la alizeti ambalo lina ujazo wa kilo sitini mpaka sabini ni shilingi 25,000 umeuza sana 35,000. Kwa kweli ni masikitiko makubwa sana kwa mfumo huu, hili tatizo limeletwa na sisi tunaoagiza mafuta ya kula kutoka nje ya nchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naiomba Serikali yangu ambayo naiheshimu sana na kwa kweli suala la kilimo lipo kwenye Ilani ya Uchaguzi ya CCM ambayo mimi niliinadi mwaka 2020, wakati tuko kwenye Uchaguzi Mkuu, kwamba tunakwenda kukipa kipaumbele kilimo na tunaenda kuki-*modernize* kiwe cha kisasa, kwenye ukurasa wa 33 kuendelea mpaka huko inakoenda kwamba Serikali ya CCM inakwenda ku-*modernize* kilimo. Sasa ku-*modernize* kilimo maana yake ni kuhakikisha hata kwenye masoko yetu, sisi wenyewe tu-*export* nje ya nchi, siyo tu *import*. Nashangaa inawezekanaje tuwe tunaagiza mafuta ya kula nchini wakati tuna mawese, tuna alizeti, karanga na pamba. Sisi ndio tunatakiwa tupeleke mafuta ya kula nje ya nchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Kunti alizungumza vizuri sana asubuhi kuhusu eneo la alizeti. Naomba mchango wake nami niutambue kwenye eneo la alizeti. Naomba Mheshimiwa Waziri kwenye eneo la alizeti, katika suala la kuagiza mafuta ya kula kutoka nje ya nchi, hii tunailetea nchi yetu laana. Tunawaumiza wakulima wetu, tunawaumiza wananchi wetu ambao maisha yao yanategemea kilimo. Mwananchi amelima kutoka mwezi wa Kumi na Moja mpaka leo Mwezi wa Sita ndiyo anaenda kuuza. *Almost seven month*s yuko kwenye kilimo anahangaika kuzalisha, unakuja kumwambia leo unamwagizia mafuta kutoka nje. Hii siyo sawa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naiomba sana Serikali yangu ifanye mambo mawili. La kwanza kwenye hili, ili kumsaidia mkulima, kumsaidia mwananchi wa kawaida wa nchi yetu, la kwanza tuhakikishe ile nakisi iliyopo, tunasema mahitaji yetu ya ndani ni tani 650,000, lakini tuna uwezo wa kuzalisha tani 300,000, basi tusiagize hivi sasa. Tusubiri wakati tunapoona nakisi kule mwishoni ndiyo tuagize, lakini tuagizie kwa kutumia vibali kulingana na

upungufu uliopo. Sasa hivi ni soko huria, ukimwambia mtu agiza, aneleta zaidi ya hizo. Anaweza kuleta tani 1,000, tutawezaje kudhibiti hili? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba sana twende kwa takwimu. Tuangalie kwanza tuna viwanda kiasi gani vinavyozalisha mafuta? Vina uwezo gani? Tuangalie na uzalishaji tunaoufanya, kweli hii nakisi tunayosema ya tani 350,000 ndiyo iko hivyo hivyo? Maana yake wenzetu wanapoambiwa walete, wanaagiza mpaka wanakuja kuua soko letu la mazao ya ndani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, tunaomba sana Waziri anisikie na Serikali kwa ujumla, kwamba kuendelea kuagiza mafuta kutoka nje ya nchi ni kuendelea kumdidimiza mkulima ambaye maisha yake asilimia 100 yanategemea hiyo mbegu ya alizeti, yanategemea kilimo, hana mshahara, hana kitu kingine chochote kinachomwingizia mapato kwenye maisha yake. Anategemea apate dawa, apate ada ya watoto wake, na kila kitu kwenye maisha yake anategemea alizeti au mazao. Sasa sisi tunavyoendelea kuagiza kutoka nje, tunamnyanyasa, tunamuumiza huyu mkulima. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, kwenye eneo la alizeti, kuagiza mafuta kutoka nje, naomba Serikali ilisikie hili na kulifanyia kazi. Serikali ifanye tafiti, kwa nini sisi mpaka leo tunaagiza mafuta kutoka nje ya nchi wakati ardhi yetu ukianzia Kigoma uende mpaka Pwani, kote unakutana na alizeti. Ukianzia Ruvuma mpaka Arusha kote tunalima alizeti; tunalima chikichi, tunalima pamba, inakuaje mpaka leo sisi ni waagizaji wa mafuta kutoka nje? Tuna hujuma? Hatufanyi kazi ipasavyo? Tatizo liko wapi? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba sana hili Mheshimiwa Waziri alichukue, ninashukuru kwamba hata yeye ni mkulima namba moja, hata kwenye hotuba yake hapa alisema amesoma kwa kupitia mifugo, amesoma kwa kupitia kilimo, kwa sababu kilimo na mifugo vinaenda pamoja. Naamini hili ninalolizungumza analielewa kaka yangu *doctor,* tunatarajia baadaye awe Profesa. Sasa Uprofesa huu tuulete kwenye maisha halisi ya

wananchi wale waliotuzaa sisi wakatusomesha mpaka leo tuko hapa. Mheshimiwa Waziri … *(Makofi)*

**MHE. ZUBERI M. KUCHAUKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Taarifa.

**MHE. ABEID R. IGHONDO:** …tunatarajia nao wapate manufaa na matunda.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Ramadhani kuna taarifa. Iko wapi taarifa?

**MHE. ZUBERI M. KUCHAUKA:** Kuchauka.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Kuchauka.

**TAARIFA**

**MHE. ZUBERI M. KUCHAUKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi ya kutoa taarifa. Nampa taarifa mzungumzaji, anachangia vizuri sana. Nami ninazo taarifa kutoka kwa wakulima wanasema, katika kuagiza haya mafuta humu, kuna watu wananufaika, ndiyo maana wanaendelea kuagiza. *(Makofi/Kicheko)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Ramadhani Ighondo, unapokea hiyo taarifa?

**MHE. ABEID R. IGHONDO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nimeshaunga mkono hoja, lakini pia anachokizungumza Mheshimiwa Kuchauka ni kweli. Hili eneo la kuagiza mafuta ndiyo linalowatesa wananchi kwa sababu kuna watu wananufaika na wametundika mirija yao, wanawatesa wananchi wenzangu kule Singida Kaskazini, Iramba, Mkalama pamoja na maeneo mengine kwa sababu ya fursa wanazozitumia za kuagiza mafuta kutoka nje.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ninashukuru. Naunga mkono hoja. Naomba hili moja kubwa la leo la eneo la mafuta ambalo nimezungumza, lichukuliwe na Serikali na lifanyiwe kazi, ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Ramadhani Ighondo Abeid. Nilimtaja Mheshimiwa Dkt. Oscar Ishengoma Kikoyo, Mheshimiwa Benaya Kapinga na Mheshimiwa Michael Costantino Mwakamo, ajiandae.

**MHE. DKT. OSCAR I. KIKOYO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa fursa nami kuchangia hoja ambayo iko mbele yetu. Nimesoma Bajeti ya Serikali, nimeona kuna mambo mengi mazuri, hongera sana Mheshimiwa Waziri. Naipongeza Serikali yangu ya Chama cha Mapinduzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa naangalia tozo ya Shilingi 100/= kwenye mafuta. Nadhani tunapoweka tozo kwenye mafuta, ina madhara makubwa kwenye uchumi kwa sababu inakwenda kwenye usafirishaji na itasababisha mpasuko, kupanda gharama kwenye sekta nyingine za uchumi. Nashauri, tuna mitandao ya kijamii; *Instagram* au tuseme *social media,* tungeangalia huko tukaiepeleka kule kwa sababu unapoipeleka kwenye *social media* haina madhara makubwa kama ambavyo tumependekeza kuipeleka kwenye mafuta. Huo ni ushauri wangu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitajikita kwenye kilimo. Wachangiaji wengi wamesema na ndivyo hali ilivyo, kilimo kinahusisha watu wengi Tanzania, hasa wenye kipato cha chini. Tunao Mradi wa *BBT,* lakini huku kwetu tunakotoka tunalima zao la kahawa, ndiyo zao kubwa sana, lakini ni zao ambalo linaiingizia kipato kikubwa nchi hii. Ukiangalia wakulima ambao wanachangia pato la Taifa kupitia zao la kahawa, ni wakulima wadogo wadogo wenye mashamba madogo madogo; ekari moja, nusa ekari na ndio hao wanaochangia uzalishaji wa kahawa hasa Mkoa wa Kagera. Mkoa wa Kagera tunazalisha zaidi ya tani 40,000 na ndiyo hizi tunakwenda kuuza nchi za nje na kutuletea fedha za kigeni, lakini ukiangalia mashamba ya wakulima, yanatia hofu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napendekeza kwenye bajeti hii tuangalie jinsi ya kuongeza uzalishaji wa kahawa kwa kuyahudumia haya mashamba madogo madogo ya wakulima wadogo wadogo, ambao huwa wanawasomesha watoto wao na kutunza familia zao. Haya mashamba tukiyapatia kipaumbele,

tukahakikisha kwamba wanapewa mbolea na ruzuku kuhakikisha kwamba haya mashamba yanahudumiwa; na ndiyo yanaweza kutoa kwenye mauzo ya kahawa ambapo mwaka 2022 tulipata shilingi bilioni 240 tukaenda mpaka shilingi bilioni labda 500 tukaanza kushindana na jirani zetu Uganda. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiangalia Uganda na Tanzania, pamoja na kwamba Tanzania ni nchi kubwa, lakini bado mauzo yetu ya nje ni kidogo. Hili ni eneo ambalo tunaweza tukapata fedha nyingi kutokana na mauzo ya kahawa. Naomba tulifanyie kazi. Ila hatuwezi kulifanyia kazi hivi hivi, lazima tuangalie na kiwango gani cha kahawa tunauza nje ambacho bila kuongezea thamani. Tuna viwanda vidogo vidogo. Kwa mfano, kwenye wilaya yangu pale, vipo viwanda ambavyo vinaongeza thamani zao la kahawa, lakini hatuvipatii kipaumbele kuongeza kiwango cha kahawa ambacho wanakifanyia kazi na kuki-*process* ili tuuze nje zao ambalo tumeshaliongezea thamani. Kahawa nyingi tunaiuza kama *raw material*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na hiyo, pale Kagera tuna kiwanda kikubwa cha *TANICA*. Pamoja na kwamba Mkoa wa Kagera tunazalisha zaidi ya tani 40,000, lakini kiwango ambacho kiwanda chetu cha *TANICA* kinaweza ku-*process* ni tani 1,500. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Naishukuru Serikali kupitia Wizara ya Kilimo, mwaka huu kupitia Bajeti ya Kilimo, Mheshimiwa Waziri ameahidi kutupatia Shilingi bilioni 8.7 ili kukipatia kiwanda hiki mtaji wa uendeshaji, lakini kukipatia mtaji wa uendeshaji pekee yake, haiongezi lolote. Napendekeza kiwanda hiki tukipatie mtaji wa kuboresha mitambo yake, kwani kina mitambo ambayo imepitwa na wakati, teknolojia wanayoitumia inasababisha kupoteza kahawa nyingi. Ndiyo maana mauzo yetu ya nje kwa kahawa ambayo imeshakuwa *processed* ni madogo mno.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vile vile pamoja na kwamba ni madogo, ukiangalia bei ya kilo moja ambayo inazalishwa na *TANICA,* kwenye soko inauzwa dola 8.5 wakati kahawa inayotoka nje kwa kilo moja hiyo hiyo inauzwa dola nne. Sasa ukiangalia uwiano wa bei, mazao ambayo yanatokana na kiwanda chetu

hayawezi kushindana katika soko lolote, kwa sababu tunazalisha kwa gharama kubwa, kwa kuwa teknolojia tunayoitumia ni ya zamani. Kiwanda hiki kilijengwa tangu mwaka 1963 na tangu hapo hatujawahi kukipatia mtaji kuboresha teknolojia. Nadhani ni muda muafaka sasa kukipatia mtaji kiwanda hiki ili tuweze kubadilisha teknolojia kiweze kuzalisha na mazao yake yaweze kushindana na mazao mengine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiangalia kahawa ambayo tunaizalisha hapa nchini, hasa ile inayotoka Bukoba ni kahawa nzuri, na ukiipeleka kwenye Soko la Dunia popote, itapata wanunuzi lakini tatizo tulilonalo ni kwamba hatuwezi kushindana kwa sababu hatuna teknolojia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikiachana na suala la kahawa, wakati tunachangia Wizara ya Ustawi wa Jamii, tuliongelea masuala ya ustawi wa jamii na maendeleo ya jamii. Tunalo tatizo kubwa sana nchi hii. Wizara yenyewe inaongelea zaidi masuala ya maendeleo ya jamii na masuala ya maendeleo ya jamii ni Wizara zote. Tumesahau Sekta ya Ustawi wa Jamii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napendekeza Mheshimiwa Waziri anapokuja kutoa hitimisho, tuangalie hili suala la ustawi wa jamii. Tumeongelea vijana wetu kuharibiwa, tumeongelea matatizo ya jamii yanayoendelea, ni kwa sababu tumesahau hii sekta muhimu ya ustawi wa jamii. Tunakimbizana na maendeleo, lakini tumeshindwa kuwekeza vya kutosha kwenye ustawi wa jamii. Napendekeza tuangalie kwenye bajeti yetu, tuone kwa jinsi gani tunaweza kuisaidia Wizara tukajenga *rehabilitation centers* kwenye majiji makubwa ambako kuna mmomonyoko mkubwa sana wa maadili na vijana wetu wameharibiwa, ili wale ambao wamebainika kwamba wamepata matatizo/wameharibiwa waweze kupelekwa kwenye *rehabilitation center* na kuwarududisha katika hali yao ya kawaida, waweze kubaki kwenye jamii na kuendelea na uzalishaji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikirudi kwenye jimbo langu, naishukuru sana Serikali, imefanya kazi kubwa sana, imetujengea shule, vituo vya afya na hospitali. Kama wachangiaji wengine walivyosema, sasa ni muda muafaka wa kuhakikisha kwamba

Serikali pale ambako imejenga vituo vya afya na hospitali tupatiwe watendaji ili tuweze kupata thamani ya fedha ambayo tumeiwekeza kwenye miundombinu ambayo imejengwa na Serikali kwa fedha nyingi za walipakodi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, naunga mkono hoja. Naishukuru Serikali kwa kazi kubwa ambayo inaendelea kuifanya, namshukuru Rais wetu, Wizara na Watendaji wote wa Wizara husika kwa kutuletea bajeti ambayo nadhani itatuvusha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Dkt. Oscar Ishengoma Kikoyo. Nilimtaja Mheshimiwa Benaya Kapinga, Mheshimiwa Michael Costantino Mwakamo, Mheshimiwa Robert Maboto na Mheshimiwa Festo Sanga wajiandae.

**MHE. BENAYA L. KAPINGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Nami niungane na wenzangu kwa dhati kabisa kuipongeza bajeti hii. Ni bajeti ambayo inaenda kuisaidia nchi, inaenda kumkomboa mwananchi wa chini kabisa. Naipongeza Serikali kwa nia ile ya dhati ya kupeleka mikopo kwa vyuo vya kati na pia kuwapeleka wanafunzi kwenye vyuo nao wakasome kwa elimu bure. Suala hili linaoenesha kwa kiasi gani Serikali hii ya Awamu ya Sita ilivyo sikivu. Kwa sababu maoni haya yalitolewa hapa, walishauri Mawaziri hapa, na muda siyo mrefu Waziri wa Fedha amekaa chini, ameshauriana na Mheshimiwa Rais, leo tunaambiwa watoto wataenda kusoma bure, kwa maana ya vyuo hivi, pia na mikopo kwa vyuo hivi vya kati. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kweli suala hili litapunguza kero kubwa kwa Mtanzania wa kawaida na kwa sisi viongozi, Wabunge baadhi yetu tulikuwa tunahangaika kusomesha hawa wanafunzi pale ambapo wamekuja maofisini kulia kwamba hawana ada. Serikali hii ya Awamu ya Sita imeliona hili na sasa inaenda kulifanyia kazi. Naipongeza sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia naendelea kuipongeza Serikali hii kwa kuendelea kutenga fedha nyingi kwenye kilimo. Tunajua

tulianza na shilingi bilioni 294 bajeti ya nyuma kidogo, lakini bajeti ya mwaka 2022 na bajeti hii inaonesha wazi kwamba Serikali hii ina nia juu ya kilimo. Ina nia ya dhati kukitoa kilimo kule kulipokuwa na kukipeleka sehemu nyingine. Safari hii Mheshimiwa Waziri mmekitengea kilimo shilingi bilioni 970. Ni fedha nyingi sana hiyo, itaenda kufanya mambo mengi sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimesikia hapa maoni ya Wabunge wenzangu, nami nina mchango kidogo hapo. Tunapokitoa kilimo kutoka sehemu moja kwenda nyingine kwa kutenga hizi fedha nyingi, tunatarajia uzalishaji mkubwa, tunatarajia wingi wa mazao. Kwa maana ya wingi wa mazao, tunatarajia kuwa na soko zuri. Sasa ziko hofu zinazoonekana hapa kwamba baadhi ya malighafi kutoka nje zimepunguziwa kodi. Kwa kupunguza kodi unasababisha mazao yetu tunayozalisha hapa nayo yashuke bei. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo moja kwa Watanzania wenzangu hapa, zao likiwa halina bei hawalimi. Hawatalima. Hofu iliyopo hapa, tutarudi nyuma; watu wataacha kulima. Tunajua kuna maeneo waliacha kulima kahawa, kuna maeneo waliacha kulima mahindi, kuna maeneo waliacha kulima mbaazi, kuna maeneo watu waliacha kulima hata korosho. Sasa kwa nini ifikie huko wakati nia yetu ni njema, Mheshimiwa Rais amefanya kazi nzuri ya kutafuta hata wawekezaji huko nje wa mazao yetu. Kwa nini tukaribishe hizo bidhaa nyingine kutoka nje kwa kuweka kodi? Hata Mheshimiwa Waziri amesema kwamba kodi imebaki vilevile, mapendekezo yangu ni kwamba ingebidi wewe uongeze ili alizeti yetu ipate soko. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, siyo hivyo tu, jana, juzi na majuzi yaliyotangulia, nimepigiwa simu nyingi sana na wananchi wangu. Sisi kule tunazalisha na tunamshukuru Mungu mwaka huu mvua ilinyesha kiasi cha kutosha. Kwa hiyo, tuna mahindi mengi sana. Mwaka 2022 niliuza swali hapa kwa Waziri Mkuu, na Waziri Mkuu alitoa maelekezo hapa kwamba hatufungi mipaka. Nami sijaona katazo hilo kwamba mazao sasa yasiuzwe nje, lakini sasa hivi ziko hofu huko mitaani, wanasema vibali vya kupeleka mazao nje vimezuiliwa. Hali hii imesababisha mahindi yetu pale jimboni yalikuwa yanauzwa shilingi 75,000 kwa gunia, sasa yanauzwa

shilingi 35,400 mpaka shilingi 40,000. Hii inamkatisha tamaa mkulima. Juzi tu hapa tulikuwa tunaongelea mahindi, yalikuwa yanauzwa shilingi 80,000 mpaka shilingi 90,000, leo hii tuna vuna mahindi... *(Makofi)*

**MHE. EDWIN E. SWALLE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

**MHE. BENAYA L. KAPINGA:** …kwa kusema yasiuzwe nje, mahindi tunaenda kununua shilingi 35,000 na shilingi 40,000/=…

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Benaya, kuna taarifa.

**TAARIFA**

**MHE. EDWIN E. SWALLE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Napenda kumpa taarifa Mheshimiwa Kapinga ambaye anachangia vizuri sana, kwamba tatizo hili kufungwa kwa soko la mahindi nje, limekuwa ni kero kubwa kwa mikoa yote ya Nyanda za Kusini. Hata Jimbo la Lupembe mahindi yameporomoka bei sana. Tunaomba Serikali itoe kauli, hili jambo likoje? Ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Benaya Kapinga, unaipokea taarifa hiyo ya Mheshimiwa Swalle?

**MHE. BENAYA L. KAPINGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naipokea hii taarifa kwa sababu ni kweli. Nami hofu yangu ni kwamba sijasikia kauli ya kukataza mahindi yasipelekwe nje, nilichosikia tuwe na hifadhi ya chakula ndani ya nchi, lakini siyo kwamba tusiuze nje. Sasa naiomba Serikali, Mheshimiwa Waziri wakati anakuja kuhitimisha hapa, atuambie, ni kweli kuna katazo la mahindi kutouzwa nje? Ni kweli lipo hilo katazo? Nasema hivyo kwa sababu wananchi wetu wamelima vizuri, waliitikia vizuri wito na kweli uzalishaji ni mkubwa na wala hatutakuwa na njaa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja nyingine ambayo ningependa kuiongelea hapa ni suala la miradi ambayo tunaendelea kuitekeleza katika nchi yetu. Niipongeze sana Serikali hii imekuwa na jitihada kubwa ya kupeleka fedha nyingi katika miradi kwenye kila eneo la nchi yetu na miradi inaonekana na katika Jimbo

langu nashukuru sana tulikuwa na shida ya barabara tulipata barabara ya kwanza ya kutoka Songea – Mbinga hadi Mbamba Bay na kipindi hiki tumepata mkandarasi anajenga barabara ya kutoka Kitai kwenda Rwanda hadi Litui lakini barabara hii imesimama kwa muda mrefu. Toka mwezi wa pili barabara hii haiendelei hawajengi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, barabara hii inapitisha magari makubwa makubwa ya makaa ya mawe. Magari zaidi ya 3,000 mpaka 4,000 yanapita lakini barabara hii ni ya vumbi. Sasa hivi tayari tumeanza kupokea taarifa za vifo kwa sababu magari yale yanavyopita vumbi jingi wanagongwa watu, zinatokea ajali watu wanavunjika. Kwa kweli inakuwa ni hatari kubwa sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, barabara hii tuliambiwa ingejengwa kwa miezi 12 lakini sasa miezi 12 kuanzia mwezi wa pili, wa tatu, wa nne, wa tano na huu wa sita miezi mitano kazi haiendelei. Kweli tutaenda kukamilisha hii barabara kwa miezi 12? Shida kubwa anayosema mkandarasi Mheshimiwa Waziri hajalipwa. Hajalipwa tangu, ameleta *certificate* huko hajalipwa. Kwa hiyo hawezi kufanya kazi ameleta *certificate* ya kwanza, ya pili, ya tatu. Ombi langu Mheshimiwa Waziri tumlipe huyu mkandarasi ili ile barabara ijengwe ikamilike, itumike kwa sababu ina manufaa makubwa sana kwa nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama makaa ya mawe yote yanayosafirishwa kwenda nje na yanayoletea pato kubwa nchi hii yanatoka pale lakini hayana njia kwa kweli inakuwa shida kubwa sana. Kwa hiyo, niombe sana mkandarasi huyu alipwe ili ile barabara iendelee na ujenzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine niipongeze Serikali kwa mradi huu wa *ETS*. Mradi huu una manufaa makubwa kwa sababu una faida kwa maana ya kwamba sisi kama nchi tunajua bidhaa zetu. Tunajua idadi ya bidhaa tulizonazo na inatuletea faida kubwa. Kwa hiyo, yapo malalamiko kidogo kwamba huyu mkandarasi huyu *charge* zake ziko juu. Kwa hiyo, niombe Waziri kaeni na huyu mkandarasi a-*charge at a minimum price* kiasi kwamba isilete kero kwa wananchi kwa kweli nikupongeze Mheshimiwa Waziri kwa kuendelea na mradi huu una manufaa

makubwa kwa nchi yetu. Hongera sana Mheshimiwa Waziri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niipongeze pia Serikali kwa kazi ile kubwa tuliyoifanya mwaka jana ya sensa na bahati nzuri mwaka huu tumepewa takwimu pale kwamba sasa matokeo ya sensa yako tayari na tumeyaona na kwa kweli ni sensa ya kipekee kwa sababu ina idadi ya watu, ina idadi ya makazi lakini ina idadi ya vituo vya kutolea huduma mbalimbali lakini na mifugo. Kwa kweli wataalamu wanavyotuambia ni sensa ya kipekee. Naipongeza sana Serikali yangu hii ya Awamu ya Sita. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hapo takwimu zile tuzitumie. Tusizitumie kwa idadi ya watu tu. Siku ile pale tumeoneshwa namna huduma zilivyo sambaa. Utakuta *concentration* ya baadhi ya huduma ziko upande mmoja na upande mwingine una watu wengi hauna huduma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, niiombe Serikali kupitia hii sensa tuitumie vizuri, tugawanye mgawanyo wa huduma vizuri. Pale ambapo kuna mapungufu tupeleke huduma siyo kwa sababu tu kwamba labda kuna huduma zigawike kwa idadi kubwa ya watu aah. Hata kwa kuona kwamba zile huduma zingine kwa mfano zahanati au kituo cha afya watu wako sehemu *of course* ni wachache lakini wanapata huduma mbali sana kwa mujibu wa sensa umeonesha pale kwamba kituo cha afya kipo sehemu fulani na sehemu fulani huku hakuna huduma kwa hiyo watu wanatembea zaidi ya kilometa 20. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano Kata yangu ya Ukata idadi ya watu kweli hiyo sifa haina lakini kwa idadi ya umbali na milima ina sifa ya kutosha kabisa. Kwa hiyo, niombe wataalamu wetu wagawanye hizi huduma kwa kutumia hizi takwimu. Wasilenge tu ile kwamba idadi ya watu ni chache. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivyo hivyo mwaka jana na mwaka huu pia nilikuja na ombi la kugawanya Halmashauri ya Wilaya ya Mbinga. Ina watu wa kutosha lakini inawezekana pakawa na kigezo cha kwamba aah, huku ni vijijini na huku ni mijini, mjini kuna *concentration* kubwa ya watu tuka *concentrate* kugawa

halmashauri za mjini. Kijiografia halmashauri hii ni kubwa sana kiasi kwamba mwananchi wa kule chini kuja kupata huduma anatumia muda mrefu, anatumia nauli kubwa, na wengine wanaishia tu kukaa nyumbani na kusema aah, acha tu hilo lipite hivyo lakini anainung'unikia Serikali yake. Kwa hiyo, niombe sana kupitia hii takwimu tugawe hizi huduma vizuri na zitusaidie kwa manufaa ya nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kusema hayo ninaunga mkono bajeti hii kwa 100% kwa sababu inaenda kutusaidia sana sana, sana, ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Benaya Kapinga. Nilimtaja Mheshimiwa Michael Costantino Mwakamo, Mheshimiwa Robert Maboto na Mheshimiwa Festo Sanga wajiandae.

**MHE. MICHAEL C. MWAKAMO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nikushukuru sana kupata nafasi jioni ya leo na ninafikiri hii imekuwa ni tabia yangu ya kupata nafasi jioni. Kwanza kabisa natoa shukrani za dhati kabisa kwa Mheshimiwa Rais kwa namna ambavyo anaitekeleza Ilani ya Chama cha Mapinduzi lakini kubwa kabisa kwa kweli katika siku mbili tatu hizi zilizopita tuna mijadala mikubwa sana inayoendelea huko nje ikihusiana na suala zima la uwekezaji wa bandari. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kusema ukweli kupitia jambo hili nampongeza sana Mheshimiwa Rais kuwa amepata utulivu, ametulia, ameruhusu watu wanafanya mjadala kwa kadiri wanavyopenda na yapo mambo mengine yanazungumzwa yana kera katika nafsi ya kawaida lakini kama kiongozi amenyamaza anawasikiliza kwa hiyo nampongeza sana na tunamwombea afya aendelee kuwasikiliza lakini viongozi wanaomsaidia waendelee kuyapokea yale yanayotolewa kama sehemu ya ushauri na kuyafanyia kazi ili mambo yale yanayokusudiwa na nchi hii yaweze kuendelea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya shukrani hizo nimpongeze Mheshimiwa Waziri. Nimpongeze Mheshimiwa Waziri na wataalamu wake wote pamoja na Naibu Waziri kwa Hotuba

nzuri ya Bajeti ambayo ametuwasilishia na Mpango mzima ambao umekuja mbele yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini katika jambo hili ningeomba nikumbushe jambo moja. Mheshimiwa Waziri utakumbuka mwisho wa Bajeti moja inayowasilishwa na kupitishwa na Bunge ndiyo mwanzo wa maandalizi ya Bajeti nyingine na kila Bajeti ina mapokeo yake kwa wananchi, ina mapokeo yake kwa viongozi ambao tuko humu Bungeni na kila Bajeti ina dhima yake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, dhima ya Bajeti ya mwaka jana ilikuwa ni Kujenga Uchumi Shindani na Viwanda kwa Maendeleo ya Watu. Nakumbuka wakati Mheshimiwa Waziri anawasilisha Bajeti ile kila Mbunge aliyesimama alisema kwa kadiri alivyoweza kwamba ni Bajeti ya pekee na niseme tulikuwa tunasema ni Bajeti ya pekee kwa namna ambavyo aliiwasilisha na kuonesha Serikali inajiandaa kwenye kufunga mikanda na kupunguza matumizi makubwa ya Serikali ili kuelekeza fedha kwenye miradi ya maendeleo na kuwafikishia wananchi maendeleo kwenye maeneo mbalimbali vijijini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa lipo jambo ambalo nafikiri Mheshimiwa Waziri atakapokuja hapa nafikiri atupe kidogo takwimu tumeokoa nini kutokana na msingi wa bajeti ya mwaka jana. Kwenye mazungumzo ya mwaka jana tulisema tutafunga mikanda lakini alisema atabadilisha namna bora ya ununuzi wa magari kwa viongozi mbalimbali katika nchi hii na lengo la kufanya hivyo ilikuwa ni kuhakikisha kwamba tunaokoa baadhi ya fedha na zinakwenda kusaidia miradi mingine ya maendeleo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa kabla sijatoa mchango wangu huku ningemuomba Waziri kwa sababu Watanzania ambao sisi ndiyo wawakilshi wao wanataka kuona ni namna gani tumeokoa kwa sababu ndani ya Bajeti ya mwaka jana kulikuwa na bajeti ya manunuzi ya magari na mambo mengine. Sasa ni kwa kiwango gani tumeweza kunusuru fedha ambazo zinaweza zikafanya kazi kwenye maeneo mengine na ninasema hivyo kwa sababu nimejaribu kusikiliza hotuba sikuweza kuona ni kiasi gani

kimeelekezwa kama sehemu ya kuokoa fedha za mwaka jana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya hapa nirudi kwenye, nijielekeze kwenye mchango wa mwaka huu. Bado mwaka huu pia tumekwenda na dhima ile ile ambayo tulikuwa nayo mwaka jana. Mwaka jana tulikuwa na dhima hiyo ya kujenga Uchumi Shindani na Viwanda kwa Maendeleo ya Watu. Tunapozungumza maendeleo ya watu tunataraji kila mmoja kwenye maeneo ambayo anayaongoza aone baadhi ya mambo yanakwenda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa tuna miradi mingi imetekelezwa, tunampongeza Mheshimiwa Rais na Wanatanzania wanapongeza kwa namna ambavyo miradi ile imetekelezwa. Tumeingia mwaka huu tunatarajia kuwa na uwekezaji mkubwa sana wa bandari. Uwekezaji ambao mimi Mbunge wa Jimbo la Kibaha Vijijini na Wananchi wa Kibaha Vijijini tunapongeza sana Serikali kwa maamuzi mazito ya kuhakikisha kwamba tunaweka mwekezaji pale na kupata fedha za kutosha za kuendesha miradi mbalimbali nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninasema hivi kwa sababu sisi watu wa Jimbo la Kibaha Vijijini tunao pale Mradi wa Bandari Kavu na ukiangalia ili Bandari ya Dar es Salaam iweze kufanya vizuri ni lazima kuwe na maandalizi mazuri kwenye lile eneo la Bandari Kavu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, bandari Kavu ya Kwala inapata bahati inaungana na barabara kubwa ya *Morogoro Road* kwa kupita pale Vigwaza lakini inapitiwa na reli mbili zote muhimu. Sasa nilikuwa na ushauri pale kwamba kwa kuwa ile bandari inategemea kupokea mizigo ya kutokea Dar es Salaam ni vizuri tukahakikisha kwamba tunafanya maandalizi hata wale wananchi walio jirani na bandari ile wanasikia amani kupokea uwekezaji huu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nasema hivyo kwa sababu gani? Nilikuwa natoa michango katika baadhi ya Wizara zilizopita lakini nilizungumzia sana suala zima la migogoro. Bandari ya Kwala ambayo ndiyo inatarajia kuwa sehemu ya upungufu wa mizigo ya

Dar es Salaam wananchi wake bado kuna maeneo vijiji vya jirani vina migogoro na Serikali. Ni vizuri Serikali ikajielekeza kwenye maeneo hayo ikaondoa hiyo migogoro ili wananchi wakawa na amani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wale watu wa Kwala kwenye eneo la Waya wana tatizo la kuambiwa wanatakiwa wahamishwe kwa sababu lile ni shamba la mifugo. Wale watu wa Mwembengozi katika Kata ya Dutumi wanaambiwa eneo ambalo limewekezwa kuwa na Kongani ya Viwanda siyo eneo lililokuwa la vijiji kwa hiyo na wao waondoke wapishe uwekezaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa mimi ningeishauri Serikali tunapokwenda kufanya uwekezaji kwa ajili ya wananchi, tunataka kupata maendeleo kwa ajili ya Watanzania hawa ni vizuri tukamaliza migogoro hii ili wananchi walio maeneo hayo na wao wakawa na amani ili waweze kufaidi michango ya wananchi wengine ambayo inakuja kuendelezwa katika maeneo yale. Hakuna busara itakayokuwa inapendezwa na watu walioko kwenye eneo hilo ikionekana kuna uwekezaji mkubwa unafanywa lakini wao wanaonekana siyo sehemu ya uwekezaji huo. Katika hali ya kawaida binadamu hawa waliokuwa jirani na eneo hilo watakuwa na kinyongo na kinyongo kikimzidi mwanadamu basi anapatwa hasira na hatimaye anaweza akaingia kwenye mgogoro mwingine na anayemsababishia hasira. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wazo langu na ushauri wangu ningeiomba Serikali hasa Wizara ya Ardhi iende ikasaidie kutuliza ile hali kule ili miradi ile itakapokuwa imekuja kuendelezwa katika maeneo yale wananchi wale nao wajisikie amani kwa sababu ni jambo jema kwa sababu linakuja kuleta maendeleo katika maeneo ambayo wanaendeleza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sambamba na hilo katika Jimbo la Kibaha Vijijini nizungumze kidogo kwenye maeneo ya Jimbo la Kibaha Vijijini ni Jimbo ambalo limekaa kimkakati kwa ajili ya miradi mingi ya kimaendeleo ikiwemo ujenzi wa viwanda na ni dhahiri shahiri kwamba unapojenga viwanda katika maeneo mbalimbali unafungua wigo kwa ajili ya uwekezaji na tunapata wawekezaji kutoka ndani na nje ya nchi hii na tunatarajia kwenye

eneo hilo kuwe na kiwango kikubwa cha ukusanyaji wa mapato ya Serikali lakini sasa ukiangalia hali halisi iliyo leo, zipo barabara zinazounganishwa na sehemu ambazo tunatarajia kukusanyia fedha hazijawekewa mikakati mizuri. Ningeishauri Serikali ikafanye utaratibu wa kuweka mikakati ya kimiundombinu ili wawekezaji wanapofika kwenye maeneo yale waweze kuwekeza na miundombinu ikiwa imekaa vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mfano wa maeneo hayo pale Ngimi – Mlandizi kwenye eneo moja la Gisunyara kuna eneo la Kongani ya Viwanda kama ekari 1,000 tayari amekabidhiwa mwekezaji Kamaka na anaendelea vizuri sana na utekelezaji wa mradi ule lakini ukiangalia barabara inayotoka Mlandizi kwenda kwenye eneo hilo la Kamaka yenye urefu kama wa kilometa nane hivi au sita ni mashimo, utaratibu wa kuishughulikia umekuwa mgumu, uendelezaji wa eneo lile unakuwa shida. Ni vizuri Serikali ikaondoa tatizo la barabara ile japo kwa kilometa hizo nane ili mradi tu pale katika lile eneo la viwanda wawekezaji wale waweze kufika kwa urahisi na wawe na moyo wa kuwekeza kwa nguvu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nasema hivi kwa sababu kila muwekezaji anachagua eneo la kuwekeza akitarajia miundombinu itakuwa rafiki kwake na kumrahisisishia uzalishaji wa maeneo hayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile pale katika lile eneo ninalozungumza la Kongani ya Viwanda Kwala linaloenda sambamba na eneo la Bandari Kavu Kwala. Kutoka Kwala kuja kwenye *station* ya Ruvu ambapo hapo ndiyo kuna *station* inaitwa *station* ya kupakia mizigo ya mwendokasi kuna urefu kama wa kilometa tatu, nne hivi lakini barabara ya kukatisha kutoka hapo Kongani ya Viwanda kuja kwenye hiyo *station* hakuna utaratibu wa kuishughulikia. Ni vizuri Serikali ikaenda kufanya miundombinu kwenye eneo lile ili tuweze kuona ni namna gani tunaunganisha kati ya Kongani ya Viwanda na *station* ambayo inatakiwa kupakia mizigo pale kutengenezwe utaratibu wa kuweka daraja katika Mto Ruvu na kutengeneza ile barabara kwa lami ili mizigo iweze kusafirishwa kwa pamoja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine tumesikia kwenye Hotuba ya mwaka huu kwenye mipango ya mwaka huu. Tunakwenda kuongeza shilingi 100 katika kila lita ya mafuta kwa mtumiaji wa Tanzania ambaye ataingia kwenye sheli yoyote Tanzania. Hili ni jambo jema kwa sababu tunaenda kuongeza pato kwa ajili ya miradi. Kuna jambo nilikuwa nataka tuliweke wazi na Mheshimiwa Waziri ikiwezekana atusaidie Wabunge na anapotusaidia Wabunge naye anakuwa amesaidia Watanzania wengine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka jana tulipokuwa na tozo, tozo ilielekezwa ilisema itakwenda kwenye ujenzi wa vituo vya afya, itakwenda kuwenye masuala mazima ya barabara. Kwa hiyo, kila Mbunge alikuwa tayari anasikiliza atapata kiwango gani kwa ajili ya miradi hiyo. Leo hapa Mheshimiwa Waziri amewasilisha tunasema tunapongeza tunaomba tu atakapokuja atuambie ni miradi ya namna gani inayokwenda kutengenezewa mazingira hii ya shilingi 100 ili tukienda Majimboni tutakapokuwa tunawahamasisha wananchi juu ya tozo hii iliyoongezwa watu wawe na matumaini sasa kumbe barabara inakuja kutengenezwa, kumbe zahanati inakuja kutengenezwa, kumbe kituo cha afya kinakuja kutengenezwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tukiiweka katika lugha ya kwamba tumeongeza shilingi 100 kwenye mafuta kila lita ya mafuta ambayo itakwenda kwenye miradi ya kimkakati uhamasishaji wa kwenye jamii waione lakini kama walivyoiona tozo ya mwaka jana unaweza ukawa mgumu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ombi langu kwa Mheshimiwa Waziri najua ni jambo ambalo analiweza na ninajua nia yake njema aje atuambie Wabunge kwa sababu tukitoka hapa tunakwenda kuyavamia Majimbo na kwenda kuwafahamisha wananchi nini Serikali imejipanga kwa ajili ya maendeleo ya nchi yao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo naamini kabisa itakuwa ni nafasi nzuri ya kuwaambia hii shilingi 100 mliyoisikia kwenye lita moja ya mafuta tunaitarajia baada ya kukusanywa Jimbo la Kibaha Vijijini, Jimbo la Makete, Jimbo la Iramba na kwingine

kwingine kokote Tanzania inakwenda kutekeleza kilometa kadhaa za lami, hii inakuwa ni sehemu ya faraja kwao na utaona watakavyoilipa pasipo tatizo kwa sababu ni watu wote wanatarajia kuhakikisha kwamba huwezi kuendesha maendeleo katika eneo lolote kama watu wa maeneo hayo hawajachangia chochote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ombi langu Mheshimiwa Waziri ukija fungua ule mtego uliouweka wa kusema ni miradi ya kimkakati. Nenda kaweke wazi kwamba ni miradi gani inakwenda kukusanyiwa hii shilingi 100 ili twende tukaiseme vizuri kwa Watanzania walio huko. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo langu la mwisho kwa leo nataka kuchangia ni jambo zima la ukamilishaji wa utekelezaji wa miradi. Sote hapa tumesimama tumempongeza Mheshimiwa Rais, tumepongeza Serikali kwa namna ya miradi ilivyotekelezwa kwenye maeneo yetu lakini kuna changamoto kwenye maeneo mbalimbali ambayo miradi hii imeshindwa kumalizwa kwa wakati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, siyo kwamba hili jambo halijulikani. Kamati zote zinazofanya upitiaji wa miradi ikiwemo *LAAC* ambayo mimi ni Mjumbe wake tunatoka na Taarifa ya *CAG* inatoka inaonesha ni kwa namna gani miradi inakwama kwenye utekelezaji lakini kwa nini jambo hili linaendelea? Linaendelea kusema ukweli kasi yetu ya kuwachukulia hatua waharibifu wa fedha za miradi ni ndogo sana na inapokuwa ndogo sasa inajenga uzoefu. Mtu aliyezoea kupiga akiona wa jirani yake kapona halafu baya zaidi hawa wapigaji wana silka ya kuchekana. Anamcheka mwenzie kiko wapi umekaa ofisini huna unachofanya. Sasa ni vizuri tukachukua hatua kwa wanaoharibu miradi ili watu waogope na miradi hii ikamilike. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi kwenye Kamati yetu ya *LAAC* tuna tatizo chungu mzima tumepitia taarifa yetu na Mwenyekiti wetu Mheshimiwa Halima Mdee pale. Kuna mambo mbalimbali yameelezwa na *CAG* kwetu lakini ukiangalia hatua ambazo tunazipendekeza Kamati na hatua ambazo zinachukuliwa hatua ni vitu viwili havifanani kabisa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa kwa hali hii sisi tunaofanya kazi ya kutoa mapendekezo ya hatua za kuchukua tunaonekana kama tunatoa mapendekezo kwa sababu tuna jazba na tunayoyatolea mapendekezo. Ni vizuri Serikali ikachukua hatua kwa maana ya kuleta *discipline* ya kusimamia utekelezaji wa miradi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye halmashauri…

**MWENYEKITI:** Ahsante sana.

**MHE. MICHAEL C. MWAKAMO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Michael Costantino Mwakamo. Nilimtaja Mheshimiwa Robert Maboto.

**MHE. ROBERT C. MABOTO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nikushukuru kwa kupata nafasi hii jioni hii ya leo lakini pia naomba nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa uhai huu alionipa siku hii ya leo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda nimshukuru Mheshimiwa Rais Mama Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kazi kubwa ambayo ameendelea kuifanya katika Majimbo yetu kwa sababu kazi ambayo Rais anaifanya ni kubwa na ambayo sisi Wabunge wake na wananchi wake kwa ujumla tunamuunga mkono kwa kazi kubwa ambayo anaifanya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, muda mrefu sana uliopita wananchi wengi wamekuwa wakihadithiwa shughuli za maendeleo bila kuziona kwa macho lakini Awamu ya Sita inayoongozwa na Mama Samia Suluhu Hassan wananchi wengi wameona shughuli za Serikali zinavyowafikia katika maeneo yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo jambo hili ni la kumpongeza sana Mheshimiwa Rais kwa sababu anafanya kazi kubwa. Kwa hiyo, hata pale ambapo wananchi wanaambiwa kwamba walipe kodi naamini kwamba wanaweza kuwa wanahamasika kwa sababu wanaona vitu vinafanyika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi ni mfanyabiashara na sisi huwa hatuendi darasani kujifunza namna ya kuweza kufanya biashara. Isipokuwa kufanya biashara ni namna tu ya mazingira uliyoyatokea nyumbani kwenu. Wakati mwingine umesoma au hujasoma na ukiona fursa ya kusoma hukuipata lazima uvamie fursa ya biashara. Sasa mimi ni mfanyabiashara, pia tupo wafanyabiashara wengi katika nchi hii ambao tunafanya biashara lakini hatukupata elimu ya biashara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nilikuwa najaribu kufikiria na kuiomba Serikali kwamba hizi kodi nyingi, mtiririko mwingi wa kodi ni kwa nini Serikali isizitengenezee utaratibu wale wafanyabiashara wakawa wanazilipa kwa *installment?* kwa sababu watu wengi wanapokwenda kwa wafanyabiashara, huyu akaenda leo kwaa jambo fulani kwa ajili ya kumwambia mfanyabiashara alipe kodi ya jambo hilo, kesho akaenda mtu mwingine, keshokutwa na mwingine; zile kodi ziko zaidi karibia ya kumi ambazo mfanyabiashara mmoja anatakiwa kuzilipa. Sasa na kwa sababu pia hatuna elimu ya biashara yule mfanyabiashara anakuwa anachanganyikiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa mimi huwa najaribu kufikiri ni kwa nini Serikali haiwezi kuona kwamba zile kodi ambazo zinaweza zikaziunganisha pamoja, kwa nini zisiunganishwe pamoja na wale wafanyabiashara wakaambiwa kuwa wanazilipa kwa wakati? Kuliko hizi ambazo wanaruhusiwa watu wengi kwenda kuwasimamia wafanyabiashara aidha kuwadai vyanzo fulani vya mapato ya Serikali ambavyo na wao wenyewe wao waliotumwa kwenda kuvidai vyanzo vile vya mapato hawajui kuvielezea vizuri kwa wafanyabiashara. Lazima mamlaka ya mapato Tanzania ambayo ndiyo imepewa mamlaka hiyo ya kukusanya kodi inaweza kuwaelewesha watu vizuri wakaelewa namna ya kulipa kodi kwa urahisi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi ninachoamini ni kwamba hawa wafanyabiashara wakieleweshwa vizuri kuhusiana na suala la kodi naamini watalipa vizuri. Serikali ili ikusanye kodi vizuri lazima iwaeleweshe wafanyabiashara wake vizuri waelewe ni kwa nini wanalipa kodi. Bahati nzuri kitu ninachokisema kwa sasa ni kwamba watu wengi hata mimi nimekuwa nikilalamika huko

nyuma kwamba inawezekana nalipa kodi halafu kazi zinazofanywa na Serikali sizioni lakini kwa awamu hii kazi zinaonekana. Kwa hiyo hata namna ya kumwelezea mtu kwamba unalipa kodi ili kifanyike kitu gani inakuwa ni rahisi. Sasa ni kwa nini Serikali isiviunganishe vitu hivi, vyanzo vyake hivi vya mapato kuliko Serikali moja inatengeneza vyanzo vingi karibia 30 halafu unawapa watu tofautitofauti kwenda kuwaelezea hao wafanyabiashara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa wafanyabiashara kwa sababu tulio wengi hatujasomea biashara ila tumeingia tu kwenye biashara kutokana na ukata wa maisha, namna ile unavyokuja kuni-*treat* mimi inakuwa ni vigumu kukuelewa. Lakini kukitengenezwa mfumo mzuri ambao wafanyabiashara hawa wa chini wakaambiwa kiwango chake cha kulipa kodi kwa mwaka ni hiki kikagawika kwa awamu kama nne, ikawa kila baada ya awamu analipa kiasi kile anachokijua yeye Serikali haiwezi kupata usumbufu na wala haiwezi kuhangaishana na wafanyabiashara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, na hata wakati nyingine mnapoona wafanyabiashara saa zingine wamegoma, wanagoma kwa sababu ya kuchanganyikiwa, yaani vitu vinakuwa vingi ambavyo vinaingia vichwani mwao na namna ya kuweza kulifanyia kazi inashindikana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri wa Fedha ambaye wewe ni daktari wa fedha ni vizuri utusaidie sisi, uwasaidie walipa kodi wako ambao wewe unaamini kwamba unatoza kodi kwa watu ambao hawajasomea biashara lakini ndio wanaokulipa kodi. Sasa wewe lazima utumie namna yoyote inayoweza kuwezekana ili wale wafanyabiashara waweze kulipa kodi katika utaratibu ambao ni mzuri na ni nafuu na ambao ni rafiki. Bila hivyo wafanyabiashara wale bado wataendelea kukuhangaisha na bado watu wataendelea kukwepa kodi. Lakini kumbe kitu kikubwa kilichopo ni kwamba wakishaeleweshwa vizuri wakajua vizuri, na bahati nzuri sasa wanaona shughuli za maendeleo zinavyofanyika katika nchi yao kwa hiyo kigugumizi kinakwisha, na watu watakuwa wanaambiwa kulipa na wanalipa katika utaratibu ambao nil aini kabisa bila kuhangaika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo jambo hilo nilikuwa naliomba sana, kwamba Mheshimiwa Waziri wa Fedha ambaye ni mtaalam wa fedha atusaidie jambo hilo. Pia na juzi niliona hapa mchangiaji mmoja anasema kwamba mimi na taasisi yangu labla kampuni yangu nina miaka 20 nayo, halafu leo nikiambiwa kwenda kuisimamia ile taasisi yangu au kuisajili kwa ajili ya kufanya biashara labda ya *microfinance* naambiwa kwamba mimi siwezi kuwa kwenye bodi ya ma-*director* kwa sababu elimu yangu mimi haikidhi vigezo hivyo. Wakati huo huo taasisi hiyo nimeanza zaidi ya miaka 20. Sasa kwa akili za kawaida hata ukijiuliza unaona haiwezekani. Uzoefu nao una-*matter* katika kazi. Ingekuwa tu kusoma peke yake ndiko kunakosababisha kila jambo liweze kufanyika vizuri mimi naamini saa nyingine tusingekuwepo hapa tunahangaika na mambo mengi ambayo saa zingine yamekwenda na saa zingine hayakwenda vizuri. Kwa hiyo Mheshimiwa Waziri hili nalo ni jambo ambalo unapashwa kuliangalia vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Jambo lingine nilitaka kusema tu kwamba wananchi wangu wale wa Kata ya Nyatwali wameshafanyiwa tathmini ya maendelezo yao kwenye kata yao ile ya Nyatwali. Na kwa vyovyote vile itakavyokuwa muda mfupi uliobaki watahama katika eneo lile. Sasa na kwa sababu wananchi wetu wale na unawajua wananchi walio wengi ni wakulima na wafugaji; ni ombi langu kwa Serikali kwamba ni vizuri yake malipo yao kwenye bajeti hii wakalipwa mapema ili wakajipange mapema kwa ajili ya kilimo katika maeneo mengine. Wakilipwa nje ya muda ule ambao unaendana na muda wa kilimo itawatesa kwa sababu pale walipo hawaruhusiwi kulima, pale walipo hawaruhusiwi kuendeleza chochote. Pia yule anayetakiwa kuwalipa hajawalipa, halafu anawaambia bado wako pale pale. Sasa hao watu wataishi katika mazingira gani?

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi naamini kwamba kwenye bajeti hii wale wananchi wetu watalipwa fedha zao mapema na wataondoka kwa wakati ili wakaanze maisha yao huko wanakokwenda. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ni lile jambo la kifuta machozi. Wananchi wetu wale maskini, wakulima, tena wakulima

wa heka moja moja ya chakula na chakula chenyewe wanachokilima hata hakiwatoshi kukila kwa mwaka. Halafu chakula hicho hicho kimekuja kimeliwa na tembo halafu kulipwa fidia analipwa laki moja, halafu laki moja yenyewe anaisubiria baada ya miaka miwili, mitatu. Kwa kweli watu wale wanaumia kwa kiasi kikubwa. Ni ombi langu pia kwa Serikali kwamba jambo hili ni vizuri Serikali ikalifanyia mkakati mpya kuhakikisha kwamba kilimo cha mwaka kile ambacho hao wananchi wamekilima, mazao yao yamelishwa na tembo, muda huo huo mwaka ukiisha wawe wamepewa fedha zile ili na wao waende watafute chakula cha kununua. Hicho chakula ambacho wenzetu wanasema kwao gunia limeshuka mpaka 35,000 mikoa ya kusini. Sisi Mara gunia la mahindi ni 120,000 au 100,000.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakipata fedha hizo mapema wataenda huko ambako chakula kinauzwa 40,000 gunia wakanunue, halafu kitawasaidia, kuliko ile sasa kwamba fedha za mwaka huu atalipwa baada ya miaka miwili au miaka mitatu. Mwananchi huyu anakuwa ameshaumia kwa kiasi kikubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ni kwamba Halmashauri yangu ya Mji wa Bunda ilitoa eneo pale kwa ajili ya ujenzi wa Ofisi za *TANAPA* kanda ya magharibi; na halmashauri ile ilishatoa eneo lipo kwa muda sasa. Ni imani yetu kwamba kwa sababu tunapisha ile Kata nzima ya Nywatali ni vizuri pia Serikali na yenyewe ikahakikisha kwamba ofisi ile iliyokuwa imetengewa pale fedha za kuanza ujenzi ni vizuri ikajengwa kwa wakati kwa sababu ndio itakayokuwa inasimamia mambo hayo ya Mbuga ya Serengeti na mambo mengine. Malalamiko mengi ya wananchi wetu wakati mwingine yataishia hapo kuliko vile ambavyo tunakuwa tunapata wakati mgumu wa namna ya kupata suluhisho la matatizo hayo ambayo tunakuwa tumeyapata katika maeneo hayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ombi langu ni kusema kwamba fedha zile zitolewe mapema ili kwamba Ofisi ile ya *TANAPA* Kanda ya Magharibi ziweze kujengwa kwa wakati ili ziweze kusaidia katika Halmashauri yetu ya Mji wa Bunda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine ni suala la fedha za miradi ya barabara. Niishukuru Serikali kwa sababu imeendelea kufanya kazi kubwa lakini bado sisi kwetu Bunda pale eneo la barabara za mitaa bado tatizo lipo ni kubwa.

Ombi langu ni kuiomba Serikali iendelee kutoa fedha kwenye *TARURA* ili kwamba uboreshwaji wa barabara zile za mitaa uweze kukaa vizuri; na kwa sababu maeneo hayo muda mwingi yamekuwa hayapitiki kwa muda mrefu lakini kwa sasa ramani imeanza kuonekana. Ombi langu ni kwa Serikali kuhakikisha kwamba wanawapa fedha za kutosha ili kwamba barabara zetu zile ziweze kulimika vizuri na wananchi wetu waweze kupita katika maeneo yao kwa wakati wote wa masika na kiangazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kuyasema hayo nakushukuru kwa kupata nafasi; ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Robert Maboto nilimtaja Mheshimiwa Festo Sanga, tutamalizia na Mheshimiwa Iddi Kasim Iddi.

**MHE. FESTO R. SANGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi niweze kuchangia kwenye hoja iliyoko mezani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la kwanza ninaunga hoja mkono asilimia 100 kabisa na kwa upekee kabisa nipende kumpongeza sana Mheshimiwa Rais kwa kazi kubwa ambayo anaifanya. Niseme wazi kabisa kwamba Mheshimiwa Rais kazi anayoifanya ni kubwa kwa kiwango ambacho tumetekeleza bajeti kwa Wizara zote kwa zaidi ya asilimia 50. Hii inaonyesha kwamba Wizara ya Fedha pia na Mamlaka ya Mapato Tanzania wanafanya makusanyo vizuri. Tuwapongeze sana; kwa sababu sehemu kubwa ya miradi ya maendeleo inatekelezwa vizuri sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili nina hoja zangu mbili. Hoja ya kwanza ni kuhusiana na suala la *unclaimed financial asset*. Nilizungumza wakati ule na niliahidiwa kwamba litakuja kutolewa ufafanuzi mwaka huu; na niko hapa nikisubiria ufafanuzi kuhusu *unclaimed financial assets* kwenye Taifa letu. Hawajawahi

kuzungumza popote ambapo hizi fedha ambazo zimekuwa *unclaimed* kwenye benki, kwenye mitandao ya simu na hata kwenye maliasili, kwenye vituo vya polisi. Ukisoma kwenye ripoti ya *CAG* anazungumzia bodaboda zipo kwenye vituo vya polisi zina miaka mitatu, minne zinauzwa hadi kwa shilingi 20,000 kwenye ripoti ya *CAG*. Kwa hiyo ni vyema Mheshimiwa Waziri wakatoa ufafanuzi fedha hizi zinaenda wapi, ambazo ni mali ya Watanzania na walituahidi kwamba watakwenda kulifanyia kazi kupitia Ofisi ya *PST*. Kwa hiyo ninaomba majibu Mheshimiwa Waziri wa Fedha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili nipende kupongeza, tulishauri kwenye Bunge kuhusu kupunguza msururu wa watendaji wa Serikali kuingia kwenye maduka ya Watanzania na wafanyabiashara wanaonzisha biashara zao. Tulizungumza hapa kwamba mtu anaanzisha biashara lakini kuanzisha kwake biashara ni kama anafanya kitu haramu kwa sababu akiamka asubuhi watu wa *fire* wameingia, watu wa *NEMC* wameingia, watu wa OSHA wameingia, watu wa *TRA* wameingia, watu wa *service levy* wameingia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tukashauri hapa Serikali itafute namna moja ya ku-*centralize* hii iwe ni moja tu. Mtu alipe tu hiyo Serikalini kwa mwezi kugawana. Na naona kuna mawazo yako kwenye bajeti hii umeyatoa; nikupongeze sana, kwamba kwa hili unakwenda kuilinda sekta binafsi, na kwamba ni nia ya dhati ya Mheshimiwa Rais kuona sekta binafsi nchini inalindwa ili mfanyabiashara apate muda wa kuhudumia zaidi wateja kuliko kuhudumia watumishi wa Serikali; na kwa kweli mnaenda kuandika historia. Ule mfumo, tulisema hata waleti mwanaume kujaa waleti mfukoni vimejaa vitambulisho sio jambo zuri tuwe na kitambulisho kimoja ambacho kinaweza kikasaidia. Kwa hiyo niseme hili unaloenda kulifanya unaenda kufanya jambo la kizalendo kabisa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ni kuzuia kamata kamata. waheshimiwa Wabunge walipiga kelele hapa wakati *NEMC* wamefungia na maeneo tofauti tofauti. Bado ni mwendelezo wa Mheshimiwa Rais kulea sekta binafsi kwenda kuzuia sasa kamata kamata tu-*deal* na muhusika ambaye

amefanya hujuma yoyote ile ndiye tuhangaike naye. Hii itasaidia hata Kariakoo na maeneo mengine ya masoko na hata sekta ya biashara kukua ili tuli-*deal* na hawa wahusika ambao sioy kuliko ku-*deal* na biashara ambayo tunakuwa tunasababisha Serikali inakosa mapato. Kwa hiyo mimi nipongeze kwenye hayo mambo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa jambo langu na agenda yangu ipo kwenye jambo moja; na hili ndio nililotumwa na Makete hili wamenituma watanzania, hili wamenituma wakulima wa ngano kwenye Taifa letu. Mheshimiwa Waziri kwenye hotuba yako ukurasa namba 149 unasema una mpango wa kutoa unafuu wa ushuru wa forodha kwa uratibu wa *duty remission* kwa kiwango cha asilimia 10 badala ya 35 kwa mwaka mmoja kwenye ngano inayotambulika kwa *HS Codes* hizo hapo, lengo lake ni kupunguza gharama za maisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikuombe Mheshimiwa Waziri inawezekana una nia ya dhati kabisa lakini nia yako ya dhati inawezekana inaenda tofauti na mpango wa Mheshimiwa Rais, tofauti na Waziri wa Kilimo, tofauti na kile kinachofanyika *field*. Mimi ni Mbunge wa Makete, Mheshimiwa Rais ametupa ngano tani 80 kwa ajili ya wananchi wetu na amegawa bure Makate na inawezekana na mikoa mingine kama Arusha ameigawa bure. Lengo la Mheshimiwa Rais ni kumsaidia mkulima na ngano iweze kuoteshwa kwa wingi nchini ili soko la ndani la ngano liweze kufanya vizuri. Unapokuja na mpango huu Mheshimiwa Waziri unataka kutuambia ni kama mnataka kumuhujumu mkulima. Kwa nini? ukisoma ukurasa wa 257 kwenye *hansard* za Bunge za Waziri wa Kilimo Mheshimiwa Hussein Mohamed Bashe anazungumza naomba Wabunge mnisikilize.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Bashe anasema hivi; "Mheshimiwa Spika, niongelee hii *issue* ya ngano na alizeti. Sisi tuna-*import* ngano tani milioni moja kwa mwaka. Ili tujitosheleze ngano tunahitaji ngano tani 50,000 za mbegu za kwenda kumpa mkulima alime. Tumechukua hatua gani?" Akaendelea; "Mheshimiwa Spika, nataka niseme mbele ya Bunge lako tukufu niseme mbele ya Wabunge na mbele ya Watanzania kwa uwezo wa Mwenyezi Mungu 2025/2026 tunaendelea kuzalisha ngano. Mwenye mamlaka ya kuwapa cheti cha ku-*import* ngano ndani

ya nchi ni Waziri wa Kilimo. Kama nitakuwa kwenye kiti viwanda vitageuka chuma chakavu, hawataingiza hata kilo moja kama hawajanunua ngano ya Watanzania." *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Bashe anazidi kuongea, anasema; "Mheshimiwa Spika, Watanzania hawatakufa kwa kukosa ngano, haiwezekani unambembeleza. Mmefanya nao *trial* tumewapa mbegu wao wenyewe kwenye maabara zao wamesema inafaa halafu wakati wa ku-*sign MOU* wanasema hatutaki. *Over my dead body* wata-*sign* mkataba, wasipo-*sign* hatutawapa *phyto sanitary* ya kuingiza ngano, watajua watakachokifanya na viwanda vyao". Huyu ni Waziri wa Kilimo analizungumza hilo, huyu ndiye aliyesambaza mbegu kwa wakulima, huyu ndiye aliyetuma hasa ikazalishe mbegu, huyu ndiye anakaa na Mheshimiwa Rais kwenye sekta ya kilimo, wanapanga ili ngano izalishwe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo kila mwananchi wa Makete amezalisha ngano leo unakwenda kumwambia huyu mtu aingize ngano kwa ushuru wa kutoka 35 kuja kwenye 10 percent, hii ni *sabotage* kwa mkulima wetu, hii ni *sabotage* kwa wana-Makete, hii ni *sabotage* kwa mwananchi aliyeko Mbulu. Hii ni Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania; mnazungumza jambo moja lakini kwa lugha tofauti. Tukimruhusu mfanyabiashara aingize ngano Mheshimiwa Waziri Bashe anasema hawa watu wamemkataa kwenye *MOU* manake unataka utuambie amezunguka nyuma, wamekutana na watumishi wako wa Wizara wamemwambia shusha kutoka asilimia *35 percent* uje kwenye asilimia *10 percent*. Kufanya hivyo ili Waziri wa Kilimo aendelee kubaki katika msisitizo wa kwamba hawa wanabaki na viwanda vyao kumbe wametengeneza lango lingine la kuingiza ngano kwa kupitia kushusha ushuru.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikuombe Mheshimiwa Waziri Mwigulu una heshima kubwa kwenye Taifa letu, ninakuomba sana achana na hii biashara. Tumepita kwenye *covid* tukiwa kwenye asilimia 35, tumepita kwenye mtikisiko wa uchumi tukiwa na asilimia 35, unaendaje saa hizi angalau hali iweze kupoa tunaanza kushusha kwenye asilimia 10? Tunaua viwanda vya ndani. Mimi nitaenda kuwaambia nini wananchi wa Makete,

Matamba na Ikuo ambao wameacha mazao yote nimewaambia limeni ngano? Leo hii mnaenda kuwaambia wafanyabiashara washushe ngano waingize kwa asilimia asilimi 10 waache 35.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimuombe Mheshimiwa Waziri kwa kushirikiana na Waziri wa Viwanda na Biashara; kweli inawezekana tuna upungufu wa ngano tafuteni utaratibu wa kuweka kibali maalum kwa ajili ya kuingiza huyo mtu lakini si kwa asilimia hii mliyoitaja, tunaenda kuua wakulima wetu. Yaani Mheshimiwa Anthony Mtaka pale Njombe amepambana kweli kuhakikisha ngano inaota. Mimi nimepambana kweli kuona ngano inaota. Mkuu wa Wilaya ya Makete Mheshimiwa Juma Sweda amepambana kweli kuona ngano inaota. Mkurugenzi wangu Ndugu William Makufwe amepambana kweli kuhakikisha ngano inaota. Na hata juzi Tume ya Mipango imekuja tumeanza kupima vijiji 41 na kuwapa hati kwa sababu ya zao la ngano. Leo tunakuja kusomewa hapa mfanyabiashara anaongezewa dirisha la kuingiza ngano nyingi ili ngano ya ndani izame. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninamuomba sana Mheshimiwa Waziri, hili ni jambo la muhimu sana kwenye Taifa letu. Waziri wa Viwanda na Biashara, Waziri wa Kilimo kaeni chini tusaidieni. Mheshimiwa Waziri najua una nia njema ninajua una nia njema lakini nia yako njema inaenda kuzamisha watoto wako wa ndani, unaenda kuzamisha familia yako Mheshimiwa Waziri. Nikuombe Mheshimiwa Waziri wa Fedha nikuombe…

**WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Taarifa.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri anakuomba tu huyo utakuja kumjibu.

**MHE. FESTO R. SANGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri nikuombe unafanya vizuri sana kwenye Wizara yako, miradi iko kedekede umetupelekea fedha huku hatujawahi kuziona fedha nyingi kwa kiwango hicho…

**MHE COSATO D. CHUMI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Taarifa.

**MHE. FESTO R. SANGA:** …hili kosa la kuruhusu ngano iingie lisiende kufanyika …

**MWENYEKITI:** Kuna taarifa Mheshimiwa Festo.

**MHE. FESTO R. SANGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, unanizamisha mimi, unazamisha Wabunge, unazamisha Wabunge ambao kila siku…

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Festo kuna taarifa yako, Mheshimiwa Cosato Chumi.

**TAARIFA**

**MHE. COSATO D. CHUMI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kumpa taarifa mzungumzaji kwamba, mojawapo ya hatua ambazo tunatakiwa kuzifanya ni kuhakikisha kwamba tunapunguza kuagiza bidhaa muhimu kutoka nje ili kujijengea uwezo wa ndani. Sasa basi analolisema la kibali ni muhimu, tumefanya hivyo katika sukari matokeo yake tulikuwa tunaagiza tani 300,000 leo hii tunaagiza tani 15,000 na viwanda ndani vimeshamiri na wananchi wetu wanapata ajira. Kwa hiyo anachokitetea siyo kwa wananchi tu wa Njombe, wa Makete, ni wa Tanzania nzima na Taifa kwa ujumla. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Festo, unaipokea hiyo taarifa?

**MHE. FESTO R. SANGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naipokea hii taarifa, kwa sababu tunaenda kulinda viwanda vya ndani, tunaenda kulinda wakulima wetu napokea kabisa. Nimwombe sana Mheshimiwa Waziri, aachane na hii biashara, huu ni mchezo, wamemzunguka Mheshimiwa Bashe kule kwenye *MoU,* mbegu wameenda nayo maabara wao wenyewe, wamepima wakasema Waziri hapa tutaingia pamoja kwenye hii. Walivyofika kwenye kusaini mezani wakamgeuka kumbe wameona dirisha nyuma ya Waziri, wamepita huko, wameenda kushusha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimwombe Mheshimiwa Waziri aachane na hii biashara, amsaidie Mheshimiwa Bashe, awasaidie

wakulima wa Makete, Njombe, Iramba, Kisasatu na awasaidie wakulima wa kila eneo la Taifa letu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, hoja yangu ni ngano na nitakufa nayo, kwa sababu hizi ndiyo kura za CCM, hizi ndiyo kura za Mheshimiwa Rais, hizi ndiyo kura za Taifa langu, lazima niwapiganie, ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Festo Sanga, naamini kabisa Mheshimiwa Waziri atatoa ufafanuzi mzuri na naamini utaukubali.

Tunamalizia na Mheshimiwa Idd Kassim Idd.

**MHE. IDD K. IDD:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa fursa ya kuchangia Bajeti Kuu ya Serikali. Kwanza kabisa, nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunijalia leo kupata nafasi ya kuchangia bajeti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimshukuru sana Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kazi kubwa anayoendelea kuifanya. Pia nimshukuru sana Mheshimiwa Waziri kaka yangu Mwigulu Nchemba kwa kazi kubwa anayoendelea kuifanya pamoja na Naibu wake Waziri naye ameendelea kufanya kazi nzuri sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo nataka kujikita kwenye mambo machache sana. Moja, niendelee kuipongeza sana Serikali kwa bajeti hii ambayo imeileta hapa mezani. Ni bajeti nzuri, ni ambayo kama itaenda kutekelezeka kwa asilimia mia moja, basi italeta matunda makubwa sana kwenye maeneo yetu. Nimeona Wizara ya Nishati imeweza kuweka nguvu kubwa katika kuhakikisha kwamba inapeleka umeme kwenye maeneo yetu. Sasa niombe sana Mheshimiwa Waziri wa Fedha aweze kutoa *support* kubwa sana kuhakikisha kwamba anapeleka fedha kuwalipa wakandarasi ili waweze sasa kuona namna gani wanaweza kuendelea na kazi ili ifanyike haraka sana ya kupeleka umeme kwenye maeneo ya vijiji vyetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ifanyike hivyo hivyo kwenye barabara na niombe sana Waziri wa Ujenzi, Jimbo la Msalala lina barabara moja ambayo tayari inafadhiliwa na Mgodi wa *Barrick* na niwapongeze sana Barrick kwa kuendelea kuonyesha jitihada za kuhakikisha kwamba wanatoa ushirikiano kwa Serikali ili kuona namna ya kujenga barabara hiyo. Niombe sana kwa Waziri wa Ujenzi, waone namna gani ambayo wanaweza wakapeleka mchakato huu haraka ili ikiwezekana basi mwezi unaokuja barabara hii ianze kujengwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, barabara hii imekuwa ni barabara ambayo ina kero kubwa sana. Watu wanapata ajali nyingi, magari yanadondoka na hasa magari yanayobeba mizigo mikubwa. Kwa hiyo, nimwombe sana Mheshimiwa Waziri pamoja na Waziri wa Ujenzi waweze kuharakisha mchakato huu ili barabara hii ianze kujengwa, kwa sababu fedha zipo kila kitu kipo tunasubiri tu mchakato ukamilike ili barabara ianze kujengwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivyo hivyo kwenye barabara zingine ambazo zimetajwa kwenye Ilani ya Chama Cha Mapinduzi, basi ni vyema pia Mheshimiwa Waziri baada ya hapo kwenye bajeti ya mwaka unaoanza akapeleka fedha mapema ili barabara hizi ziweze kujengwa, zirahisishe kujenga uchumi wa maeneo yetu hasa katika Jimbo la Msalala.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka nizungumzie mambo mawili. Jambo la kwanza nataka nizungumzie habari ya *oil* ambayo imekuwa ni changamoto kubwa kwenye nchi yetu hii ya Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama unavyofahamu Mheshimiwa Waziri wa Nishati, kaka yangu January Makamba amekuwa akizungumzia sana habari ya mafuta na pia akaacha kuzungumzia habari ya *oil* ambayo pia inatumika katika maeneo mengi sana. Sisi tunatumia kwa ajili ya magari na vyombo vya moto vyote. Sasa kumekuwa na changamoto, nakubaliana kabisa na Mheshimiwa Waziri kwamba makubaliano ambayo huwa wanaaingia pamoja na Nchi za Afrika Mashariki katika kuweka ushuru wa malighafi ya *oil* kuingiza nchini kwa kiwango

cha asilimia 10. Hata hivyo, niendelee kuomba sana, makubaliano ambayo huwa wanaingia huko kwenye Nchi za Afrika, wenzetu wanakuja kurekebisha kodi mbalimbali za ndani kuhakikisha kwamba wanajenga mazingira ya uwekezaji mzuri kwenye maeneo hayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo nimwombe Mheshimiwa Waziri kwenye suala zima la *oil,* aende akafanye mabadiliko, afute *VAT* na apunguze kodi mbalimbali zitakazowezesha wananchi kuingiza malighafi ya *oil* ili waweze kuwekeza viwanda vingi na tuweze kuzalisha *oil* hapa hapa nchini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwani utaona kabisa kwamba kwa sasa hali ilivyo ni rahisi kununua *oil* katika nchi zingine, nchi za Jirani kwa sababu *oil* ni bei rahisi kuliko kununua *oil* hapa nchini hii. Hii inasababishwa na kuweka kodi mbalimbali kwenye malighafi ambayo inakuja hapa kwenye viwanda vyetu ambayo itazalisha *oil* hiyo. Kwa hiyo nimwombe sana Mheshimiwa Waziri, aende akakae, aangalie kama inawezekana wapunguze hiyo gharama ya kuingiza/kutoza malighafi ambazo zinakuja kuzalisha *oil* kwenye viwanda vyetu hivi vya ndani. Hii itasaidia kuhakikisha kwamba wananchi sasa wanaenda kuwekeza kwenye sekta ya kutengeneza *oil.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nirudi kwenye suala zima la Jimboni ambalo wananchi wa Msalala wamenituma na hasa kwenye Sekta ya Madini. Mheshimiwa Waziri hapa naomba anisikilize vizuri sana, kuna jambo linaendelea la asilimia mbili kwa wachimbaji wadogo wadogo. Niombe sana, asilimia mbili hii nimehudhuria semina mbalimbali za watu wa Waziri wa *TRA,* wakitoa ufafanuzi juu ya asilimia mbili kwa wachimbaji. Mheshimiwa Waziri ameweka asilimia mbili kuanzia mchimbaji yeyote yule mwenye mapato ya kuanzia *zero* mpaka milioni mia ndiyo atayehusika na kulipa asilimia mbili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka nimwambie Mheshimiwa Waziri, kama hataweka mfumo mzuri, wachimbaji wadogo wadogo mitaji yao inaanzia milioni mia na kuendelea juu. Sasa niombe kama tutaenda kupitisha hii asilimia mbili kwa wachimbaji wadogo wadogo, basi tuongeze kutoka kipato cha asilimia *zero*

kwenda mpaka bilioni tano kwa sababu uchimbaji wa madini si kama biashara nyingine. Uchimbaji unaanzia kwenye mtaji mdogo sana, ni milioni mia moja kwenda juu. Kwa hiyo Waziri akisema kwamba mtu atakayechajiwa asilimia mbili ni kuanzia *zero* mpaka mia moja, maana analenga wale wachimbaji wadogo wadogo akinamama ambao wanaenda kuokota mifuko michache na kwenda kuchoma kupata gramu mbili, tatu kwa ajili ya kuendesha maisha yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo nimwombe sana Mheshimiwa Waziri, hii asilimia mbili haiendi kumsaidia mchimbaji mdogo mdogo isipokuwa waje na mfumo, waweke utaratibu mzuri wa kwenda kuona ni namna gani wanaweza kuwajengea mfumo mzuri wachimbaji wadogo wadogo ili waweze kutunza hesabu zao na waweke mfumo mzuri kuona namna gani wanaweza kukubaliana na matumizi ambayo yanafanyika kwenye maeneo yale, kwa sababu kwenye maeneo ya wachimbaji wadogo wadogo ni nadra sana kumkuta mama ambaye anauza maji ana risiti, ni nadra sana kumkuta mtu ambaye anauza matimba ya kufunga mle ndani ana risiti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nashauri *TRA* na Mheshimiwa Waziri wa Fedha wakae na timu yake waangalie ni namna gani sasa wanaweza kuweka mfumo mzuri utakaomwezesha mchimbaji mdogo anapokuja kufunga hesabu zake kwa mwaka, baadhi ya matumizi wayakubali. Kwa hiyo wafanye *research,* waje na utaratibu huo, lakini wakisema kwamba mchimbaji mdogo mdogo alipe asilimia mbili, hii asilimia mbili haiendi kumgusa mchimbaji mdogo mdogo, isipokuwa inaenda kumgusa mama mnyonge kabisa ambaye anaenda kufanya sisi tunaita ukwale, mifuko miwili, mitatu, anaenda kusaga, anapata pointi mbili, gramu mbili ndiyo hii sheria ambayo wameileta ya asilimia mbili inaenda kum–*favor*, lakini kwa mchimbaji mwingine yeyote yule ile asilimia mbili haiendi kum–*favor* kabisa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama hawataweka utaratibu wa namna gani wanaweza kukubaliana na matumizi ili mchimbaji huyu aweze kuweka gharama zake vizuri, itakuwa ni changamoto sana. Kwa hiyo nimwombe Mheshimiwa Waziri, hii asilimia mbili ikiwezekana waende kuipitia upya, waiache kwanza, tukae vizuri

kuona namna gani tunajadiliana, ni yupi atakayeweza kunufaika na hii asilimia mbili. Kama mapato yatakuwa ni asilimia *zero* mpaka bilioni tano tunakubaliana na hii asilimia mbili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri ailete na sisi tutaipitisha, lakini kama ni mapato kuanzia asilimia *zero* mpaka milioni mia moja, biashara ya dhahabu siyo biashara ya vitumbua. Biashara ya dhahabu mtaji wake duara moja tu gharama yake ni milioni mia tano mpaka bilioni moja. Sasa Waziri akisema asilimia asilimia *zero* mpaka mia moja, maana yake bado ni changamoto na wachimbaji watakuwa hawajaelewa chochote kile. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine, nizungumzie habari ya leseni. Nimpongeze sana Mheshimiwa Waziri wa Madini, Mheshimiwa Doto Biteko, anafanya kazi kubwa sana. Pia nimpongeze sana Mheshimiwa Rais, leo hii utaona wachimbaji walikuwa kupata leseni ni kazi sana, lakini ukisoma Ripoti ya Wizara ya Madini, utaona kabisa wamegawa leseni nyingi kwa wachimbaji. Leo hii tuna uhuru wa kumiliki leseni kwenye maeneo yetu, lakini bado kuna changamoto hapo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika baadhi ya maeneo ya wachimbaji wadogo wadogo, kumekuwa na wawekezaji ambao wanatoka nje kuja kuchukua leseni hizi kubwa kwa maana ya *prospecting license* na leseni hizi hawaziendelezi. Wanapokuja kuchukua maeneo haya, wanatoka hapo baada ya kupatiwa leseni ya *prospecting license* wanaenda na *documents* zetu kwenda nje kutafuta mikopo na mikopo ile hairudi kuja kuendeleza leseni zile. Matokeo yake wanachukua zile fedha wanaenda kufanya mambo mengine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niombe, kuna wachimbaji ambao tayari wapo kwenye maeneo yale, kwangu ukiangalia kuna maeneo ya Nyangalata, kuna maeneo ya Segese na maeneo mengine yote, kuna wachimba wengi ambao wanahitaji kuchimba na wamewekeza kwenye leseni zile za *prospecting license,* lakini bado hawajapatiwa leseni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimwombe Mheshimiwa Waziri aje na mfumo kuhakikisha kwamba wale ambao wanapatiwa leseni

za *prospecting license* hawazifanyii kazi, utaratibu ufanyike ikiwezekana kuwafuta ili wapewe wachimbaji wadogo wadogo waweze kufanya kazi, kwani wachimbaji wadogo wadogo kwa sasa ndiyo wanaochangia mapato makubwa kwenye Sekta hii ya Madini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimwombe sana Mheshimiwa Waziri Biteko anapokuja ku-*wind up* hapa aje na kauli atueleze je, ni vipi sisi wachimbaji wadogo wadogo ambao tuko kwenye maeneo ambayo yameshikiliwa na leseni kubwa na leseni kubwa hizo hazifanyi kazi, namna gani anaenda kuzifuta ili wachimbaji wadogo wadogo tuweze kunufaika na maeneo hayo? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kusema hayo, nakushukuru sana na naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Iddi Kassim Iddi ahsante sana. Waheshimiwa Wabunge kuna jina moja nililiruka na mwenyewe yumo humu ndani, kwa hiyo huyo ni Mheshimiwa Moshi Selemani Kakoso, atakuwa ni mchangiaji wetu wa mwisho, karibu sana Mheshimiwa Moshi.

**MHE. MOSHI S. KAKOSO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nishukuru sana kwa kunipa nafasi ya kuwa mchangiaji wa mwisho. Awali niipongeze sana Serikali kwa kazi kubwa ambayo wanaifanya hasa ya kupeleka miradi ya maendeleo, hasa kwenye miradi mikubwa ambayo imeanza kutekelezwa na inaonekana mbele ya nchi yetu. Miradi hiyo hiyo mikubwa ni kama ujenzi wa reli, barabara, miradi ya umeme, miradi ya maji, miradi ya elimu ambayo kimsingi imekuja kuwa na mafanikio makubwa sana mbele ya nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninalo eneo moja ambalo ningependa kulichangia kwa kina kuishauri Serikali. Bahati mbaya tu leo hata wasaidizi wa Waziri ambao wanaweza wakachukua mawazo ya Wabunge hawapo kabisa, yupo Waziri na Naibu Waziri, lakini yapo mambo ya msingi ambayo tunaweza tukalisaidia Taifa letu ili liweze kuepukana na kodi tunazozichukua kwa wananchi za kila mwaka kwenye eneo la mafuta na eneo la bia na kwenye maeneo mengine madogo madogo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka jana niliishauri Serikali, lipo eneo ambalo hatujawekeza kabisa na kuna fedha nyingi na wenzetu wananufaika sana. Nchi yetu imebahatika kuwa na misitu mingi na sasa hivi tunapata fedha nyingi kwa sababu dunia nzima wanahamasa kubwa ya uvunaji wa hewa ya ukaa, kwa sababu mataifa ya nje yameharibu hali ya hewa huko duniani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa fursa tuliyonayo sisi Watanzania hatujaitumia vizuri kabisa. Ninao mfano, Nchi jirani ya Kenya, wenzetu wanavuna hewa ya ukaa kwa mwaka wanapata dola bilioni moja ambazo wanazivuna kupitia kwenye hifadhi zao. Sisi nchi yetu Tanzania ina maeneo makubwa mno karibu kila sehemu tuna Hifadhi za Taifa, tuna misitu inayomilikiwa na *TFS,* tuna misitu inayomilikiwa na vijiji, nchi yetu tu tunao uwezo wa kuvuna karibu tani zinazoweza kutoa shilingi trilioni 6.9 kwa mwaka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tungepata hizi fedha zingeweza kutusaidia kuepukana kuwakamua wananchi kupitia kwenye mafuta, lakini bahati mbaya Wizara hawajatoka ofisini na hatujazitumia Balozi zetu zilizoko huko nje. Nimwombe sana Mheshimiwa Waziri, eneo hili lina fedha nyingi na inawezekana mkawa mnaona kama hadithi. Nchi ya Brazil inavuna hewa ya ukaa na asilimia kubwa wanatumia hizo fedha kwa ajili ya maendeleo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimetolea mfano Nchi jirani ya Kenya, wao wanavuna hewa ya ukaa karibu dola bilioni moja. Sisi tuna nafasi ya kufika dola bilioni tatu ambazo zinaweza kutupelekea shilingi trilioni 6.9. Tunao mfano ambao kwa nchi yetu tayari walishaanza kuvuna hewa ya ukaa. Katika Jimbo langu wanavuna hewa ya ukaa kupitia misitu ambayo ipo, kati ya shilingi bilioni nne na wanaweza kufika mpaka bilioni 30 na kuachana na utegemezi wa kutegemea Serikali Kuu. Eneo hili ni eneo muhimu, waendeni wakajifunze. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Pakistan baada ya kupata tatizo la mafuriko, yale maeneo ambayo walihama wananchi wao saa hizi wanayatumia kwa ajili ya uvunaji wa hewa ya ukaa. Mheshimiwa Waziri aende akalifanyie kazi eneo hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunayo aina tatu za uvunaji wa hewa ya ukaa na inawezekana hata kwenye Wizara yake Mheshimiwa Waziri hajui hivi vyanzo. Kuna *soil carbon* ambayo inazalisha *organic* kwenye eneo la *agriculture,* wanaweza kupata fedha huko. Kuna eneo lingine ambalo ni kwenye *blue carbon* inayopatikana kwenye Maziwa Makuu na ufukwe wa Bahari, katika maeneo hayo yote wanaweza wakapata fedha hizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vile vile tunayo *green carbon* ambayo inaweza ikazalisha fedha nyingi kupitia misitu tuliyonayo. Maeneo haya Serikali haijawahi kuyafanyia kazi, tunakaa tu kwa ajili ya kuhakikisha wanyama wanaongezeka na wakiongezeka ndiyo wanaoenda kuleta shida kwa wananchi, kula mazao ya wananchi. Eneo hili Waziri aende kulifanyia kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, najua wana mipango mizuri ambayo Serikali wanategemea kupeleka fedha. Mimi kwenye eneo langu Jimbo la Mpanda Vijijini, tunayo Barabara ya kutoka Kabungu kwenda Kalema, Serikali wamewekeza ujenzi mkubwa sana wa bandari karibu shilingi bilioni 48. Zile fedha ni kama wameenda kuzi-*dump,* muhimu ni kujenga ile barabara ili waweze kuunganisha na nchi jirani ya DRC, Congo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na hayo wenzangu wa Mikoa ya Rukwa, Katavi na Kigoma wamezungumzia umuhimu wa kuwepo kwa meli itakayofanya shughuli za maendeleo kwenye Ziwa Tanganyika. Ziwa Tanganyika ndiyo pekee ambalo halina usafiri wa aina yoyote na kwenye maeneo ambayo yana mzigo mkubwa sana ni Ziwa Tanganyika, tunayo Bandari ya Kasanga ambayo ikitumika vizuri itaunganisha na eneo la Lubumbashi upande wa Congo, Bandari ya Kalema yatakayounganishwa na Mji wa Kalemie, lakini tunayo Bandari ile ya Kigoma itakayounganisha na nchi ya Burundi na Kongo ya Mashariki kwa maana ya Miji ya Uvila na Goma wanaweza wakatumia hiyo na tukatengeneza uchumi mkubwa sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naishauri Serikali tujenge barabara ya haraka na ya dharura ili iweze kuunganisha na ile bandari ambayo tumeijenga kwenye maeneo yale.

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo lingine ambalo tunaomba kwa Mheshimiwa Waziri, tunaomba fedha za dharura za Mkoa wa Katavi, Mkoa wa Katavi kwa sasa hauna umeme. Tunaishukuru Serikali ilileta jenereta, lakini kadri ya idadi ya watu na shughuli za maendeleo zinavyokuwa tayari Mkoa wa Katavi una shida kubwa sana ya upatikanaji wa umeme. Nimwombe Mheshimiwa Waziri kwenye hii bajeti wapeleke jenereta mpya ambayo inaweza kwenda kusaidia na kutatua kero ya wananchi. Wakati tunasubiri ule mradi mkubwa wa Gridi ya Taifa bado kuna haja ya kupeleka umeme wa dharura kwenye eneo hilo ambalo litasaidia ukuaji wa kiuchumi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimalizie kwa kuiomba Serikali kujenga mradi mkubwa wa maji. Nimwombe Mheshimiwa Waziri wa Fedha ampe Waziri wa Maji ajenge Mradi mkubwa wa Maji kutoka Ziwa Tanganyika kuleta Makao Makuu ya Mkoa pale Mpanda Mjini. Watakuwa wamewasadia wananchi na hilo linawezekana, kama maji wanayatoa Ziwa Victoria na wana mpango wa kuyafikisha mpaka Dodoma ambako ni eneo la kilometa nyingi zaidi ya kutoka pale, kutoka Mji wa Kalema hadi Mpanda ambao ni kama kilometa 100. Nina imani Serikali ikiwa na dhamira ya dhati wanaweza wakawasaidia wananchi wa Mkoa wa Katavi na wao wakanufaika na keki ya Taifa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikushukuru sana, lakini narudia kuisisitiza Serikali, wapate mawazo kutoka kwa watu wa chini, wana uwezo kabisa wa kuweza kupata mbadala wa fedha. Mawazo ya Wabunge tunapoishauri Serikali kwamba iache kukamua watu hapa, kuna eneo lingine walifanyie kazi, huko ndiko ambako tunaishauri Serikali. Naamini na nina uhakika, chanzo hiki cha mapato wakikitumia vizuri Serikali watapata fedha nyingi na wana uwezo mkubwa sana wa kukusanya mapato na nchi ikanufaika, ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Moshi Selemani Kakoso, pamoja na wachangiaji wote ambao mmechangia kwa siku ya leo. Naamini kwamba Serikali yote imo humu ndani akiwemo Waziri mwenye dhamana, Naibu Waziri, Mawaziri wengine akiwemo pia Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu. Kwa hiyo msiwe na hofu sana, naamini yote ambayo mmeyasema

Mheshimiwa Waziri na timu yake wameyapokea kwa uzito unaostahiki.

Waheshimiwa Wabunge, kabla sijafunga shughuli za leo kuna matangazo ya wageni.

Tuna wageni 19 ambao ni Maafisa Habari, Mawasiliano na Uhusiano kutoka Serikali ya Mapinduzi Zanzibar wakiongozwa na Mkurugenzi wa Idara ya Habari Maelezo, Zanzibar, Ndugu Hassan Khatibu, karibuni sana wageni wetu ambao ni Maafisa Habari kutoka kule Habari Maelezo, Zanzibar katika Bunge letu. *(Makofi)*

Pia tuna wanafunzi 80 kutoka Chuo cha Serikali za Mitaa Hombolo, Kampasi ya Dodoma Mjini wakiongozwa na Dkt. Ismail Kaudunde, Meneja wa Kampasi, karibuni sana wanafunzi ambao mnatoka Chuo chetu cha Serikali za Mitaa - Hombolo hapa Jijini Dodoma. *(Makofi)*

Vilevile tuna wanafunzi tisa kutoka Chuo cha Elimu ya Biashara *(CBE)* cha Jijini Dodoma pia. Wale pale karibuni sana kwa ujumla wenu wanafunzi wote ambao mmekuja kututembelea leo hapa, karibuni katika Bunge letu. *(Makofi)*

Tuna tangazo kutoka kwa Katibu wa Bunge ambaye anasema kwamba niwakumbushe Waheshimiwa Wabunge kuwa mabadiliko ya uendeshaji wa shughuli za Bunge kutoka matumizi ya nakala ngumu kwenda Bunge Mtandao yalienda sambamba na mabadiliko ya namna ya uwasilishaji wa taarifa na nyaraka mbalimbali za Bunge ikiwemo uwasilishaji wa hoja mbalimbali na taarifa kama vile maswali ya Bunge na michango ya maandishi kwa Wabunge ambao wanachangia hoja kwa maandishi. Aidha, mpaka sasa wapo baadhi ya Waheshimiwa Wabunge ambao wameendelea na matumizi ya uwasilishaji wa nyaraka hizo kwa kutumia nakala ngumu badala ya kutumia Mfumo wa Bunge Mtandao.

Hali hii imesababisha changamoto ya kuratibu nyaraka hizo na kushindwa kuwafikia wahusika kwa wakati. Mfumo wa Bunge Mtandao umetengenezwa kuwezesha nyaraka kuwafikia wahusika wote kwa wakati. Mfano, unapotuma mchango wa

maandishi kupitia Bunge Mtandao mchango huo huelekezwa wakati huo huo kwenda Idara ya Taarifa Rasmi za Bunge, Idara ya Shughuli za Bunge, Mtoa hoja Waziri au Naibu Waziri au Mwenyekiti wa Kamati au Mbunge pamoja na Maafisa wanaohususika na uratibu wa hoja hiyo.

Hivyo Waheshimiwa Wabunge wote mnakumbushwa kuhusu matumizi ya Bunge Mtandao wakati wa kuwasilisha nyaraka hizo hususan michango ya maandishi ili kurahisisha uratibu wa kuwafikia wahusika kwa wakati na hatimaye mchango huo kufanyiwa kazi na kupata majibu stahiki. Nafikiri tumeelewana.

Tunaambiwa pia namna ya kuchangia kwa maandishi ili kutuma mchango wa maandishi Mheshimiwa Mbunge anapaswa kufuata hatua zifuatazo; atafungua Mfumo wa Bunge Mtandao kupitia Kishikwambi, kisha atafungua dirisha la Shughuli za Bunge, kisha atabonyeza maandishi yaliyoandikwa mchango wa maandishi, kisha atabonyeza kisanduku cha toa mchango. Baadaye atachagua hoja ya kuchangia, kisha ataweka mchango wa maandishi kwenye kisanduku kilichoandikwa andika mchango wako hapa na mwisho atabonyeza wasilisha ili kutuma mchango wa maandishi.

Ikiwa Mheshimiwa Mbunge atapata changamoto kwenye matumizi ya Bunge Mtandao ataomba msaada kwa Wataalamu wa TEHAMA ambao wanakuwepo Bungeni wakati wote wa vikao vya Bunge.

Waheshimiwa Wabunge, msione aibu kama unakwama, unaenda tu kuuliza. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, pia kuna tangazo lingine ambalo mnakumbushwa kuwa, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI) inaendelea na zoezi la ukusanyaji wa maoni juu ya Ujenzi wa Ofisi za Waheshimiwa Wabunge katika Majimbo ya Tanzania Bara. Katika kufanikisha zoezi hilo TAMISEMI imeandaa dodoso la ujenzi wa ofisi hizo ili kupata maoni kutoka kwa Waheshimiwa Wabunge ili kusaidia kufanya maamuzi ya suala hilo. Dodoso hilo litatagawiwa, nafikiri limeshagawiwa kwa kila

Mbunge na baada ya kujaza lirejeshwe kupitia Wahudumu wa Ukumbini.

Waheshimiwa Wabunge, wote wa Tanzania Bara mnaombwa kujaza dodoso hilo. Nafikiri wote mnayo barua hii na dodoso zake.

Waheshimiwa Wabunge, nafikiri tumemaliza kwa leo…

**MHE. KUNTI Y. MAJALA:** Mwongozo wa Kiti.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Kunti, nafikiri wewe ni Mbunge mzoefu yaani huku tunamaliza Shughuli za Bunge na wewe unaomba mwongozo. Kwa hiyo, naomba usamehe tu leo.

Baada ya kusema hayo, nawatakia kila la kheri na naahirisha Shughuli za Bunge hadi kesho saa 3.00 asubuhi. *(Makofi)*

*(Saa 12.43 Jioni Bunge liliahirishwa hadi Siku ya Jumatano, Tarehe 21 Juni, 2023 Saa Tatu Asubuhi)*